**Set1**
**101/1**
**Karatasi ya 1**
**(Insha)**
**Saa: 13/4**

**Maagizo**

(i) Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima
(ii) Chagua insha moja nyingine kutoka hizo tatu zilizobaki
(iii) Kila insha isipungue maneno 400.
(iv) Kila insha ina alama 20

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

1. Wewe ni katibu wa kamati iliyoteuliwa na rais kuchunguza chanzo cha kudorora kwa usalama nchini. Kamati imepewa muda wa miezi mitatu kuwasilisha ripoti.

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Andika ripoti miliowasilisha.

2. Utelekezaji wa mtoto wa kiume katika nchini ni janga kuu. Jadili.
3. Mpiga mbizi nchi kavu huchunua usowe.
4. Andika insha inayomalizia kwa:

.... Alianza kubabaika kijasho kikaanza kumtoka kwapani. Nikatambua moja kwa moja kuwa yeye ndiye mkosa!

# Set1

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya Pili**
**(LUGHA)**

---

**1. <u>UFAHAMU (ALAMA 15)</u>**

***Soma kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Lugha inaweza kuelezwa kwa jumla kuwa ni mfumo wa kueleza chanzo au kiini cha mawasiliano na sote tunakubaliana kuwa matumizi yake yameanza tangu kuumbwa kwa binadamu kwani ni vigumu kukisia kuwepo kwa jamii ya watu bila lugha ya mawasiliano yoyote ile.

Katika taifa lolote,huwepo na lugha moja au hata zaidi ya moja ambayo huwa ndicho chombo zatika cha mawasiliano ya taifa katika nyanja za:elimu, maandishi, siasa na biashara.Kwa mfano mataifa ya Kanada hutumia lugha mbili kwa usawa kama lugha za taifa na za kikazi. Maana ya lugha ya taifa ni lugha moja ambayo huteuliwa kutumika katika shughuli zote za taifa hasa katika nchi yenye lugha nyingi za kikabila. Lugha ya taifa ni muhimu sana kwa maisha na maendeleo ya taifa lolote lile.Lugha hii huwa ndiyo kiungo cha kueneza umoja na uelewano miongoni mwa jamii nyingi tofauti na huwa kama kitambulisho kwao kwa kuwa wao ni ndugu wa jamii moja kubwa, yaani taifa lao.

Kenya ni mfano mzuri wa taifa lenye lugha nyingi zinazozidi 40 za vikundi vidogo vidogo vya kikabila.Hapo kabla ya miaka mia moja hivi iliyopita kila kimojawapo cha vikundi hivi kilijitambulisha kama taifa huru.Baada ya kuja kwa serikali ya kikoloni na hasa baada ya Kenya kujinyakulia uhuru,haja ya kuunganisha raia wote chini ya taifa moja lenye uongozi na shabaha moja lilikuwa ndilo jambo lililozingatiwa sana.Kwa hivyo utamaduni wa taifa la Kenya ni mchanganyiko wa tamaduni za watu wengi wenye mila,desturi,imani na itikadi tofauti. Utamaduni humaanisha jumla ya amali na tabia za watu wa jamii fulani. Amali hizi zinafungamanisha fikira, ustaarabu, mila, taasisi na sanaa za aina zote za jamii inayohusika. Ili kujieneza na kujiimarisha,taifa huhitaji chombo hicho kuwasiliana na kuwaunganisha watu wake wenye asili mbalimbali.Chombo hicho huwa ni lugha ambayo siyo tu kwamba ni sehemu ya utamaduni wa jamii bali pia ni njia muhimu sana ya kutawanyia na kustawishia ule utamaduni.

Katika taifa lenye lugha nyingi kama Kenya kwa mfano,lugha ya taifa inayozungumzwa na kueleweka na idadi kubwa ya raia ambayo imekiuka mipaka na tofauti za kikabila ni njia muhimu sana ya kueneza maongozi ya taifa, bendera ya taifa, ndicho kielelezo cha taifa lolote lile lililo huru. Lugha kama hiyo huvunja na hukomesha hisia za kibinafsi na kikabila na badala yake kuunda moyo wa uaminifu wa kitaifa.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Zaidi ya kuwa chombo cha mawasiliano, lugha ni kielelezo cha fikira na hisia za binadamu.Lugha ya watu fulani haituelezi tu ujuzi au maarifa yao bali pia mtazamo wao kimaisha, falsafa na mawazo yao. Kwa ufupi lugha hutufahamisha namna akili za watu waizungumzayo ile lugha zinavyofikiri na kutafanya maazimio.Lugha ni sehemu ya utamaduni wa taifa ilimozaliwa na lazima lugha hiyo ifunzwe katika muktadha wa maisha ya jamii ihusikayo.Utamaduni wa jamii havitenganiki na lugha yake.

**MASWALI**

a) Ni nini fasiri ya neno lugha? (alama 2)
b) Tofautisha baina ya lugha ya taifa na lugha ya kikazi. (alama 2)
c) Kwa nini lugha ya taifa huhitajika sana katika nchi kama Kenya? (alama 2)
d) Taja kazi **tatu** kuu zinazotekelezwa na lugha ya taifa. (alama 3)
e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na taarifa. (alama 3)
   (i) Haiyamkiniki:
   (ii) Amali na tabia za watu :
   (iii) Kielelezo:
   (iv) Muktadha wa maisha ya jamii:
f) Eleza majukumu mawili ya lugha kwa ujumla. (alama 2)

for freepast papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**2. UFUPISHO: (ALAMA 15)**

***Soma kifungu kifuatasho kisha ujibu maswali.***

Kwa kawaida, binadamu huishi kwa kutangamana na binadamu wenzake. Katika kutangamana huku, watu huathiriwa kitabia, kifikira, kimavazi na kimaisha kwa jumla. Watu wote katika jamii wana uwezo wa kuathiri na kuathiriwa na wenzao wa umri mmoja. Hata hivyo, walio katika hatari ya kuathiriwa zaidi na mahirimu wao ni vijana. Hali hii ya kuathiriana huitwa shinikizo-rika au shinikizo-marika. Vijana huaminiana na kuthaminiana sana. Kwa sababu hiyo, ni rahisi sana kuingizwa katika mitego na wenzao. Isiaminiwe kuwa vijana pekee ndio wanaoathiriwa na shinikizo-rika. La hasha! Watu wazima pia huwafuata wenzao mithili ya bendera kufuata upepo. Mwenzake akinunua gari, yeye pia hukimbilia mkopo kununua gari la sampuli iyo hiyo bila kuwazia kima cha kibindo chake.

Wataalamu wa saikolojia husema kuwa kukabiliana na tatizo la shinikizo-rika si rahisi kwa sababu shinikizo-rika huleta mtafaruku wa kinafsi akilini mwa anayeathiriwa. Nafsi moja humshawishi kufuata wenzake huku nyingine ikimnasihi kuandamana upekee au ubinafsi wake. Shinikizo-rika huathiri sana mahitaji ya kisingi ya binadamu. Ikumbukwe kuwa mahitaji haya ya kimsingi ni ya kila mwanadamu, nayo ni kama vile kupata lishe, hewa safi, kupenda na kupendwa miongoni mwa mengine. Kila mtu hutaka kujihusisha na kundi la watu ambao watamfanya kuhisi kuthaminiwa na kukubalika. Kutokana na haja ya kutaka kukubalika, anayetaka kutambuliwa huridhia matakwa ya wenzake bila hata kuyawazia.

Shinikizo-rika hujittokeza kwa sura nyingi. Mathalani, vijana huwafanya wenzao kuona kuwa wana hatia wasipoafiki kutekeleza kama wanavyoshinikizwa. Kauli kama vile 'tulifikiri wewe ni mmoja wetu' au 'usiposhirikiana nasi utakuwa umetuvunja moyo' hutamalaki. Wanaokataa kushinikizwa hubezwa na kufanyiwa stihizai na wenzao na hata kutengwa. Vitisho hutolewa, wakati mwingine, na anayeshinikiswa akidinda, mabavu hutumika.

Ni muhimu kwa watu, hasa vijana, kufahamu kuwa shinikizo-rika lipo na wanapokabiliwa na tatizo hilo, watambue kuwa wana haki ya kusimama kidete kutetea msimamo wao dhidi ya wenzao. Kumbuka, baridi huwazizima kondoo kwa namna tofauti.

Kama njia moja ya kukabiliana na shinikizo-rika, wanasaikolojia wanapendekeza watu kujiamini na kuelewa kwamba wana haki ya kuwa tofauti na kuwa na upekee wao. Mtu anapojiamini na kushikilia msimamo wake, anaweza kujiepusha na madhara yatokanayo na shinikizo-rika. Asiyejiamini huwa mwepesi sana wa kuingizwa katika lindi la mashaka na wenzake.

**Maswali**

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

(a) Bila kupoteza maana, fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa **maneno (40)**.
**(alama 8, 1 ya utiririko)**

<u>**Nakala chafu**</u>

<u>**Jibu**</u>

(b) Fupisha mambo muhimu ambayo mwandishi amezingatia katika aya tatu za mwisho.
(maneno 30)

**3. <u>MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 4)</u>**

(a) Tofautisha kati ya: (i) / e / (ii) / u /(alama 2)

(b) Onyesha **muundo** wa **silabi** ya kwanza katika maneno yafuatayo: (alama 2)
(i) Nyakua
(ii) Chura

(c) Tunga sentensi kwa kutumia kibadala cha kiasi jumla. (alama 2)

(d) Changanua sentensi ifuatao kwa kutumia **jedwali**. (alama 4)
Mkongojo mrefu sana ulioletewa babu utauzwa na fundi mcheshi.

(e) Andika **kinyume** cha sentensi ifuatayo:
Mtoto msichana anathema dawa. (alama 2)

(f) Kanusha: (alama 2)
Nikimpiku masomoni nitatuzwa zawadi.

(g) Andika katika usemi halisi. (alama 3)
Chifu wetu alitwambia kuwa watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa wezi wa mabavu.

(h) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni. (alama 2)
(i) (-la) (kauli tendeshea)
(ii) Toa (tendeka)

(i) Eleza matumizi ya alama zifuatazo za uakifishi. (alama 2)
(i) **!**
(ii) **?**

(j) Bainisha mofimu **–Li-** katika tungo hili. (alama 3)
Alivyolikimbilia

(k) Tunga sentensi moja yenye shamirisho hizi. (alama 3)
(i) Kipozi
(ii) Kitondo
(iii) Ala

(l) Ainisha vishazi. (alama 2)
Mhamiaji haramu aliyeshikwa amefikishwa mahakamani.

(m) Andika katika wingi <u>karibu</u>. (alama 2)
Mtu yuyo huyo aliubeba mzigo uo huo licha ya kukanywa.

(n) Andika sentensi ifuatayo katika watati ujao timilifu. (alama 2)
Mbunge alitawazwa kabla ya mpinzani wake kufika.

(o) Andika kwa wastani. (alama 1)
Magoma haya yatachezwa wanjani.

(p) Taja na utoe mifano, matumizi <u>mawili</u> ya kiimbo. (alama 4)

(q) Eleza maana mbili za sentensi. (alama 2)
Nenda ukaniletee mbuzi.

**4. <u>SEHEMU YA D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)</u>**

(a) Eleza mitazamo mine kuhusu chimbuko la Kiswahili. (alama 4)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

(b) Eleza njia za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. (alama 6)

## Set1

**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

1. **SWALI LA LAZIMA**
   MSTAHIKI MEYA
   Uvundo haswa! Hata wageni sijui wataonaje hali hii. Aibu kubwa inatungojea kama watakuja!
a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b. Jadili hulka zozote **mbili** za msemaji zinazojiktokeza katika muktadha huu. (alama 4)
c. Thibitisha kuwa Cheneo ilikuwa imejaa 'uvundo.' (alama 12)

**SEHEMU YA B: RIWAYA:**
**KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA**
***Jibu swali la 2 au 3***

2. Ujenzi wa jamii mpya ni wajibu wa vijana. Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)
   AU
3. "Lowela tunapendana mno na ni msiri wangu wala hakuogopa kuniambia yaliyojiri.
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Fafanua 'yaliyojiri' kwa mujibu wa msemaji. (alama 8)
   (c) Lowela ni kielelezo kibaya cha msichana wa kisasa. Thibitisha. (alama 8)

**SEHEMU C: HADITHI FUPI: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**
***Jibu swali la 4 au 5***

4. Eleza kwa Kutolea mifano uozo wa jamii katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine. (alama 20)
   AU
5. Kanda la Usufi.
   Muhula wa tatu wa kidato ulipoanza alijiunga na wanafunzi wengine.
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Eleza dhana ya utatu katika hadithi Kanda la Usufi. (alama 4)
   (c) Thibitisha ukweli wa methali hii 'mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi. (alama 8)
   (d) Eleza umuhimu wa mhusika mkuu katika hadithi. (alama 4)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**
***Jibu swali la 6 au 7***

6. **Soma shairi hili kasha ujibu maswali yanayofuata:**
   Jukwani naingia, huku hapa pasokota,
   Kwa uchungu ninalia, hii tumbo nitaikata,
   Msiba mejiletea, nimekila kiso takata,

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wazee hata vijana,wote umewasubua,
Huruma nao hauna, heshima kawakosea,
Ukambani na Sagana, hata mbwa wararua,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wahasibu ofisini,kibwebwe mejifunga,
Miaka mingi vitabuni, ili wasikose unga,
Nadhari wanadhamini, hesabu wanazirenga,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wapenzi wa kiholela, pia wanakuogopa,
Baada yao kulala, wana wao wanatupa,
Wakihitaji chakula, wanachokora mapipa,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wafugaji hata nao, kama dawa wakwamini,
Hawajali jiranio, wamesusia amani,
Wanaiba ng'ombe wao, na kuzua kisirani,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Nayo mizozo ya maji, kaonekana kwa mara,
Hiyo nayo ni dibaji, sababu sio harara,
Njaa wahepe wenyeji, huo ndio mkarara,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Ningeweza kukuuza, ingekuwa siku njema,
Tena kwa bei ya meza, sokoni nimesimama,
Wala tena singewaza, kuhusu wali na sima,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?
Hatima umefikika, naenda zangu nikale,
Mate yanidondoka, kwa mnukio wa wale,
Naomba kwenda kukaa, wala sio nikalale,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Maswali**

(i) Lipe anwani mwafaka shairi hili. (alama 2)
(ii) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (alama 2)
(iii) Huku ukitolea mifano mwafaka, taja arudhi zilizotumiwa katika ubeti wa tatu. (alama 4)
(iv) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)
(v) Thibitisha kuwepo kwa idhini ya ushairi. (alama 2)

(vi) Taja madhila anayoelezea mtunzi wa shairi hili yaletwayo na tumbo. (alama 4)
(vii) Elezea maana ya maneno yafuatayo. (alama 2)
(a) Dibaji
(b) Harara
AU

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

7. **FASIHI SIMULIZI.**
   i. (i) Eleza maana ya misimu. (alama 2)
      (ii) Eleza dhima ya misimu. (alama 4)
   ii. Taja aina **nne** za ngomezi za kisasa. (alama 4)
   iii. Eleza sifa **nne** za maapizo. (alama 4)
   iv. Eleza kikwazo **vitatu** vinavyokumba Fasihi simulizi. (alama 6)

# Set2

**102/1**
**INSHA**
**KARATASI YA 1**

---

**Swali la Lazima.**

1. Mwandikie barua pepe rafiki yako anayeishi nchi jirani ili ahudhurie siku ya arusi yako. Barua pepe hiyo iandamane na ratiba ya siku hiyo.

2. Jadili hatua zinazoweza kuchukuliwa kukabiliana na ukabila nchini Kenya.

3. Andika kisa kinachothibitisha ukweli wa methali painamapo ndipo painukapo.

4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
   Nilijaribu kuuinua mguu wangu uliojaa maumivu kutokana na jeraha …

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

# Set2

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

---

**SEHEMU A: UFAHAMU (ALAMA 15)**
**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Ni fedheha kuona taifa ambalo halijakuwa likitambua msamiati wa shibe kwa zaidi ya miongo miwili sasa limeacha chakula kiharibike mashambani kutokana na ukosefu wa soko. Taarifa kuwa ni zamu ya wakulima wa mahindi kukadiria hasara baada ya wenzao wa maziwa ni za kuhuzunisha. Inasemekana wakulima wa zao la mahindi katika mikoa ya pwani, mashariki, kati na Bonde la ufa wanendelea kuhesabu hasara kutokana na ukosefu wa soko la mahindi kutoka kwa serikali.

Hii ni hata baada ya serikali kuwapatia na kuwauzia pembejeo kwa bei nafuu kama njia mojawapo ya kuimarisha uzalishaji wa chakula nchini. Kinachovunja moyo zaidi ni habari kuwa serikali iyo hiyo ilitoa ahadi ya kununua mazao yote ya wakulima hao kama njia mojawapo ya kuwatia moyo katika kazi yao.

Kando na wakulima wa kibinafsi, ilitumia mamilioni ya pesa za umma kuzindua miradi ya kilimo cha mahindi kwa kunyunyizia mashamba maji na mazao yake pia yanaharibikia. Wakulima wa mradi wa kilimo cha kunyunyizia mashamba wa Hola, kwa mfano, wameathirika pakubwa kutokana na ukosefu

wa soko la mazao yao. Imekuwa ikijikokota kutokana na sababu kadhaa ikiwemo ukosefu wa fedha za kununua mahindi.

Hii ni hata baada ya uchunguzi kuonyesha kuwa usalama wa chakula nchini umedorora kutokana na kiangazi cha muda mrefu. Mbali na kutokuwepo kwa utaratibu wa kununua mahindi kutoka kwa wakulima hao halmashauri ya nafaka haina uwezo wa kuwashughulikia wakulima wote nchini.

Hii ni kwa sababu wakulima wengi hawapati huduma za halmashauri hiyo ambayo imejikita katika maeneo yaliyokuwa yakizalisha chakula kwa wingi miaka iliyopita. Eneo la Hola, kwa mfano, liko mbali kutoka kwa kituo cha halmashauri hiyo kwa sababu eneo hilo ni kame.

Ni kutokana na muktadha huu serikali inapaswa ichukue hatua za haraka kuepusha kuharibika kwa zao la mahindi nchini. Serikali inapaswa kutenga fedha zaidi za kununua mahindi kutoka kwa wakulima. Inakisiwa kuwa hasara zaidi inatarajiwa kutokea ikiwa pesa zaidi hazitatengwa kwa sababu idadi ya wakulima wanaovuna mahindi inatarajiwa kuongezeka.

***Maswali***

1. (a) Kwa nini chakula kinaharibikia mashambani? (alama 2)
   (b) Serikali ilichangia vipi katika kuimarisha uzalishaji wa chakula? (alama 2)
   (c) Eleza vile halmashari ya nafaka haijaweza kuepushia wakulima wa mahindi hasara. (alama 1)
   (d) Kwa nini wakulima wa maeneo kame hawajashughulikiwa na halmashuri ya nafaka?(alama 1)
   (e) Kutokana na taarifa hii serikali inaweza kutatua tatizo la wakulima kwa njia gan (alama 1)
   (f) Pendekeza namna taifa linaweza kuepuka na kupambana na uharibifu wa chakula mashambani. (alama 3)
   (g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 3)
      (i) Miongo
      (ii) Pembejeo
      (iii) Umedorora

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**<u>SEHEMU YA B: UFUPISHO: (ALAMA 15)</u>**
**<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata:</u>**

Katika safu yangu hii sina lengo la kuzishambulia dini zetu na namuomba
Mungu sana asiniandikie dhambi kutokana na ninayotaka kuyaandika. Lakini nashawishika kuikumbusha jamii yangu ambayo inatufanya watu tuzione dini zetu zinamkandamiza mwanamke. Dini zetu kubwa kama Uislamu na Ukristo zinatuelekeza mwanamke kumheshimu mumewe na kumsikiliza anachosema, lakini kwa yeye kufuata maadili ya dini na si kukuambia uue ukakubali.

Wakati dini inasema utekeleze amri ya mumeo na wao wameelezwa mambo ya kuwafanyia wanawake, ikiwa ni pamoja na kuwaheshima na kuwaridhisha kadri ya uwezo wao.

Kutokana na hilo la amri, wanaume wengi ndio wamechukua kama tiketi ya kunyanyasa mwanamke na hata kumnyima fursa ya kujiendeleza kielimu na hata kufanya shughuli za kuongeza kipato. Unakuta familia ni ya kimaskini, baba hana fedha za kutosha kuihudumia familia yake, lakini baba huyo anataka kujishughulisha
na shughuli yoyote ya kumuingizia kipato kinachoweza kuwasaidia wote na matokeo yake kuendelea kuwepo, kwenye dimbwi la umasikini. Wengine kwa hofu ya kupata changamoto kutoka kwa wake zao wanawakatalia wanawake walio wao kujiendeleza kielimu au kutafuta mwanamke asiyeelimika ili asiweze kuhoji mambo kadhaa ndani ya nyumba.

Hili limebainishwa hivi karibuni na shirika moja lisilo la kiserikali huko kigoma ambapo katika utafiti wao asilimia 90% ya wanawake wa vijijini wanashindwa kutoa hoja kutokana na uelewa wao

duni na kutoa sababu ya kuwa hiyo ni kutokana na ukosefu wa elimu, masuala ya kidini yanayomwelekeza mwanamke kufuata amri za mumewe, mila na desturi kadhaa.

Dini zote zinaeleza wazi umuhimu wa mtu kupata elimu bila kubagua kama ya kiislamu inavyosema; mtu anapata thawabu anapotafuta elimu na anatakiwa aitafute popote bila kujali umbali na hata ikiwezekana kufika China ambapo inaaminika ni mbali.

Sijawahi kuona wala kusikia dini ikisema mwanamke asipate elimu lakini baba zangu na kaka zangu wanaume wanalipotosha hili kutaka kuendelea kumkandamiza mwanamke bila kufikiri kuwa mwanamke ni msaada mkubwa kwao na kwa maendeleo ya taifa lote; ikiwa leo tupo katika harakati za kupata maendeleo na nchi hii hivi kweli tutafanikiwa?

Mapambano ya kuleta maendeleo yaanze katika ngazi ya familia kwa kuondoka kwa ujinga wa kumkandamiza mwanamke ili naye aelimike, aweze kujenga hoja, aweze kujitafutia kipato na mwisho kusaidia katika maendeleo ya familia ambayo kwa njia nyingine ndiyo maendeleo yenyewe ya taifa hili.

(a) Fupisha aya tano za kwanza. **(Maneno 70).**
(b) Mwanamke anaweza kuendelezwa vipi. Rejelea aya mbili za mwisho. **(Maneno 50)**.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

## SEHEMU YA C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

A Taja aina **mbili** kuu za ala za sauti kisha utoe mfano mmoja mmoja. (alama 2)

B Taja maneno yenye **miundo** ifuatayo ya silabi. (alama 2)
  (i) KKKI
  (ii) Irabu pekee (II)

C Eleza ni kwa nini neno umma ni la asili ya kigeni. (alama 1)

D Viambishi vilivyopigiwa **mstari** vinawakilisha dhana zipi za kisarufi? (alama 2)
  (i) Udhaifu
  (ii) Walani?

E Neno lifuatalo liko katika ngeli gani? (alama 1)
  (i) Matukio

F Andika kwa **msemo** wa taarifa: (alama 2)
  Askari: Ulikuwa unaelekea wapi uliposhambuliwa?
  Jirani: Nilikuwa nikienda sokoni jana.

G Onyesha **vishazi** katika sentensi ifuatayo kisha **uelezee** ni vya aina gani. (alama 2)
  Ajapo tutamlaki kwa shangwe.

H **Sahihisha** sentensi ifuatayo.
  Mtu ambaye aliyechukua kitabu chenye kilikuwa hapa arudishe. (alama 1)

I Tumia mzizi **–w-** katika sentensi kama: (alama 2)
  (i) Kitenzi kisaidizi.
  (ii) Kitenzi Kishirikishi.

J Tunga sentensi moja kubainisha matumizi ya **'na'** kama. (alama 2)
  (i) Kihusishi cha 'na' ya mtenda.
  (ii) Kiunganishi

K Weka kirejeshi **'O'** tamati kwenye kitenzi **chunga** kisha ukitungie sentensi. (alama 1)

L Eleza na utoe mifano ya mazingira **mawili** ambapo mistari mshazari hutumika. (alama 2)

M Nyambua kitenzi ja jiwe katika kauli ya kutendewa kisha **utunga** sentensi. (alama 1)

N (i) Eleza dhana ya shamirisho. (alama 1)

(ii) Onyesha aina tofauti za **shamirisho** katika sentensi hii.
Ali alimnunulia Asha viatu kwa pesa zake. (alama 2)

O Tumia kivumishi kionyeshi cha karibu pamoja na nomino katika ngeli ya I-ZI kisha utunge sentensi katika **ukubwa - wingi**. (alama 2)

P Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali **timilifu wingi**. (alama 2)
(i) Msomi hakutuzwa siku hiyo.

Q Eleza **matumizi** ya kwa katika sentensi hii. (alama 3)
(i) Kwa nini umeishi kwao kwa miaka mingi?

R Eleza maana **tatu** zinazopatikana katika sentensi hii. (alama 3)
(i) Alikuwa amenijuza kuwa angefika kwao.

S Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya **mishale**. (alama 4)
(i) Kuku na mbuzi ni mifugo.

T Eleza maana ya nomino. (alama 1)

**SEHEMU YA D: ISIMU JAMII: (ALAMA 10)**

(a) Ali: Wee kuja hapa. Wewe ni nani? Sema haraka!
Ebo: Mimi ... ni ... afande ni Ebo
Ali: Unatoka wapi sa ii? Hapa hakuna sheria?
Ebo: Samahani mkubwa. Mimi niku...
Ali: Mkubwa wa nani? Wakubwa wako ofisini.
Ebo: Pole mzee.
Ali: Mzee gani? Hii mtu lazima niiwekwa store. Yaani self-contained. Toa viatu.
Ebo: Tafadhali Bwana Askari, nilichelewa ...
Ali: Mimi sitaki hadithi! Hizo pelekea nyanya yako, eh. Fanya haraka!
Ebo: Naomba mkubwa ...
Ali: Hapa si kanisani. Unaomba! Hata ...

Fafanua sifa tano za sajili hii. (alama 5)

(b) Eleza maana ya istilahi zifuatazo za isimu jamii. (alama 5)
(i) Lugha ya taifa.
(ii) Lugha ya ishara
(iii) Lugha mwiko
(iv) Sajili za lugha
(v) Uchanganyaji msimbo.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

## Set2

**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

**SEHEMU A: USHIAIRI**
**SWALI LA LAZIMA**

1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

**LONGA**

Longa Longea afwaji, watabusarika,
Longa uwape noleji, watanusurika,
Longa nenea mabubu, sema na viduko.

Longa usichachawizwe, tamka maneno,
Longa usitatanizwe, mbwa aso meno,
Longa usidakihizwe, kishindo cha funo.

Longa yote si uasi, si tenge si noma,
Longa pasi wasiwasi, ongea kalima,
Longa ukuli kwa kasi, likate mtima,
Longa zungumza basi, liume ja uma.

Longa japo ni kombora, kwa waheshimiwa,
Longa liume wakora, kwani wezi miwa,
Longa bangu na papara, hawakuitiwa,
Longa bunge si kiwara, si medani tawa,
Longa ni simbamarara, wanaturaruwa.

***Maswali***

(a) Tambua nafsineni katika nudhumu hii. (alama 1)
(b) Onyesha vile kibali cha utunzi wa mashairi kilivyotumiwa kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)
(c) Kwa kutoa maelezo mwafaka, tambua bahari **nne** zilizotumiwa na mtunzi kwenye shairi hili. (alama 8)
(d) Onyesha vile shaha alivyofua dafu kutumia mbinu zifuatazo. (alama 5)
  (i) Anafora
  (ii) Usambamba wa kiusawe.
  (iii) Usambamba wa kifahiwa/dhamira.
  (iv) Tabaini.
  (v) Jazanda
(e) Tambua toni ya shairi hili. (alama 1)
(f) Neno kasi ni adhidadi. (alama 1)
(g) Neno afwaji limetumika kumaanisha nini katika shairi hili. (alama 1)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**SEHEMU B: MSTAHIKI MEYA**

2. "Mimi na Meya ni mfano wa mafuta na maji. Hatuonani uso kwa uso."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Ni mbinu gani ya lugha iliyotumika katika dondoo na inamaanisha nini? (alama 2)
(c) Kwa kurejelea tamthilia nzima, thibitisha kuwa Meya ni sawa na mafuta na wengine ni maji. (alama 14)

**AU**

3. Thibitisha ukweli wa msemo kuwa sikio la kufa halisikii dawa kwa mujibu wa Tamthilia ya Mstahiki Meya (alama 20)

**SEHEMU C: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**
**KANDA LA USUFI**

4. "Wanafunzi hao wawili waliandamana hadi ilipokuwa kliniki ya shule."
   (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
   (b) Kwa kurejelea hadithi kanda la usufi thibitisha kuwa sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto myingi. (alama 10)
   (c) Wanafunzi wanaorejelewa walikuwa wamekutana kisadfa. Toa mifano mingine **mitatu** ya sadfa kutoka kwenye hadithi hii. (alama 6)

   **AU**

5. **MIZIZI NA MATAWI**
   Thibitisha kuwa majina Sudi na Kudura ni ya kimajazi. (alama 20)

**SEHEMU YA D: KIDAGAA KIMEMWOZEA**

6. Mwandishi wa Kidagaa Kimemwozea amenuia kujenga jamii mpya. Tetea kauli hii. (alama 20)

   **AU**

7. "Hatimaye Tarishi alikuja na barua moja ya Mtemi na nakala ya siku hiyo ya gazeti la Tomoko Leo: Mtemi Nasaba Bora akapokea barua hiyo na gazeti toka kwa tarishi aliyekuwa kanywea si haba."

   (a) Jadili mambo yaliyomshtua Mtemi Nasaba Bora kuhusiana na barua na gazeti alizopokea siku hiyo. (alama 10)
   (b) Onyesha jinsi madhubuti alivyoendeleza uasi dhidi ya babake. (alama 10)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

8. (a) Maigizo ni nini? (alama 2)
   (b) Fafanua sifa zozote **tano** za maigizo. (alama 10)
   (c) Eleza dhima ya michezo ya watoto. (alama 8)

# Set3

**102/1**
**INSHA**
**KARATASI YA 1**

---

1. **LAZIMA.**
   Kumekuwa na visa vingi vya ukosefu wa usalama nchini. Wewe kama katibu wa jopo lililoteuliwa na Waziri wa Usalama nchini, andika ripoti kuhusu suala hili.

2. Teknolojia ya kisasa imechangia kudhurika kwa maadili ya vijana wetu. Jadili.

3. Tunga kisa kinachooana na methali ifuatayo.
   "Wema hufa mwili, hawafi jina."

4. Andika insha itakayoishia kwa
   ... Ilinichukua muda mrefu kuyaamini niliyoyaona!

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

# Set3
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

**SEHEMU YA A: UFAHAMU (ALAMA 15)**
***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Ulimwengu unapaswa kuzuka na mbinu za kulitadarukia tatizo ambalo linakwamiza juhudi za maendeleo. Umaskini unaoyakabili mataifa yanayoendelea, unayatosa kwenye dhiki kubwa huku mataifa ya kimagharibi yakipiga hatua kubwa kimaendeleo. Ufa uliopo baina ya mataifa yanayoendelea na yale yaliyoendelea kama vile Marekani, nchi za Ulaya na Ujapani unapanuka kila uchao.

Vyanzo vya umasikini huu ni anuwai mathalan, ufisadi uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika, idadi ya watu inayoupiku uwezo wa uchumi wa taifa linalohusika na ukosefu wa nyenzo na amali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini. Ukosefu wa elimu na nafasi adimu za ajira huchangia pia katika tatizo hili.

Jamii ya ulimwengu inapaswa kuelewa kuwa umaskini, unaothiri nchi fulani una athari pana sana. Uvunjifu unaotokana na umaskini unaweza kuwa mboji ambako matendo mabaya huchipuka. Raia maskini huweza kushawishiwa haraka kujitosa kwenye matendo ya kihalifu ili kujinasua kutoka dhiki ile. Hii inaweza kuwa mbegu ya kuatika maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.

Mataifa ya magharibi yanapaswa kuyaburia madeni ya mataifa yanayoendelea kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. Katika hali hii inakuwa muhali kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na pingu za umasikini. Njia nyingine ni kustahabu kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi zinazoendelea.

Kwa upande wake, mataifa yanayoendelea yanapaswa kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini. Ni muhimu pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini. Pana dharura ya kuzalisha nafasi za ajira, kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tegemeo kuu la mataifa mengi, kuendeleza elimu na kuimarisha miundo msingi. Ipo haja pia ya mataifa haya kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru unaotawala ulimwengu sasa hauishii kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umaskini zaidi. Kwa ufupi, maamuzi yote ya sera za kiuchumi lazima yauzingatie uhalisi wa maisha ya raia wa mataifa hayo.

**Maswali:**

(a) Kwa nini umaskini umetamalaki katika mataifa yanayoendelea? (alama 4)

(b) Madeni yana athari gani kwa mataifa yanayoendelea? (alama 2)

(c) Ni mapendekezo yapi ambayo mwandishi anatoa kwa mataifa machanga kuhusu utatuzi wa tatizo la umaskini? (alama 4)

(d) Mfumo wa soko huru una madhara gani kwa mataifa machanga? (alama 2)

(e) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya: (alama 3)
- (i) Kulitadarukia.
- (ii) Kuatika.

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

(iii) Kuyaburia madeni.

**SEHEMU YA B: UFUPISHO**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Kadiri jamii mbalimbali zinavyotagusana, ndivyo lugha zinazozungumzwa na jamii hizi nazo zinavyoingiliana na kuathiriana. Mojawapo ya athari hizi ni ukopaji wa msamiati. Jamii zinazopakana au kutagusana hukopa msaimiati kutoka kwa lugha jirani na kuutumia kuelezea dhana mpya zinazoingia katika utamaduni wao kupitia kwa mitagusano ya kijamii.

Lugha ya Kiingereza, kwa mfano, imekopa kutoka lugha nyingine kama vile Kifaransa na Kilatini. Mathalani, istilahi nyingi za kisheria zimekopwa kutoka lugha ya Kifaransa. Aidha, Kiingereza kimekopa kutoka lugha ya Kiswahili. Maneno ya Kiswahili kama vile mwalimu, jiko, mandazi, panga, buibui, ngoma na hata wananchi, sasa yameingia katika kamusi za Kiingereza, kumaanisha kuwa yamekubaliwa kama msamiati rasmi wa lugha ya Kiingereza.

Kiswahili nacho kimeathiriwa na lugha nyingine. Kimekopa msamiati wa Kiingereza na hata Kiarabu. Katika tungo nyingi za kishairi, kwa mfano, Utenzi wa Mwanakupona utapata msamiati wa Kiarabu uliotoholewa. Lugha nyingine ambazo zimeathiri Kiswahili ni pamoja na Kijerumani ambako msamiati kama vile 'shule' ulikopwa na kutoholewa kutokana na neno *schule*. Msamiati kama vile *'leso', 'karata' na 'mvinyo'* yamekopwa kutoka lugha ya Kireno, huku majina 'balozi' na 'bahasha' yakikopwa kutoka Kituruki.

Pamoja na ukopaji wa vipengele vya lugha, mtagusano wa lugha una athari nyingine. Lugha zinapokuja pamoja, mazingira ya wingi-lugha hazuka. Baadhi ya watu hujifunza zaidi ya lugha moja. Mtu anayeweza kuzungumza zaidi ya lugha moja anaweza kujieleza kwa urahisi kwa kuchanganya msamiati wa lugha tofauti. Aidha, anaweza kubadilisha msimbo kulingana na matilaba yake. Ikiwa anataka kukubalika na jamii-lugha anayotagusana nayo, atatumia lugha ya jamii hiyo ili kujinasibisha na kujitambulisha nayo. Wazungumzaji hupata visawe vya maneno kuelezea dhana zile zile, hivyo kuboresha mitindio yao ya mawasiliano.

Kadhalika, kutagusana kwa lugha kunaweza kusababisha kubuniwa kwa lugha ngeni ambayo inarahisisha mawasiliano. Wakati mwingine, watu wanaozungumza lugha tofauti wanapokutana, hubuni mfumo sahili wa lugha ili kufanikisha mawasiliano. **Pijini** ni mfano wa lugha iliyobuniwa kwa njia hii. Pijini huchota msamiati kutoka lugha zilizotagusana. *Sheng* ni mfano mwingine wa lugha ambayo ilibuniwa kutokana na kutagusana kwa lugha ya Kiswahili, lugha za kiasili na Kiingereza.
Japokuwa kuna faida nyingi za wingi-lugha, hasara pia zipo. Mazingira ya wingi-lugha huwapa wazungumzaji fursa ya kuchagua lugha wanayotaka kuwasiliana kwayo. Katika hali hii, lugha yenye ushawishi mkubwa kijamii, kiuchumi na kisiasa ndiyo ianyopendelewa zaidi. Wingi-lugha unaweza kusababisha kukwezwa kwa lugha moja na kudunishwa kwa lugha nyingine. Mathalani,
kuwepo kwa lugha nyingi nchini kulizua haja ya kukwezwa kwa lugha ya Kiswahili huku lugha nyingine za kiasili zikipuuzwa.

Lugha hukua kwa kutumiwa. Lugha isipozungumzwa kwa muda mrefu, watu hupoteza umilisi ambao huifanya kuwa vigumu kuirithisha kwa vizazi. Lugha inaweza pia kukosa wazungumzaji ikiwa wale wanaozungumza ni wachache, au ikaathiriwa na mtagusano na lugha nyingine iliyo na wazungumzaji wengi. Katika hali kama hii, lugha hiyo hukabiliwa na tisho la kudidimia au hata kufa. Ikiwa jamii lugha itakosa kudhibiti sera za matumizi ya lugha yake, baadhi ya lugha ama zitafifia au zitakufa na kusahaulika kabisa.

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

1. Bila kupoteza maana, fupisha aya za kwanza tatu. **(Maneno 50)** **(alama 6, 2 za mtiririko).**
2. Kwa mujibu wa taarifa hii, mtagusano wa lugha una athari gani? **(Maneno 30)**

3. **MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)**

(a) Andika sifa za **kutambulisha** sauti zifuatazo. (alama 2)
(i) /d/
(ii) /th/
(b) **Fafanua** dhana ya **mofimu**. Bainisha **mofimu** katika maneno yafuatayo. (alama 2)
(i) Samaki
(ii) Mtu
(c) Ainisha **viambishi** kwa kurejelea **majukumu** ya kisarufi katika neno hili. (alama 3)
Alijipelekea
(d) Maneno **yaliyopigiwa** mstari yametumikaje? (alama 2)
Pahali pema pako si pema pa mwenzako.
(e) Andika sentensi **mbili** kutofantisha **vitate** hii. (alama 2)
(i) Apisha
(ii) Apiza
(f) Andika sentensi ifuatayo **upya** ukibadilisha neno **lililopigiwa** mstari kuwa kivumishi. (alama 2)
Mgeni alipewa dawati mpya.
(g) Unda nomino m**bilimbili** kutokana na vitenzi hivi. (alama 2)
(i) Kagua
(ii) Hini
(h) **Kosoa** sentensi ifuatayo kisarufi. (alama 3)
Mahali kule pana siafu wengi.
(i) Tambua matumizi ya **'a'** katika sentensi ifuatayo. (alama 1)
Mwanafunzi acheza uwanjani.

(j) **Yakinisha** sentensi hii: (alama 2)
Usipofanya bidii hutapita mtihani.
(k) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya **kuamrisha.** (alama 2)
Tafadhali acheni kucheka ovyo.
(l) Andika kwa msemo wa **taarifa**: (alama 3)
"Sitakwenda sokoni leo ila nitakwenda kesho", Nikamjibu.
(m) Eleza matumizi **matatu** ya **kinyota**. (alama 3)
(n) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. (alama 4)
Mlango umevunjwa na fundi aliyeujenga.
(o) Onyesha matumizi ya **chagizo** ya **mfanano** katika sentensi. (alama 2)
Alitembea kitausi kupokea zawadi.

(p) Andika sentensi ifuatayo kwa **udogo/wingi**. (alama 2)
Mtoto mkaidi aliiba kitabu cha mwenzake.
(q) Tunga sentensi kuonyesha **matumizi** ya kiambishi **'ji'**. (alama 2)

4. **ISIMU JAMII**:
**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

"Ndugu na madada, sote tumealikwa katika karamu hii ya Bwana kabla ya kujongea mezani pake, Bwana. Pana haja ya kutakasa nyoyo zetu na kujutia madhambi yetu. Sisi sote ni watenda dhambi na inastahili kumwendea ili aweze kutuondolea madhambi yetu."

**Maswali**

(i) Weka maneno haya katika sajili yake. (alama 2)
(ii) Nini kimekufanya uchague sajili uliochagua katika swali (i). (alama 1)
(iii) Eleza sifa za matumizi lugha katika sajili hii. (alama 7)

# Set3

**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

**SEHEMU A: USHAIRI – LAZIMA**

1. **SHAIRI A**

Wewe,
Utazame mlolongo wa
Waja unaoshika njia likiwapo;
Unaofuata pembe za barabara zisokuwapo,
Kwenda kuisaka auni,
Kuitafuta kazi inayowala chenga.

Itazame migongo ya wachapa kazi,
Watokwao na jasho kapakapa na,
Wanaotafunwa uhai na jua liso
huruma:
Wakiinua vyuma na magunia,
Wakiinua makontena,
Wakichubuka mashambani,
Wakiumia viwandani,
Wakiteseka makazini,
Halafu
Uangalie ule ujira wa kijungu meko,
Mshahara usokifu haja,
Nguo zisizositiri mwili dhaifu,
Kilo chao kisichokuwa na machozi,
Na
Ujiangalie
Mwili wako unaomereta ujana wa ufanisi,
Gari lako la kifahari lililozibwa vioo,

Jumba lako la kujishasha kama uwanja mdogo,
Malaki ya pesa unayomiliki,
Ujiitapo mwajiri kwa raha, hunusi usaha wa hali yao?

**SHAIRI B**

Dunia kitendawili, hakuna ateguaye;
Dunia kama tapeli, hadaa nyingi ujuye;
Dunia mwenye akili, inampiku na yeye;
Dunia ina mizungu, tena yapika majungu.

Dunia na yake hali, hupumbaza hatimaye;
Dunia ina akili, binadamu sichezeye;
Dunia uwe na mali, huiwezi dhorubaye;
Dunia ina mizungu, tena yapika majungu.

Dunia wenye muali, ambao waichezeye;
Dunia kipigo kali, huwakumba hatimaye;
Dunia wakaja kuli, "menipata nini miye?"
Dunia ina mizungu, tena yapika majungu.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Maswali**

(a) Je, mashairi haya mawili ni ya aina gani? Toa sababu. (alama 2)
(b) Taja dhamira kuu katika kila shairi. (alama 2)
(c) Kwa kutoa hoja zozote **tatu** linganua mashairi haya kiumbo. (alama 3)

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

(d) Taja na uelezee **nafsi-nenewa** katika mashairi haya mawili. (alama 2)

(e) Kwa kutolea mfano **mmoja mmoja** eleza matumizi ya mbinu hizi za kimtindo katika shairi la A. (alama 2)

   (i) Kweli-kinzani
   (ii) Mishata

(f) Tambua **idhini** ya kishairi iliyotumika katika neno "Waichezeye" na uelezee dhima yake katika utoshelezi wa kiarudhi. (alama 1)

(g) Dondoa mfano **mmoja mmoja** wa mbinu ya tashhisi kutoka kwenye mashairi yote mawili. (alama 2)

(h) Andika ubeti wa **tatu** katika **shairi la A** kwa lugha nathari. (alama 4

(i) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika vifungu hivi. (alama 2)

   (i) Inampiku.
   (ii) Makontena.

**SEHEMU YA B: MSTAHIKI MEYA: TIMOTHY AREGE**

**Jibu swali la 2 au 3**

2. "Nanyi vilevile msikate tamaa. Endeleeni kushinikiza kumwona Meya.
   Mlango hatimaye huenda ukasalimu amri ---"
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hii. (alama 4)
   (b) Taja tamathali zozote **mbili** za lugha zilizotumika katika dondoo hii. (alama 4)
   (c) Eleza ni kwa nini wanaorejelewa wanakaribia kukata tamaa. (alama 8)
   (d) Eleza sifa **mbili** za mnenaji. (alama 4)
3. Viongozi katika bara la Afrika wameonyesha hali ya juu ya kutowajibika.
   Eleza dhana hii kwa kurejelea tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 20)

**SEHEMU YA C: RIWAYA**

**KEN WALIBORA: KIDAGAA KIMEMWOZEA**

***Jibu swali la 4 au 5***

4. "Ujenzi wa jamii mpya ni jukumu la vijana." Jadili kwa kurejelea riwaya hii. (alama 20)
5. Mwandishi kama huyo watu hukutana naye kwa nadra sana.
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Tambua mbinu iliyotumika katika kauli hii. (alama 2)
   (c) Toa mifano mingine **saba** ya matumizi ya mbinu hii katika riwaya hii. (alama 14)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI: DAMU NYEUSI**

**KEN WALIBORA**

***Jibu swali la 6 au 7***

6. "Alitembea kando ya barabara kwenye kijia cha wapitia njia huku akinyapia nyapia nyapunyapu na kupepesuka kama mlevi chakari".
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Anayerejelewa katika dondoo hili alikuwa anaenda wapi? (alama 2)
   (c) Eleza sifa za anayerejelewa katika muktadha kuu. (alama 6)
   (d) Mhusika huyu yuko na umuhimu gani katika hadithi husika? (alama 5)
   (e) Eleza mbinu zozote **tatu** ambazo zimetumiwa na mwandishi katika Muktadha huu . (alama 3)

7. **MIZIZI NA MATAWI: ALI ABDULLA ALI**
   (a) Eleza sifa mbili na umuhimu wa wahusika wafuatao katika hadithi ya **MIZIZI NA MATAWI**:

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

(i) Bi. Mkubwa. (alama 3)

(ii) Bi. Kidura. (alama 3)

(iii) Sudi Abdalla. (alama 4)

(b) Taja na ueleze jinsi maudhui ya mapenzi yanavyojitokeza katika hadithi hii.(alama 10)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

8. (a) Maghani ni nini? (alama 2)

(b) Eleza sifa za maghani. (alama 6)

(c) Fafanua aina zozote **tatu** za maghani. (alama 6)

(d) Taja na ueleze umuhimu wa maghani. (alama 6)

## Set4

**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

---

1. Kumekuwa na ongezeko la migomo ya wafanyakazi nchini katika siku za hivi karibuni. Wewe ni katibu wa tume iliyobuniwa na rais kusimamia suala hili. Andika ripoti

2. Ufisadi umechangia pakubwa kuwepo kwa maendeleo duni nchini. Jadili.

3. Andika insha inayoafikiana na methali Baniani mbaya kiatu chake dawa

4. Andika insha itakayomalizikia kwa;
...walipofungua mlango huo hatimaye,wengi hawakuweza kuzuia hisia zao.Waliangua vilio kwa maafa waliyoshuhudia.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

## Set4

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

---

**UFAHAMU: (Alama 15)**
**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Tokea muundo mpya wa serikali ya ugatuzi uanze kutekelezwa miaka miwili iliyopita, kumeendelea kushuhudiwa matatizo mengi hali iliyopelekea kushuhudiwa kwa msururu wa migomo na maandamano ya raia.Fujo za karibuni kabisa ni zile zinazoshuhudiwa katika miji mikubwa za wachuuzi na wafanyibiashara wakipinga hatua za serikali za kaunti kuwatoza ushuru takribani kwa kila huduma na bidhaa ikiwemo wanyama,kuku na ndege.La kuhuzunisha zaidi katika baadhi ya majimbo imeripotiwa kuwa raia wamelazimishwa kulipa ushuru kwa kutaka tu kuona maiti za jamaa zao kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti!

Wanasiasa wameonekana kuwa na wakati mgumu kutetea mfumo huu mpya wa ugatuzi huku baadhi wakisema kwamba matatizo yanayoshuhudiwa kwa sasa yametokana na ugeni wa mfumo huo.Wengine wameinyoshea kidole serikali ya kitaifa kwamba ndiyo inayosambaratisha muundo huu.Wengine wanahoji kuwa bado ni mapema na kwamba kunatajika muda mrefu ili kufaulu

Ni wazi kwamba kumekosekana nidhamu bora ya kusimamia maisha ya raia nchini Kenya.Matatizo yanayokumba raia kwa sasa ni dalili kuwa mfumo wa serikali ya ugatuzi umeongezea chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu.Swali ni je,hadi lini nidhamu ya kusimamia raia itakuwa ni suala la majaribio na makosa?

Hatua ya kuwarundikizia raia ushuru mkubwa ni kitendo cha unyonyaji na cha dhuluma kinachofaa kupingwa. La kufahamishwa hapa ni kwamba ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi wa kibepari ikiwemo Kenya.Asilimia 90 ya mapato ya serikali za kibepari huegemea ushuru. Kwa hivyo hatua ya serikali za kaunti katika kuwanyonya raia kwa kuwalipisha ushuru si ajabu bali ni thibitisho kuwa jamii ya Kenya inaongozwa na nidhamu ya kiuchumi ya ubepari mfumo wa unyonyaji na ukandamizaji.Ukweli unabakia kuwa ndani ya serikali za kibepari raia ndio hubebeshwa mzigo wa ushuru unaoishia matumboni mwa viongozi!

Miito ya mabadiliko ya katiba na ya miundo mipya ya kiutawala si lolote ila ni moja tu ya hatua za mfumo wa kibepari kujipa muda wa kuishi na kuziba aibu zake za kushindwa kusimimia maisha ya watu.Kufeli huku kwa mfumo huu kunashuhudiwa hadi kwenye nchi kubwa za kibepari kama Marekani na Uingereza hivyo nazo zimekumbwa tele na maandamano na fujo za raia wakilalamikia hali ngumu ya maisha.

for free past papers visit www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Maswali**

a) Yape makala haya anwani mwafaka. (alama 1).
b) Eleza mtazamo wa wanasiasa kuhusu utepetevu wa mfumo huu. (alama 3)
c) "Ugatuzi nchini Kenya ni mfumo wa kibepari" Thibitisha kauli hii kwa kurejelea makala (alama 3)
d) Migomo ni zao la matatizo yaliyogatuliwa kutoka serikali kuu. Toa sababu nyingine zinazosababisha migomo katika serikali za ugatuzi (alama 4)
e) Thibitisha jinsi mfumo wa ugatuzi umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu (alama2)
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo (alama 2)
(i) Ugatuzi

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

(ii) Kibepari

**UFUPISHO (Alama 15)**

**Soma makala yafuatayo na ujibu maswali.**

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo ulimwenguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malghafi yanayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji, viwanda vinavyoimarika ni vile vidogo. Hivi ni viwanda ambavyo huhusisha amali za mikono. Kuimarika kwa viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu hasa kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa na bidhaa za viwanda. Katika msingi huu, viwanda vikubwa vitawiwa vigumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vidogo pia vina uwezo wa kuwaajiri wafanyakazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine.Uajiri huu wa wafanyakazi wengi ni muhimu katika maeneo mengi ambako tatizo la uajiri ni mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasnia, mataifa yanayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo vidogo hakuhitaji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Sambamba na suala hili ni kuwa ni rahisi kujaribisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo. Ikiwa mzalishaji yeyote atazalisha bidhaa mpya kwa mapana, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hizo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa zenyewe.

Majaribio mazuri huwa ni kwa kiwango kidogo. Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa ni chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikisha kuwa nafasi za ajira zimesambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huu wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa kiununuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo. Upanuzi na ueneaji wa viwanda vidogo vidogo ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa msingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

Licha ya faida zake, ueneaji au kutanda kwa viwanda hukabiliwa na matatizo mbalimbali. Tatizo la kwanza linahusiana na mtaji. Lazima pawepo na mbinu nzuri za kuweka akiba ili kuwa na mtaji wa kuanzishia biashara. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kwa kutegemea masoko ya mitaji ambayo katika mataifa mengi hayajaendelezwa vyema. Inakuwa vigumu katika hali hii basi kupata pesa kwa uuzaji wa hisia kwenye masoko hayo.

Tatizo jingine linalotokana na ukosefu wa mikopo ya muda mrefu ya kibiashara kwa wenye viwanda vidogo vidogo. Mikopo ya aina hii huwa muhimu hasa pale ambapo anayehusika ana mradi wa kununua vifaa kama mashine. Mikopo ya muda mfupi inayopatikana kwenye mabenki huweza kuwashinda wengi kutokana na viwango vya riba kuwa juu. Haimkiniki kwa viwanda kama hivi kukopa kutoka nje ya nchi zao. Juhudi za kuendeleza viwanda hivi huweza pia kukwamizwa na tatizo la kawi kama vile umeme. Gharama za umeme huenda ziwe juu sana. Isitoshe, si maeneo yote ambayo yana umeme. Matatizo mengine huhusiana na ukosefu wa maarifa ya kibiashara, ukosefu wa stadi za ujasiriamali au kuwa na ujasiri wa kujiingiza kwenye shughuli Fulani na miundo duni.

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

For free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Ili kuhakikisha kuwa viwanda vimekuzwa na kuendelezwa pana haja ya kuchukua hatua kadha. Kwanza, kuwepo na vihamasisho kwa wanaoanzisha viwanda vidogo vidogo kama vile punguzo la kodi, kuhimiza kuanzishwa kwa viwanda vidogo vidogo na kusaka kuyapanua masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo. Aidha kuanzishwa na kupanuliwa kwa taasisi za kuendeleza upanuzi huo. Pana haja ya kuwekeza kwenye rasilimali za kibinadamu; kuelimishwa na kupanua uwezo wao wa kuyaelewa mambo mbalimbali. Miundo msingi haina budi nayo kupanuliwa na kuimarishwa.Upo umuhimu pia wa kuongeza kasima inayotengewa maendeleo na ukuzaji wa viwanda ili kuharakisha maendeleo yake pana umuhimu wa kupambana na ufisadi unaoweza kuwa kikwazo kikubwa. Inahalisi kutambua ikiwa viwanda vitatanda nchini, uchumi wa nchi nao utawanda.

(a) Kwa **maneno 65-75,** eleza ujumbe muhimu unaopatikana katika aya ya pili hadi ya nne.
**( alama 8,1 utiririko)**

**Maandalizi**

**Jibu**

(b) Kwa **maneno (50-55)** fafanua mambo yanayotinga ukuaji wa viwanda. **(alama 5, 1 utirirko)**

Maandalizi

Jibu

**MATUMIZI YA LUGHA** **(alama 40)**

a) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa (alama 2)
Nyuso za vijana wale zilichujuka walipoanguka

b) Tumia **KI** katika sentensi kuonyesha masharti yanayowezekana (alama 2)

c) Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi **'abudu'** katika kauli ya kutendesheana (alama 2)

d) Akifisha (alama 4)
aisee yale mawimbi ya tsunami yaliyotokea bahari hindi yaliangamiza biashara nyingi sana alisema bomet

e) Changanua sentensi hii kwa njia ya mstari. (alama 4)
Rais alihutubu lakini walimpuuza

f) Huku ukitolea mfano eleza tofauti kati ya kishazi huru na kishazi tegemezi (alama 3)

g) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu lake (alama 2)
Pika ugali kwa kuku kila Jumamosi ukitumia gesi

h) Tunga sentensi moja ya kuonyesha rai (alama 1)

j) i Eleza maana ya chagizo (alama 2)
ii. Bainisha chagizo katika sentensi ifuatayo (alama 1)
Shamba lilipaliliwa haraka na mkulima

k). Andika katika usemi wa taarifa (alama 3)
"Hicho kijicho cha paka cheupe leo marufuku kwangu" alisema Mzee Kambumbu

l) Tunga sentensi moja ukitumia kitenzi kimoja kilichoundwa kutokana na nomino **zawadi** (alama 2)

m). Tambua matumizi ya kiambishi **ji** katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Jino la jitu hilo lililiwezesha kujilia chakula kingi kuliko mkimbiaji Yule

a) Tunga sentensi moja kuonyesha maana ya neno: **ilmradi.** (alama 2)

b) Andika sentensi moja ukitumia kihisishi cha bezo (alama 1)

c) Ainisha viambishi katika neno **waliibiana** (alama 2)

d) Nini maana ya kiimbo? (alama 1)

e) (i) Vokali ni nini? (alama 1)
(ii) Eleza sifa mbili za sauti ifuatayo **/i/** (alama 2)

f) Panda ni kuatika mbegu ardhini au kuparaga mti. Andika maana nyingine mbili (alama 2)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

ISIMU JAMII (Alama10)

a. Eleza nadharia tatu kuhusu chimbuko la Kiswahili. alama6)

b. Fafanua istilahi zifuatazo: (alama 4)

i. UwiliLugha

ii. LinguaFranka

iii. Misimu

iv. Sajili

## Set4

**102/3**

**FASIHI**

**KARATASI YA TATU**

---

**SEHEMU YA A : USHAIRI**

1. **Swali la Lazima.**

***Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Naujuwa mwanzo wake, vile ulivyochipuza,
Kilofanya mkereke, na kisichowaumiza,
Ya kuwa sepata mke, katu hakuwapendeza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Mwasema matako hana, yako sawa kama meza,
Tena pua yako pana, kama ya kubandika,
Lakini mimi naona, yenu sitoyasikiza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Kipita nae pahali, sakubimbi hubwagiza,
Nzitonzito kauli, asengenywazo aziza,
Nywele za kipilipili, hasongi asongomeza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Munenayo ni mazito, hadi yeye humliza,
Bali kwangu ni matoto, muhali kunichukiza,
Japo miguuye fito, haitoshi mtembeza ?
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Nataka watowa khofu, kwa munayo mtangaza,
Si yule mpenda pofu, kawambia ni kengeza,
Ni mwenyewe nimeshufu, muhali kunigeuza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Tafadhalini mwachie, musilumbe kumaliza,
Unyonge musitumie, kila siku kumaliza,
Haya ni yeye na mie, yawaje mukachagiza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Hakujiumba mwenyewe, musighafilike wenza,
Aloumba mimi nawe, ndiye aliyemtweza,
Tusijitie kiwewe, tukakufuru muweza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

**Maswali**

a) Eleza bahari za shairi hili kwa kutoa ithibati kamili (alama 3)

b) Kwa kutoa mifano mwafaka, eleza methali zozote mbili kwenye shairi (alama 4)

c) Bainisha mambo yoyote manne nafsineni anayazungumzia (alama 4)

d) Fafanua idhini ya mshairi (alama 4)

e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi (alama 3)

f) Eleza maana za vifungu hivi kama vilivyotumika kwenye shairi

(i) Sakubimbi hubwagiza (alama 1)

(ii) Musighafilike wenza (alama 1)

**SEHEMU YA B : RIWAYA**

Said A. Mohamed : *Kidagaa Kimemwozea*

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. 'Alaa ! Mtoto mdogo hata ubwabwa haujakutoka shingoni unakimbilia nini...... ?'
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   b) Bainisha tamathali mbili za usemi katika dondoo. (alama 2)
   c) Kwa kutoa mifano mitatu, onyesha kwamba kwa hakika ubwabwa ulikuwa umemtoka shingoni anayerejelewa (alama 6)
   d) Asasi inayorejelewa katika muktadha huu inakumbwa na matatizo mengi. Kwa kurejelea riwaya nzima, jadili matatizo yoyote manne kwa mifano mwafaka (alama 8)
3. Kifo cha Uhuru ni jazanda ya hali ya mambo katika jumuiya ya kidagaa kimemwozea. Thibitisha. (alama 20)

**SEHEMU YA C : TAMTHILIA**

T. Arege : *Mstahiki Meya*

**Jibu swali la 4 au 5**

4. • • •Nashukuru sasa umeanza kuona mambo yanavyostahili kuenda.
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   b) Fafanua sifa za msemaji (alama 4)
   c) Eleza umuhimu wa msemewa (alama 4)
   d) Jadili jinsi maudhui yoyote manne yanayodokezwa katika dondoo yanavyojitokeza katika tamthilia nzima (alama 8)
5. Tamthilia ya Mstahili Meya ni kiakisi cha mataifa ya ulimwengu wa tatu. Jadili(alama 20)

**SEHEMU YA D : HADITHI FUPI**

K. Walibora na S.A. Mohamed : *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 6 au 7**

6. Huku ukitoa mifano maridhawa, onyesha jinsi wanawake wamesawiriwa katika Diwani ya Damu Nyeusi kwa kurejelea hadithi zozote tano.
7. '.....Nimegundua amekuwa akininyima uzuri wa mandhari ya makaburini siku zote hizi.'

for freepast papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)

b) Tambua mbinu ya lugha inayojitokeza katika dondoo hili (alama 1)

c) Huku ukirejelea diwani ya Damu Nyeusi, onyesha jinsi mbinu hii ilivyotumiwa katika hadithi zozote tano (alama 15)

**SEHEMU YA E : FASIHI SIMULIZI**

8. a) Eleza maana ya maigizo (alama 2)

b) Fafanua dhima tano za michezo ya chekechea (alama 10)

c) Eleza sifa nne za mivigha (alama 8)

## set5

**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

---

1. Wewe ni balozi mteule wa nchi yako katika nchi ya kigeni. Andika tawasifu utakayotoa katika siku ya kutoa stakabadhi zako kwa rais wa nchi uliyoteuliwa kuwa balozi.

2. Utumizi wa afyuni[mihadarati} katika taasisi za masomo nchini ni suala ambalo ni muhali kutatuliwa. Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu usidhani kapoa.

4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa: ….hivyo ndivyo ukurasa mpya katika kitabu cha maisha yangu ulivyofunguka.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

## Set5

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

---

1. **UFAHAMU**
**<u>Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali.</u>**
**Historia ya katiba**
Katiba ni utaratibu wa sheria unaoweka mpango wa jamii kuendesha mambo.Ni muhimu kila raia ajue katiba ya nchi yake.

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Katiba yaweza kuwa imeandikwa au haikuandikwa. Katika jamii za jadi, katiba ilihifadhiwa na kupokezwa kwa mdomo. Mtindo wa kuandika katiba ulianza nchini Marekani mwaka 1787. Ingawa katiba hii imefanyiwa mabadiliko hapa na pale,bado ni ileile. Kenya ilipowekwa chini ya himaya ya Uingereza mwaka 1895, ilianza kutumia katiba ya Uingereza. Baada ya masetla wa kikoloni kujikita, Kenya kuwa koloni. Hii ililazimu pawe na katiba nyingine mwaka 1920. Waafrika waliupinga mfumo huu kwa sababu haukuwahusisha kikamilifu kwenye masuala ya uongozi. Utetezi wa wanasiasa uliilazimisha serikali ya Uingereza kuitisha makongamano mbalimbali kama vile lile la Devonshire na mengine ili kurekebisha katiba. Waafrika hawakuridhika. Wakaendelea kudai katiba mwafaka. Harakati hizi zilileta kuitishwa kwa kongamano la katiba la Lancaster. Lengo lilikuwa kuandika katiba itakayotumiwa nchini hadi leo. Kati ya wajumbe walioenda Uingereza kuandika katiba mwaka 1962 ni pamoja na Tom Mboya, Jean Marie Seroney, Julius Kiano, Jomo Kenyatta, Masinde Muliro, Oginga Odinga, Ronald Ngala, Daniel Arap Moi na James Gichuru. Wengine ni Martin Shikuku, Dennis Akumu, Taita Towett, Abdilahi Nassir, Jeremiah Nyaga na John Keen.

Katiba ni kitovu cha taifa. Baina ya mambo inayotekeleza ni kuweka utaratibu na kanuni za utawala, kwa mfano, utawala wa kimikoa na serikali za wilaya. Pamoja na haya, katiba hufafanua vyombo vikuu vya serikali ,mamlaka yavyo na mipaka yavyo ya kutenda. Vyombo hivi ni bunge, mahakama, urais, jeshi n.k. Hali kadhalika, katiba hupambanua haki za raia.

Hii hudumisha demokrasia na huwawezesha wananchi kupata uhuru na haki za kimsingi. Katiba hukinga haki za kila raia, hasa kutokana na udhalimu wa wengi au wenye uwezo mkubwa. Zaidi ya yote, katiba huimarisha asasi za umma ili kudumisha uwajibikaji.

Katiba huhalalishwa na watawaliwa. Hii hutokea wanaposhirikishwa katika uandishi wake. Kuanzia miaka ya themanini, raia walianza kudai katiba igeuzwe. Mwamko wa kutaka mageuzi ulianza kwa harakati za kubadilisha mfumo wa kisiasa kutoka ule wa chama kimoja hadi ule wa demokrasia ya vyama vingi. Haja ya mfumo mpya wa kisiasa ulilenga kuwashirikisha wananchi katika utawala na kuondoa uimla.

Harakati zilitia fora miaka ya tisini. Mambo yaliyochochea hali hii ni mengi. Kwanza, katiba iliyokuwa imeandikwa na watu wachache ilikuwa imefanyiwa marekebisho mengi. Marekebisho haya yalimpa rais mamlaka mengi juu ya serikali kuu na vyombo tofauti vya serikali. Pili, viongozi na watu wenye uwezo na utajiri walipuuza katiba. Raia walihisi wanadhulumiwa. Walipinga hali ya wachache waliomzunguka rais kunufaika huku umma ukitengwa. Tatu, kutokana na uongozi uliokuweko wakati huo, wanawake, watoto na walemavu walidhulumiwa na kukosa uwakilishi

ufaao.Hatimaye, pakawa na ongezeko la uharibifu wa mazingira, ufisadi na unyakuzi wa mali ya umma kama vile ardhi.

Waliopigania katiba mpya walikuwa na haja ya katiba ambayo uandikaji wake ungewahusisha Wakenya wote. Mwanzoni, serikali ilipinga wito wa mabadiliko. Lakini mnamo mwaka 2001 iliunda Tume ya Marekebisho ya Katiba ili kutekeleza mahitaji ya wananchi. Tume hii iliwahamasisha na kuwashawishi raia kutoa maoni. Tume iliandaa vikao katika maeneo ya ubunge 210 ambapo wananchi walitoa mapendekezo kuhusu marekebisho ya katiba waliyotaka.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Katika mapendekezo hayo raia walisisitiza mambo kadhaa. Jambo la kwanza ni utawala mwema na uwajibikaji wa viongozi na maafisa wa umma .Jambo lingine ni kulinda haki za binadamu zikiwemo za wanawake, watoto na walemavu. Raia walidai kanuni za usawa na ulinganifu. Aidha walitilia mkazo mahitaji ya msingi kama chakula, afya nzuri, makao, elimu, usalama, uchumi, na kadhalika.

Msingi wa mapendekezo hayo yote ni kuwepo na amani ya kitaifa, umoja na uadilifu ili kulinda maslahi ya wananchi wote na taifa.

**Maswali :**

(a) Eleza kilichosababisha kongamano la katiba la Lancaster (alama3)

(b) Taja mambo matatu yaliyotiliwa mkazo na raia katika maoni yao kuhusu katiba. (alama3)

(c) Eleza umuhimu wa katiba kwa mujibu wa taarifa. (alama3)

(d) Taja sababu zilizochangia ubadilishaji wa katiba. (alama3)

(e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama3)

(i) Kitovu

(ii) Harakati

(iii) Hamasisha

## 2. UFUPISHO

***Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Lugha ya Kiswahili ni lugha iliyoendelea sana. Leo hii lugha hii inasemwa na watu wote nchini Tanzania, Rwanda,Burundi, nchini Kenya, Nchini Uganda, Zaire, Malawi, msumbiji, Zambia, Somalia, Bukini (Madagascar) na Ngazija (Comoro), inasemwa na asilimia kubwa ya wananchi wa huko. Aidha lugha hii ina wasemaji si haba katika kisiwa cha Soktana nchini Oman.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Fauka ya maendeleo haya, Kiswahili kinatumika kwa minajili ya matangazo ya habari katika idhaa nyingi za mashirika ya habari ulimwenguni. Nchi zenye idhaa za Kiswahili ni kama vile hizi zetu za Afrika ya Mashariki na kati, Afrika ya kusini, Nigeria, Ghana, Uingereza, ( shirika la B.B.C) Marekani ( shirika la V.O.A), Ujerumani ( shirika la Radio DeutchWelle, Cologne), Urusi ( Radio Moscow), China, India nakadhalika.

Maendeleo mengine yanapatikana katika upande wa elimu. Marekani peke yake, kuna vyuo zaidi ya mia moja vinavyofundisha Kiswahili kama lugha muhimu ya kigeni. Huko Uingereza vyuo kama London, Carmbridge na Oxford vinafundisha lugha hii. Nchi nyingine ambazo zina vyuo vinavyofunza lugha ya Kiswahili ni kama vile Japan, Korea, Ghana, Nigeria na kadhalika.

Kweli Kiswahili kimeendelea jamani. Lakini je, kilianza vipi? Na ilikuwaje kikaweza kupiga hatua hizi zote?

Kiswahili kilianza kuzungumzwa na kabila dogo la watu walio kuwa wakiitwa wangozi. Watu hawa walikuwa wakiishi mahali palipoitwa shungwaya. Shungwaya ni nchi ya zamani iliyokuwa eneo lililoko katika nchi mbili jirani ambazo siku hizi ni Kenya na Somalia. Kabila hili la wangozi liliishi jirani na makabila mengine kama vile wajikenda, wapokomo, Wamalakote ( au Waelwana) naWangazija ( kabla hawajahamia visiwa vya Ngazija). Lugha ya wangozi siku hizo, ambayo ndiyo mzazi wa Kiswahili cha leo, ilijulikana kwa jina kingozi. Kama ilivyosemwa hapo awali, kingozi kilisemwa na watu wachache sana.

Je lugha hii ilikuwaje mpaka ikapata maendeleo haya makubwa tunayoyashuhudia siku hizi? Ama kwa hakika, Kiswahili ni lugha iliyo bahatika tu.Inaweza kusemwa kwamba lugha hii ilipendelewa na mazingira na historia.

Jambo la kwanza, wageni waliotoka mashariki ya kati kufikia hizi janibu zetu Afrika ya mashariki walikaribishwa vizuri na hawa wangozi. Wakaingilia wageni na wenyeji kindakindaki, kidini, kitawala, kibiashara na kitamaduni kwa jumla. Punde si punde wangozi, ambao baadaye walijulikana kama waswahili na wageni hawa, wakaelimika katika dini (yakiisilamu), biashara na mambo ya utawala aina mpya. Lugha yao nayo ikapanuka pale ilipochukua msamiati wa kigeni hususan wa Kiarabu na Kiajemi na kuufanya uwe wake, ili kueleza kwa rahisi zaidi mambo haya mageni katika taaluma za dini, biashara, siasa na hata sayansi kama vile unajimu.Wakati huo, lugha ya Wangozi sasa ikaitwa Kiswahili wala sio kingozi. Tatizo hapa ni kuwa kwa vile Kiswahili kilichukua msamiati mwingi wa kigeni ili kuelezea taaluma hizi mpya, baadaye kimekuja shukiwa kwamba ni lugha ya kigeni ilhali ni lugha ya Kiafrika asilia, na kitovu chake ni nchi mpya za kiafrika ziitwazo Kenya na Somalia hii leo.

(a) Thibitisha kuwa Kiswahili kimekuwa lugha ya kimaitaifa ( maneno 35 – 40) ( alama 7)

**Matayarisho:**

**Nakala Safi:**

(b) Ukitumia maneno yako mwenyewe, eleza ujumbe ulio katika aya ya mwisho. ( alama 8)

for free pastpapers visit: www.freekcsepastpapers.com or call:0720502479

**SARUFI**

1. Eleza sifa bainifu za sauti /j/. (al 2)
2. Tofautisha mofimu huru na tegemezi kwa kutolea mifano mwafa (al 2)
3. Unda neno lenye silabi ifuatayo KIKKIKI (al 1)
4. Tia shadda katika sentensi ifuatayo (al 1)
   *Wachezaji wamo uwanjani.*
5. (i) Kiimbo ni nini? (al 1)
   (ii) Onyesha matumizi mawili ya kiimbo. (al 2)
6. Ainisha (al 3)
   Wasiorithishwa
7. Sahihisha sentensi ifuatayo. (al 2)
   *Sukari zilizowekwa mfukoni zimenyeshewa*
8. Eleza maana ya sentensi zifuatazo. (al 2)
   (i) Tunda lenyewe limeoza.
   (ii) Tunda lenye shimo halinunuliki
9. Kanusha sentensi ifuatayo. (al 2)
   Ningalifuzu katika mtihani wangu ningalituzwa.
10. Tunga sentensi na ubainishe kijalizo. (al 2)
11. Andika sentensi usemi halisi.
    Rais alisema kuwa wangepata tiba ya bure kama bunge lingepitisha mswada huo.
12. Tunga sentensi yenye muundo wa: (al 3)
    Kiima, kiarifa, yambwa tendwa, yambwa tendewa na yambua ala..
13. Changanua sentensi kwa kutumia jedwali. (al 4)
    Wachezaji vikapu watakifanikiwa katika mechi hiyo watatuzwa medali
14. Nyambua kitenzi hiki katika kauli iliyo mabanoni *pa* (tendeka) (al 1)
15. Bainisha virai katika sentensi hii. (al 3)

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Juma alikwenda mjini kwa miguu

16. Tunga sentensi kudhihirisha matumizi mawili ya <u>KU</u>. (al 2)
17. Onyesha matumizi mawili ya nukta mkato. (al 2)
18. Toa maana mbili ya sentensi ifuatayo: (al 2)

Laleni!

**<u>ISIMU JAMII:</u>** **(ALAMA 10)**

(a) (i) Eleza maana ya krioli. (alama 2)

(ii) Eleza sifa zozote tatu za krioli. (alama 3)

(b) (i) Eleza maana ya Lingua Franka (alama 2)

(ii) Tambua sifa zozote tatu za Lingua Franka (alama 3)

## Set5

**102/3**

**FASIHI**

**KARATASI YA TATU**

---

1. (a) Eleza sifa nne za kimtindo zinazopatikana katika methali za Kiswahili.(alama 8)

(b) Eleza mbinu tatu ambazo hutumiwa kuzua misimu. (alama 6)

(c) Ni jukumu la jamii kudumisha fasihi simulizi. Dhihirisha. (alama 6)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**SEHEMU YA B: HADITHI FUPI**

**<u>DAMU NYEUSI</u>**

***Jibu swali la 2 au 3***

2 Diwani ya Damu Nyeusi imesheheni jamii ya watu dhulumati. Jadili ukirejelea hadithi za:

(a) Maskini, Babu Yangu.

(b) Mwana wa Darubini. (alama 20)

**<u>NDOA YA SAMANI</u>**

3. "Chambilecho Waswahili atafutaye hachoki, na akichoka keshapata."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Fafanua mtazamo wake Abu kuhusu maisha. (alama 16)

**<u>SEHEMU YA C; RIWAYA</u>**

**KIDAGAA KIMEMWOZEA - Ken Walibora**

***Jibu swali la 4 au 5***

4. "……Moyo ulimpapa na kijasho chembamba kumtekenya juu ya mwanzi wa pua. Akahisi uchungu wa pua. Akahisi uchungu wa mwiba wa kujidunga…."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Tambua mbinu mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

(c) Eleza umuhimu wa mrejelewa. (alama 4)

(d) Ustawi wa nchi yoyote hutegemea vijana wake. Jadili ukiirejelea KIDAGAA KIMEMWOZEA. (alama 10)

5. (a) Thibitisha jinsi mwandishi wa Riwaya ya <u>Kidagaa Kimemwozea</u> alivyofanikisha maudhui ya uwajibikaji. (alama 10)

(b) Jadili mbinu ya sadfa katika Kidagaa Kimemwozea. (alama 10)

**SEHEMU YA D; TAMTHILIA**

***Jibu swali la 6 au 7***

6. " Huu ni ukoloni mamboleo"
   (a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
   (b) Fafanua umuhimu wa msemewa katika tamthilia hii (alama 8)
   (c) Eleza kwa tafsili namna ukoloni mamboleo unavyojitokeza katika tamthilia (alama 8)
7. Jadili matumizi ya mbinu zifuatazo; (alama 20)
   (i) kinaya
   (ii) methali
   (iii) majazi
   (iv) Uzungumzi nafsia

**SEHEMU YA E; USHAIRI**

***Jibu swali la 8 au 9***

**Soma shairi hili kisha ujibu maswali.**

**8. Wenye vyao Watubana**

1. Wenye vyao watubana, twaumia maskini,
La kufanyiza hatuna, hali zetu taabani,
Kwa sasa kilo ya dona, bei mia ishirini,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

2. Washindana matajiri, kwa bei siyo utani,
Na pigo kwa mafakiri, tunao hali ya chini,
Wazeni kutafakari, wanyonge tu madhilani,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

3. Limekuwa kubwa zogo, hakwendeki madukani,
Fungu moja la muhogo, sasa shilingi miteni,
Huo mkubwa mzigo, waelemea vichwani,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

4. Si hichi wala si kile, hakuna cha afueni,
Bei imekuwa ndwele, wenye macho lioneni,
Ukiutaka mchele, pesa jaza mfukoni,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

5. Waliko hao samaki, huko ndiko uchawini,
Wachuuzi hawacheki, zimewatoka huzuni,
Vibuwa havishikiki, kimoja kwa hamsini,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

6. Maisha yetu viumbe, yamekuwa hilakini,
Wenye vyao kila pembe, wametukaa shingoni,
Nyama ya mbuzi na ng'ombe, sasa hali maskini,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

7. Maji yamezidi unga, kwa lodi wa darajani,
Kajitolea muhanga, kwa bei hawezekani,

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Mvao wake wa kanga, ni shilingi elifeni,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

**Maswali**

(a) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)

(b) Jadili dhamira ya nafsi neni. (alama 2)

(c) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. (alama 4)

(d) Fafanua kwa kutoa mfano, mbinu moja aliyotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. (alama 2)

(e) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili ukizingatia: (alama 4)
- (i) Ubeti
- (ii) Vina

(f) Ujumbe unaowasilishwa katika shairi hili una hadhira lengwa tatu. Zitaje na utoe mifano. (alama 6)

au

**9. MKWARUZANO WA NDIMI**

Huyo! Mshike huyo !
Hakuna bunduki wala kifani
Bomu na risasi hata hawazijui
Lakini mno wanashambuliana
Kwa ndimi zilizonolewa kwa makali
Vipande vya matusi silaha zao.

Yu imara mmoja wao
Akirusha kombora la neno zito!
Limtingishe adui wake
Na kumgusa hisia kwa pigo kuu
Pigo linalochoma moyoni kama kichomi
Kuchipuza joto la hasira na kisasi
Katika mapigano yaso na kikomo

Filimbi ya suluhu inapulizwa kuwaamua!
Nani anayekubali suluhu?
Roho zinakataa katakata
Huku ukaidi ukinyemelea na kutawala kote
Mapandikizi ya watu yakipigana
Vita shadidi visivyo ukomo
Vita vya ndimi!

Magharibi sasa
Jua linapungia mkono machweo
Nalo giza likinyemelea kwa kiburina
Kasi
Sisikii tena sauti za misonyo
Mate yawatesi yamekauka
Makanwa yao yamelemewa na uchovu
Sasa wameshikana mikono
Ishara ya suluhu.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

***Maswali***

(a) Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)

(b) Eleza dhamira ya mshairi. (alama 2)

(c) Eleza kanuni za utunzi alizotumia mshairi. (alama 4)

(d) Taja mbinu zozote tatu za kifasihi alizotumia mshairi. (alama 3)

(e) Jadili toni ya mshairi katika beti tatu za awali. (alama 2)

(f) Tambua matumizi ya mistari mishata na utoe mifano miwili. (alama 3)

(g) Andika mishororo ya kwanza mitatu katika ubeti wa 4 kwa lugha ya nathari. (alama 3)

(h) Toa maana ya msamiati huu. (alama 2)

(i) Kombora

(ii) Misonyo

## Set6

**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

---

1. Wewe ni katibu wa kamati ya maslahi ya klabu ya wasanii chipukizi mtaa wa Rehema. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanywa hivi karibuni kujadili suala la usalama uliozorota.

2. Ufisadi umekuwa janga linalohitaji kujitolea ili kupiga vita. Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Ulimi huuma kuliko meno.

4. Tunga kisa kinachomalizika kwa maneno haya:
.................hapo ndipo iliponipambazukia kuwa nilikuwa naogelea baharini pekee, kinyume na wenzangu wote.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

## Set6

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

---

**1. <u>UFAHAMU (ALAMA 15)</u>**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Mafuta yanayopatikana kwenye fukwe za bahari, moshi wa magari, takataka na bidhaa nyinginezo zinazotupwa hapa na pale ni vichafuzi vya mazingira. Vichafuzi huathiri afya zetu na kuathiri wanyama na mimea. Wanadamu wanayachafua mazingira yao kwa kila aina ya bidhaa mbaya

za kikemikali zinazotoka viwandani mwa kawi/nguvu. Bidhaa hizo ni matokeo ya maisha ya siku hizi anayoishi binadamu.

Licha ya ukweli huu, ni muhimu kujua kuwa uchafuzi wa mazingira haukuanza leo. Miaka na miaka iliyopita, viwanda vimekuwa vikitoa mawingu makubwa ya moshi yenye sumu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira umeongezeka mara dufu kutokana na kuongezeka kwa viwanda. Uchafuzi umesambaa ardhini, kwenye anga na majini. Msambao huu unapatikana katika pembe zote za ulimwengu wetu. Je, kuna aina zipi za uchafuzi?

Kwanza, kuna uchafuzi wa hali anga. Huko juu angani kuna tabaka linalojulikana kama ozoni. Tabaka hili ni aina ya gesi ya oksijeni na linaunda kinga fulani dhidi ya miale ya jua. Miale hiyo ya jua huweza kusababisha saratani ya ngozi inapomfikia binadamu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira unaelekea kuliathiri tabaka hili. Vilevile, baadhi ya kemikali zinazotumiwa katika jokofu au kwenye mikebe ya marashi ya kupulizia na upakiaji bidhaa, huuharibu ukanda huo.

Uchafuzi mwingine ni uchafuzi wa kiajali, uchafuzi huu hutokea bila binadamu kukusudia. Mfano mzuri ni meli inayovuja mafuta baharini. Mafuta haya huwaathiri na kuwaua wanyama wanaoishi baharini kama samaki na ndege na hata kuyaharibu mazingara yenyewe.

Miji mikubwa hukumbwa na uchafuzi mwingine unaohusiana na kuwako kwa idadi kubwa ya magari. Magari haya hutoa moshi unaochanganya gesi ambazo huungana na nyingine zinazoletwa na viwanda vikubwa. Mchanganyiko huu unapoungana na maji, husababisha mvua ya asidi. Mvua hii huweza kuiua mimea, kuathiri majengo na hata kuwaua wanyama wa pori ambao huenda wakayatumia maji hayo. Magari hayo hutoa moshi uliochanganyika na madini aina ya risasi ambayo huweza kuathiri siyo tu mazingira bali pia mfumo wa akili wa binadamu.

Uchafuzi mkubwa ni utupwaji ovyo wa takataka. Fauka ya hayo watu hufukia ardhini takataka ambazo huweza kuwa na matokeo mabaya kwa sababu ya kupenyeza kwenye udongo na maji yanayotumiwa na watu na mimea. Kila siku tunatupa takataka bila kujali wala kukubali. Takataka hizi ni kama makopo, mifuko ya plastiki, mabaki ya sigara au maganda ya matunda. Baadhi ya takataka ni hatari kwa wanyama na nyingine huweza pia kusababisha majanga kama moto. Aidha, hufanya mazingira yaonekane machafu.

Sote tuna jukumu kubwa la kuchangia kupunguza uchafuzi wa mazingira. Kwanza, kuelimisha na kutambua umuhimu wa usafi wa mazingira yetu. Tunapaswa kutia takataka zetu kwenye vijalala maalum au mahali tunapoweza kuzichoma na kuziteketeza. Tuhakikishe tunatunza vitu kama mifuko, chupa na kadhalika ambavyo huweza kuundwa upya na kutumika tena. Hali kadhalika, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na juhudi za kuwahimiza wenye magari kutumia mafuta ya gari ambayo hayana madini ya risasi. Kwa njia hii tutasaidia kuyaboresha mazingira yetu. Vilevile pana umuhimu wa kutilia mkazo utumiaji wa bidhaa ambazo zinaweza kuoza na kuvunjikavunjika au kusagika na kuwa sehemu ya udongo. Hatua ya kwanza ya kupambana na uchafuzi wa mazingira ni kujielimisha na kuwajibika. Kila mmoja akitoa mchango wake tutafanikiwa. Kumbuka; kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

**Maswali**

(a) Uchafuzi ni nini? (alama 1)
(b) Ongezeko la viwanda umechangiaje uchafuzi wa mazingira? (alama 2)
(c) Tabaka la ozoni huathiriwaje na uchafuzi? (alama 2)
(d) Athari zipi zitatokea iwapo mazingira hayatatunzwa? Eleza. (alama 4)
(e) Kwa nini miji mkibuwa hukumbwa na uchafuzi kuliko sehemu nyingine? (alama 2)
(f) Eleza nui **mbili** za uchafuzi wa mazingira zilizotajwa katika kifungu hiki.(alama 2)

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

(g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika kifungu: (alama 2)
   (i) Msambao:
   (ii) Makopo:

**2. UFUPISHO: (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Ukeketaji ni mfumo wa upasuaji unaofanyiwa wanawake na wasichana sehemu nyingi duniani. Istilahi hii ya ukeketaji ina maana pana kwani inaweza kutumiwa kuelezea upashaji tohara kwa wasichana na ukataji wa sehemu za siri kwa wanawake.

Ukeketaji haupatikani tu katika bara la Afrika bali katika sehemu nyingi ulimwenguni. Umri ambapo ukeketaji hufanyika hutegemea jamii inayohusika. Mwanamke anaweza kufanyiwa ukeketaji siku chache baada ya kuzaliwa au baada ya kujifungua mtoto wake wa kwanza. Miongoni mwa jamii ambazo hupasha tohara wanawake, huthamini sana amali hii kwani kwao ni hatua muhimu ya mpito wa maisha katika jamii za jadi mwanamke hupitishwa kutoka rika moja hadi lingine, yaani kutoka utotoni na kuingia kwenye utu uzima. Ukeketaji unafungamana na sherehe ya kuwapa wasichana mafunzo kuhusu kanuni za uzazi, malezi na ndoa. Dhima kuu ya sherehe hiyo ya kuwapasha wasichana tohara inadaiwa ya kwamba ni kuwapunguzia wanawake uchu na kuhifadhi ubikira. Jamii nyingine hutekeleza tohara kwa sababu za kidini zinazoshikilia kuwa mwanamke aliyetahiriwa huwa nadhifu. Wengine wanaamini kuwa tohara huwafanya watoto wanapozaliwa kuwa na nafasi nzuri ya kuishi, ilhali wengine hupashwa tohara ili wapate waume wa kuwaoa. Kwenye jamii ambazo wanaume wanasisitiza tohara kama kigezo cha mwanamke kuolewa ukeketaji umeshamiri. Katika jamii kama hizi wanaume huwa hawataki kuoa wanawake ambao hawajatahiriwa.

Wanawake wenyewe huhakikisha ya kwamba watoto au wajukuu wao wanapelekwa kupashwa tohara. Wakati mwingine mipango ya siri hupangwa na kina mama hao pamoja na mangariba, kuhakikisha kuwa jambo hili linatekelezwa. Kwa hivyo jambo hili la ukeketaji lina utata miongoni mwa jamii nyingi ulimwenguni.

Hata hivyo ukweli ni kwamba swala zima hili la ukeketaji lina madhara makubwa na linamdhalilisha mwanamke. Katika hali ya upashaji tohara wanawake huvuja damu nyingi na aghalabu huaga dunia. Wale wanaopona huwa kwenye hatari ya kuambukizwa maradhi ya zinaa ambayo huharibu sehemu za uzazi. Kwani madaktari wanadai uchungu wa uzazi huwa mwingi na hudumu muda mrefu.
Kwa sababu tohara hufanywa mara moja kwa mwaka, wasichana wote wa rika moja hukusanyika mahali maalum ili kufanyiwa tohara. Kifaa ambacho hutumiwa sana ni wembe. Wembe huo hutumiwa kuwakatia wasichana wote ambao wanapashwa tohara katika kipindi hicho. Wembe huo hauchemshwi angalau kuua viini vinavyosababisha na kueneza magonjwa mbalimbali. Hali hii

huwaweka wasichana hao kwenye hatari ya kuambukizwa ugonjwa hatari wa ukimwi. Licha ya hivyo wasichana waliotahiriwa nguvu za kinga dhidi ya magonjwa hupungua. Kwa hivyo wanaweza kupata magonjwa mengine ya kuambukiza kwa urahisi. Kwa hivyo ukeketaji ni tendo la hatari na la kumdhalilisha mwanadamu ambalo linastahili kulaaniwa.

for freepast papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Maswali**

(a) Ukizingatia mambo muhimu anayoeleza mwandishi, fupisha aya tatu za kwanza. (Maneno 70)
(alama 9, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

(b) Eleza mambo anayoeleza mwandishi katika aya mbili za mwisho. (Maneno 50)(alama 6, 1 ya mtiririko)

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

**Matayarisho**
**Nakala safi**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Eleza tofauti iliyopo kati ya jozi hii ya sentensi. (alama 2)
(i) Rehema alinikimbilia
(ii) Rehema alinikimbia

b) Yakinisha (hali ya kukubali) huku ukigeuza sentensi ifuatayo katika nafsi ya pili kwa umoja
Nisiposamehewa na Mola sitapata amani mchana kutwa. (alama 2)

c) Eleza kwa kutolea mifano matumizi **mawili** ya kiambishi maalu "Ku." (alama 2)

d) Andika sentensi zifuatazo kwa wingi. (alama 2)
(i) Ngoma ile inalia vibaya kwa kuwa imepasuka.
(ii) Ni mlango upi uliofungwa na wewe nilipoenda maktabani?

e) Tunga sentensi ukitumia vihisishi hivi. (alama 2)
(i) Ahaa!
(ii) Taib!

f) Geuza kitenzi kilichopigwa mstari kiwe jina bila kubadilisha maana ya sentensi.(alama 2)
Walimu wanawajibika kuwakomeza vyema wanafunzi wao.

g) Andika sentensi zifuatazo kwa kufuata maagizo. (alama 2)
(i) Watoto wanakumbana na dhiki kubwa kuna haki za watoto (Anza: Fauka ya ....)
(ii) Tarishi alikula staftahi. Tarishi aliend Ofisini (Anza: Licha ya .......)

h) Andika neno jingine lenye maana sawa. (alama 2)
(i) Heshima:
(ii) Ruhusa:

i) Eleza maana ya misemo ifuatayo. (alama 2)
(i) Enda jongomeo:
(ii) Piga unyende:

j) Tunga sentensi ukitumia neno "kile" kama
(i) Kivumishi (alama 1)
(ii) Kiwakilishi (alama 1)

k) Eleza tofauti iliyopo kati ya tanakali hizi za sauti. (alama 2)
Anguka chubwi na anguka tapwi.

l) Tunga sentensi za kuonyesha kuwa unaelewa tofauti kati ya maneno yafuatayo. (alama 2)
(i) Gati
(ii) Kati

m) Tumia –enye au –enyewe kukamilisha sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) Shule ............................. shida daima husaidiwa.

(ii) Kucheza ........................... kulikuwa kwa kupendeza.

n) Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi vifuatavyo vikiwa katika hali ya kufanyiza.(alama3)
(i) La:
(ii) Nywa:
(iii) Fa

o) Andika neno **moja** lenye sauti king'ong'o. (alama 1)

p) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia kielelezo cha mstari. (alama 3)
Samaki huogelea mtoni.

q) Andika sentensi inayoonyesha 'ki' ya masharti. (alama 1)

r) Onyesha viambishi awali na tamati katika kitenzi. Alimkemea. (alama 2)

s) Bainisha matumizi ya 'ni' katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) Ondokeni

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

(ii) Kiptoo ni mwizi sugu:

t) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii. (alama 2)

(i) Alimpigia simu

4. **<u>ISIMU JAMII (ALAMA 10)</u>**

(a) Eleza majukumu **<u>matatu</u>** ya lugha ya taifa. (alama 3)

(b) Fafanua mtindo wa lugha uliotumiwa katika taarifa ifuatayo huku ukieleza sababu za matumizi ya vitambulisho maalum vya lugha. (alama 4)

Wananchi, mimi sina mengi. Hapana katika nyinyi asiyenielewa. Sina la kusema, ila ninawakumbusheni kuwa mnahitaji kiongozi atakayeshughulikia maslahi ya taifa zima. Mtu huyo ni mimi na ninajitahidi niwezavyo kujenga masoko, barabara, shule zaidi na mazahanati na maisha yenu yatakuwa ya raha zaidi.

(c) Thibitisha kuwa adabu za lugha hazizingatiwi miongoni mwa wanajamii siku hizi. (alama 3)

# Set6

**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

**<u>SEHEMU YA A: USHAIRI (SWALI LA LAZIMA)</u>** (alama 20)

1. **<u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.</u>**

1) Nilifika Nairobi, jiji bora na mufti,
Palipojaa <u>shababi</u>, wazee na mabenati,
Nikasalimu kibibi, kanijibu eti fiti!
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

2) Kibibi kasonga kwangu, nimpe kiti asiti,
Nikaona mbele yangu, kwa mapozi kajiseti,
Sikupatwa na uchungu, wala chembe kibuhuti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

for free pastpapers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

3) Kumwuliza wenda wapi, kanijibu marikiti,
Kwenye kazi au vipi, jibu lake nina deti,
Ana majibu mafupi, na taimu hawesti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

4) Mtu huyu hushangaza, lugha yake sijageti,
Hataki kunisikiza, ati mimi sina senti,
Bila doo aeleza, yu tayari kunibuti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

5) Punde dakika kidogo, nikaanza utafiti,
Naona ana <u>mikogo</u>, na haogopi umati,

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Hawataki wa ushago, wenye koti bila noti.
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

6) Ni kibibi maridadi, ila mambo tofauti,
Asema mboga si fudi, bwana kunipa donti,
Chuma mobu sina budi, kujaza langu poketi
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

7) Ana fujo hatulii, sijaonapo laiti,
Arifu hunibalii, kamsosi hata switi,
Ebu acha uchalii! Huji homu kwa kufuti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

8) Na kutaka kualee, akawasha sigareti,
Hamuogopi madhee, asije kumripoti,
Pegi mbele ya fadhee, mkali kama ghosti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

9) Alipozidi udhia, nikaanza kumsweti,
Naye akaniwevia, kuniona simfati,
Sistee kaingia, kwa motii kalosti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

10) Nikabaki kudangana, la kusema silipati,
Lugha zetu kulingana, hakuna japo katiti,
Ndipo hatukuelewana, hadi kuenda benati,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

11) Kudadisi kwa makini, tabia na harakati,
Za vijana wa mjini, zina nyingi atiati,
Tafadhali jikanyeni, ni huu ndio wakati,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

12) Hunishangaza jamani, tuelezane kwa dhati,
Nairobi mitaani, pa watu watanashati,
Panasemwa lugha gani, na kanuni haifati!
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**MASWALI**

(a) Mtunzi wa shairi hili ana dhamira gani? (alama 2)
(b) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili ukizingatia: (alama 4)
  d. Vina
  e. Vipande
(c) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, onyesha aina **mbili** za idhini ya kishairi katika shairi hili. (alama 4)
(d) Taja na ufafanue tamathali **mbili** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili(alama 4)
(e) Andika ubeti wa kumi katika lugha nathari. (alama 4)
(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao ulivyotumika. (alama 2)
  (i) Shababi

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

(ii) Mikogo

**SEHEMU YA B: RIWAYA – KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA**

**Jibu swali la 2 au 3**

2. "Wema wako umeniua kabisa. Kuna mahakama ndani ya moyo wangu nanakojishtaki mwenyewe…."
(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
(b) Taja na ueleze tamathali mbili zilizotumiwa kwenye muktadha huu. (alama 4)
(c) Ukirejelea Riwaya nzima, jadili makosa ambayo mnenaji wa maneno haya anajishtaki kwayo. (alama 12)

3. "Amani ni mhusika anayestahili kuigwa katika jamii." Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

**SEHEMU C: TAMTHILIA**

***MSTAHIKI MEYA (TIMOTHY M. AREGE)***

**Jibu swali la 4 au 5**

4. "Tunaweza kutangaza katika vyombo vya habari. …. Watu wengi huko nje wana njaa."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Fafanua sifa **mbili** za mzungumzaji wa dondoo hili. (alama 2)
c) "Hali inayoipata Cheneo katika muktadha ambambo dondoo hili limekitwa ni msiba wa kujitakia." THibitisha. (alama 14)

5. Anwani 'Mstahiki Meya' ni kinaya. Jadili. (alama 20)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI.**

**K. Walibora na S.A. Mohammed - Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.**

**Jibu swali la 6 au la 7**

***"Damu Nyeusi" (K. Walibora)***

6. "Waafrika hupitia matatizo mbalimbali wakiwa masomoni ughaibuni." Jadili. (alama 20)

**au**

***"Ndoa ya Samani" (Omar Babu)***

7. "Hapa huingii bila kunionyesha mkono."
(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Eleza sifa **mbili** za msemaji katika dondoo hili. (alama 4)
(c) Jadili maudhui sita yanayojitokeza katika hadithi hii. (alama 12)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

8.
(a) Eleza sifa **tano** bainifu za fasihi simulizi. (alama 5)
(b) Taja njia **mbili** za kisasa za kuhifadhi fasihi simulizi. (alama 2)
(c) (i) Eleza sifa za misimu. (alama 7)
(ii) Taja njia mbalimbali za kuunda misimu katika jamii. (alama 6)

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

**Set7**
**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

---

1. **<u>INSHA YA LAZIMA</u>**
   Wewe ni katibu wa jopo lililoteuliwa kuchunguza changamoto zinazokabili uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili nchini.Andika ripoti hiyo.

2. Samaki mkunje angali mbichi.

3. Serikali za ugatuzi zitakuwa na manufaa kwa maendeleo ya nchi.Jadili.

4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya.........
   Niliyakumbuka maneno ya mwalimu mkuu,machozi yalitoka njia mbilimbili.Hayawi hayawi huwa.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Set7**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

---

1. **<u>UFAHAMU (ALAMA 15)</u>**
   **<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanoyofuatia.</u>**
   **Malengo ya maendeleo ya Milenia**

Malengo ya maendeleo ya Milenia (yajulikanayo kwa kimombo kama Millenium Development Goals (MDG), Ni malengo manane ya nchi wanachama wa umoja wa mataifa, ambayo nchi hizi zilikubaliana kujitahidi kutimiza kufikia mwaka wa 2016.Azma ya kufikia malengo haya ilizinduliwa rasmi mnamo septemba 2000 katika azimio la millennia la umoja wa mataifa.Wakati wa uzinduzi, mataifa yote 189 wanachama wa umoja wa mataifa yalihusika.Kwa sasa, mataifa wanachama yameongezeka na kufikia 193 na yote yanajizatiti kutekeleza azma hii.

Azma ya kwanza ni kukomeza au kupunguza umaskini uliokithiri kwa asili 50 miongoni mwa watu ambao kipato chao ni chini ya dola moja kwa siku.Aidha lazima hii inalenga kupunguza kwa kiasi hicho idadi ya watu wanaokumbwa na dhiki ya njaa kufikia mwaka wa 2016.Kwa kielelezo, kwa mfano vijiji viitwavyo 'vijiji vya milenia'vilianzishwa katika nchi sahara,ambazo ni Uhabeshi, Ghana, Kenya, Malawi, Rwanda, Nigeria, Senegal, Tanzania na Uganda vilichaguliwa.Wakazi hawa wanapookolewa kutoka kwa ulitima, hatua zilichukuliwa vijijini humu yanaonyesha athari chanya.Kunayo matumaini.

Lengo la pili lilikuwa kutimiza elimu ya msingi kwa wote chini ya wito 'Elimu kwa wote', yaani kwa kingereza Eduction for All (EFA) kufika mwaka wa 2016.Nchini Kenya, elimu ya msingi ilifafanuliwa upya katika katiba mpya ya 2010, ikawa yaanzia shule ya chekechea hadi kidato cha nne. Aidha imetajwa kuwa ya lazima, kwamba mtoto sharti ahudhurie masomo.Ina maana kuwa mzazi analazimika kumpeleka mtoto shuleni. Lengo pia lipo, kuhakikisha watoto wote wa jinsia za kike na kiume wanahitimu.

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Lengo jingine ni kuwania usawa wa kijinsia kwa kuhakikisha kuna nafasi sawa kwa wote.Katika janibu nyingi za wanachama wa umoja wa mataifa, wanawake kwa miaka ya ayami walionekana kuwa chini ya wanaume kutokana na taasubi ya kiume, mwanamke alifaa kuwa chini ya mwanamume.Hatua ya kwanza ya malengo ya maendeleo ya millennia inanuia kuondoa tofauti ya uwiano wa wasichana na wavulana katika elimu ya msingi hadi sekondari ifikapo mwaka 2005; na katika ngazi zote za elimu ifikapo 2016. Kuondoa utoro miongoni mwa wahudhuriao masomoni hutahakikisha usawa huu.

Lengo la nne ni kupuuza vifo vya Watoto wa umri chini ya miaka mitano kwa theluthi mbili kufikia mwaka wa 2016. Jitihada zinatiwa kuhakikisha kuwa kina mama waja wazito hawazai njiti wala watoto wao hawaagi punde baada ya kuzaliwa.Changamoto imekuwa kwamba watoto wengi katika nchi zinazoendelea hufa kabla kufikia umri wa miaka mitano. Mapambano dhidi ya magonjwa kama vile kifaduro, polia na malaria yaliyosababisha vifo hivi pamoja na jitihada za kujizatiti za kufikia lengo hili.

Kunayo azma ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za uzi ili kupunguza kwa robo tatu vifo vya uzazi kufikia 2016. Kua kwa wajawazito kunaashiria huduma duni wakati wa kuhimili.Kina mama wengine katika nchi zinazoendelea hawahudhurii kliniki wakati wakati wa kulea mimba.Kwingineko, huduma hizi huwa mbali sana, huku namna za usafiri zikiwa duni.Kina mama huishia ama kuhudumiwa na 'wakunga' wasiohitimu au hata kujifungua pweke .Mataifa wanachama wanahimiza kuongezea zahanati na vituo vingine muhimu vya afya.Kadhalika jitihada zinatiwa kuwaelimisha kina mama na jamii kwa jumla kuhusu umuhimu wa kuhudhuria kliniki wakatiwa ujauzito na kuhakikisha mama yu salama wakati wa kujifungua.

Magonjwa sugu yanayotishia kuwamaliza walimwengu ni kikwazo cha jitihada za walimwengu kujiendeleza.Ndiyo maana lengo la sita ni kupambana na Ukimwi, malaria na magonjwa mengineyo.Kampeni zinaimarishwa katika jumuiya hii kuzuia kabisa na kupunguza maambukizo mapya ya Ukimwi.Jitihada zinatiwa kupunguza au kuzuia kabisa ugonjwa wa malaria au magonjwa mengine hatari. Vyombo vya habari, vituo tamba vilivyo na maafisa wa nyanjani vinatumiwa nyanjani katika mataifa wanachama ili kufaulisha kampeni hii.

Aidha wanachama wanalenga kuhifadhi mazingira kwa kujumuisha misingi ya maendeleo endelevu katika sera na program za nchi.Zinalenga kuzuia upotevu wa rasilimali ya mazingira kama vile miti na maji.Lengo lipokuhakikisha kuwa katika kipindi hiki wanachama watapunguza
kwa asilimia 50 idadio ya watu wanaoshindwa kupata maji safi na salama – hii ni moja wapo ya malengo ambayo, kwa mujibu ya tovuti ya umoja wa mataifa www.un.org/milleniumgoals, kuna matumaini ya kutimiza zaidi ya 2016

Mwisho kuna lengo la kujenga mshikamano wa maendeleo duniani, kwanza kwa kuboresha zaidi mfano wa Fedha na biashara duniani kuhakikisha ni wa usawa, unafuata sheria na kamwe hauna ubaguzi.Utawala bora; kushughulikia mahitaji ya kipekee ya nchi changa kama vile kuziondolea ushuru wa bidhaa muhimu,kuzipunguzia au kuziondolea madeni; kutoa misaada zaidi kwa nchi maskini zinazotia jitihada kutoa umaskini kushughulikia mahitaji muhimu, ya visiwa vidogo na nchi zisizo na bandari miongoni mwa nchi zinazoendelea; kuwapa vijana ajira bora; kushirikiana na sekta za kibinafsi ili kuimarisha teknolojia ya kisasa hasa katika habari na mawasiliano ni baadhi ya yanayozingatiwa kulenga kutimiza mshikamano huu.

**MASWALI.**

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

1. Malengo ya maendeleo ya milenia ni nini? (Alama 2).
2. Ni wachochole wa kiwango gani wanaolengwa kuinuliwa na hatua za malengo ya maendeleo ya milenia? (Alama 1)
3. Taja vipengele viwili muhimu kuhusu elimu katika katiba mpya ya Kenya vinavyo changia kufikia malengo ya maendeleo ya milenia? (Alama 2)
4. Gusia changamoto tano zinazowakabili kina mama wajawazito katika ulimwengu wa tatu. (Alama5)
5. Kampeni dhidi ya magonjwa sugu inafanywa kwa namna gani. (Alama 2)
6. Hali ya maji inatarajiwa kuwaje kufikia 2016. (Alama 1)
7. Eleza maana ya vifungu hivi. (Alama 3)
   a) Hawazai njiti
   b) Vifo vya uzazi.

**UFUPISHO: (Alama 15)**

**Soma kifungu kisha uyajibu maswali yanayofuata.**

Nidhamu ni kitu cha maana sana maishani mwa binadamu. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana.Akiwa na nidhamu hiyo, atakuwa mtu mwadilifu, anayeweza **kustahiwa** na kusadikika katika mambo, shughuli na hali tofauti.

Kwanza, mtoto mwenye nidhamu huwa kama anga au nuru nyumbani mwao, shuleni na pia katika jamii.Watu wote wanampenda na kumheshimu. Wazee kwa **vijulanga** wote wanamtegemea kama msimamizi wa mambo **nyeti** ya maisha yao. Kwa hivyo, ni **dhahiri shahiri** kwamba mwadilifu hunufaika sana, kinyume na mkaidi ambaye wahenga walimwambia kwamba atakosa kufaidi hadi siku ya Idi.

Pili, huwadia nyakati ambapo huwa kuna jambo la busara, **mathalani** jukumu ama dhima fulani ambayo huhitaji tu mwakilishi mmoja darasani, shuleni au katika jamii. Watu hapana shaka watamteua yule mwadilifu kuchukua nafasi kama hiyo. Ndio maana viranja wanaoteuliwa shuleni, huwa ni wanagenzi ambao tayari wamekwisha tiliwa katika mizani na kupigwa msasa madhubuti.

Vile vile, mwadalifu daima atajiepusha na shutuma na majanja yote yanayoweza kuchipuka. Kuna msemo maarufu, kwa busara yake iliyobusarisha mwadilifu kwamba "aliye kando haangukiwi na mti."Pia waliambiwa kwamba, "pilipili usiyoila yakuwashiani?"

Ni bayana kutokana na misemo hiyo miwili kwamba mwenye nidhamu hawezi kuhusishwa na majanga hatari yanayoweza kuyakumba watu.

Walakini ni vyema kujiuliza, je, nidhamu huanzia wapi, na kwa nini kuna baadhi ya 'watoro' ambao ni utovu wa nidhamu? Utovu wa nidhamu huanzia awali sana maishani mwa mja. Mtoto anapozaliwa, anategemea miongozo na mielekeo ya watu wazima ambao wakomazingirani mwake.Ndipo wakale wale waliokaramka walisema kwamba mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha nina.

Hivi ni kusema kwamba, nidhamu au utovu wa nidhamu huanzia nyumbani hadi shuleni, kisha hupanuka hadi kufikia kiwango ambapo mja anatangamana na watu wote katika maisha yake.Ikiwa sehemu moja ya ukuaji wa nidhamu maishani mwa mja itasambaratika, basi hawezi akawa mkamilifu kinidhamu maishani mwake.

Kwa vile ni bayana kwamba mabaya yote ayatendayo duniani hulipwa na Mola papa hapa duniani,watovu wa nidhamu wote huishia kuangamia, ama kujuta mno kwa amali zao potovu.Ni kheri mja kujihidi mwenyewe, kwani uhalifu haulipi chochote.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

a) Nini umuhimu wa nidhamu? (maneno kati ya 50-55) (al. 1 ya mtiririko) (alama 7)

**Matayarisho**

**Jibu**

(b) Bila kubadilisha maana, fupisha aya nne za mwisho. (tumia maneno 55-60)
(alama 1 mtiririko ) (alama 8)

**Matayarisho**

**Jibu**

**MATUMIZI YA LUGHA.**

a) Taja sifa tatu kuu za sauti /k/ (alama 3)

b) Andika sentensi hii katika msemo halisi
Mwalimu alimuambia mwanafunzi amalize kazi hiyo haraka (alama 2)

c) Huku ukitoa mifano, eleza maana ya silabi funge (alama 2)

d) Weka nomino hizi katika ngeli zake (alama 2)
Mbalungi
Mturuki

e) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi, wakati uliopita hali ya kuendelea (alama 2)
Mwalimu humuadhibu mwanafunzi mwenye hatia.

f) Changamua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali (alama 4)
Omondi anaazimia kuwa mhasibu Lakini hatii bidii masomoni

g) Yakinisha katika nafsi ya tatu wingi (alama 2)
Sijasafiri kwenda marekani

h) Bainisha matumizi ya kiambishi 'ku' katika sentensi hii (alama 20)
Naomi atakupikia chai alafu aende kule uwanjani

i) Onyesha virai katika sentensi zifuatazo na ueleze ni vya aina gani. (alama 2)
i) Anachukia kusoma riwaya yenye masuala ya kisiasa.
ii) Watoto wa kike hudunishwa katika jamii nyingi

j) Onyesha matumizi mawili ya alama zifuatazo za uakifishaji (alama 4)
Koloni (:)
Kistari kifupi (-).

k) Bainisha aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo.
Walimu ni watu wasiopendwa wanaposema ukweli kuhusu wanafunzi (alama 3)

l) Eleza sifa mbili za vishazi tegemezi (alama 2)

m) Onyesha matumizi ya kiimbo katika sentensi hii
Ondoka hapa! (alama1)

n) Andika neno lenye maana sawa na (alama 2)
Hawala
Katani

o) Eleza maana ya sentensi hii (alama 2)
Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari na ningalistarehe.

p) Eleza tofauti iliyopo kati ya sentensi hizi (alama 2)
Tulipofika hoteleni tulipewa soda na chupa.
Tulipofika hotelini tulipewa soda kwa chupa

q) Kanusha katika ukubwa ( alama 1)
Mwizi huyu aliiba kisu na ng'ombe wa mwanamke yule.

**ISIMU JAMII**

a) Eleza sababu zozote sita zinazochangia kufa kwa lugha. (alama 6)

b) Taja mambo yoyote manne yanayofanywa na serikali yetu kuimarisha lugha ya Kiswahili
(alama4)

for freepast papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**set7**
**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

1. **SEHEMU YA A: SHAIRI (Lazima) (alama 20)**

Nimechoka
Nilivyofikisha hapa, na juu kupandishwa
Na kwa hila gani, au, zilipofungwa
Ncha za waya hii ngumu ya maisha, sijui.

Wanadamu wameinama.Wanasali kwa haraka sasa.
Utafikiri wanahesabu mchanga utakaojaza kaburi langu.
Vichwa vyeupe vinacheka.Kingine kinasema tena:
"Mnaliona Hilo! Joga !" Vichwa vinachela.Wanasali.
"Nyinyi nyote hamna akili!Mnaniudhi!
Hamwoni hali yangu!" Napiga kelele.Lakini vichwa
Havitishi,na wanadamu hawatingishiki.

Sauti ya baba inasema kwa msisitizo
"Najua utafika wakati itakulazimu kudondoka.
"Lakini unazo nguvu bado,na usikate tamaa,
Ila usitegemee kusifiwa au kusaidiwa;
Vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo,
Nawe kudondoka,utadondoka!

Ninaendelea kuning'inia.Nimechoka.Mikono
Inaniuma;hatari ya vitimbo.Vinacheka.Wanasali
Sasa wanaimba.Sitaki nyimbo zao;maana
Mimi bado nimeniong'inia na vitimbo having'oki.
Lakini pole pole ninaanza kutabasamu.
Sijafikia hatua ya kucheka;maana nimechoka,
Kichomi kimenipata na sijadondoka

Lakini najiona nimening'inia kama ndege
Aliyenaswa na mtego wa mtoto mdogo
Mimi,Lakini ni mwanadamu na akili zangu
Timamu.Ninaweza kudondoka, kama nikipenda.

Lakini ninaogopa chini yangu naona miti
Iliyochongwa ikifuata usawa wa waya hii,
Ikingoja kwa hamu,kama mshikaki kunichoma,
Kunitoboa na kufurahia kimya kimya,
Uzuri wa kupita katika mwili mwororo wa binadamu.
Lazima nishike kwa nguvu nisianguke kama kifurushi
Cha pamba cha mtoto mdogo kilichokwisha pimwa.

Mikono inaniuma, na waya imekwishanikata vidole.
Damu imetiririka hadi kwapani;kujipangusa siwezi.
Nimechoka.Kadiri niendeleavyo kunig'inia, ndivyo

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Sura yangu ionyeshavyo vizuri alama za uchovu.
Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma.
Lakini wanadamu wote wazima wanainamisha vichwa
Chini kama kwamba hawanijui;hata jamaa zangu!

Ninaendelea kuning'inia kama picha iliyotundikwa
Katika shamba la mawele, na mwenye shamba
Huvuta waya kutoka nyumbani,itingishike kuwatisha
ndege.
Machozi yananitoka,kuyapangua siwezi.
Ninajitahidi kutoa sauti kwa nguvu;
"Jamani e! Nisaidie! Ng'oeni hivyo vitimbo!"
Lakini wanadamu wameinama.Wanaanza sasa kusali.

Kati ya vitimbo, vichwa vinazuka ardhini
Ukweli wa maisha unakuwa kama ndoto ya uwongo.
Kichwa kimoja kinasema kwa sauti "Mnaliona Hilo!"
Halafu vichjwa vyote vyeupe vinacheka.Ninashangaa.
Ninashangaa zaidi kusikia sauti ya baba
Ikicheka miongoni mwa vichwa hivyo vyeupe.
Siyaamini macho,siyaamini masikio, sikiamini kichwa.

**Maswali:**

1. Shairi hili ni la "udhanaishi" Fafanua kauli hii. (alama 4)
2. Eleza kwa kutoa mifano miwili, jinsi msanii alivyotumia tamathali zifuatazo (alama 6)
   (a) Jazanda
   (b) Uhuishi
3. Andika ubeti wa saba kwa lugha tutumbi. (alama 4)
4. Eleza maana ya mishororo "vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo, nawe kudondoka utadondoka". (alama 2)
5. Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)

**SEHEMU B: RIWAYA**

**Kidagaa Kimemwozea**

1. "....usiniweke pembeni kama tanbihi, mimi na wanawake wenzangu kama wanaume wengine wafanyavyo waandikapo..."
   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   b) Fafanua mbinu mbili za uandishi zilizotumika hapa (alama 2)
   c) Hakiki usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya hii (alama 14)

2. Wananchi wa Tomoko wamesalia katika ndoto ya uhuru.Dhibitisha ukweli wa kauli hii.(alama 20)

**TAMTHILIA**

**Mstahiki Maya**

3. "Si ninyi nd'o mjuao wanangu!..nilikiona afadhali".
   (a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)

   (b) Taja na utolee mifano ya mbinu zozote mbili za uandishi zilizotumika katika kifungu hiki. (alama 4)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

(c) Fafanua maudhui yanayorejelewa na dondoo hili. (alama 12)

4. "Mtu huvuna alichopanda.Ukipanda pojo huwezi kuvuna kunazi.
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

   b) "Ukipanda pojo huwezi kuvuna kunazi" ina maana gani kulingana na muktadha huu. (Alama 6)

   c) Taja na ueleze matendo mengine manne ya kuonyesha kuwa walipanda pojo na kuvuna pojo si kunazi. (Alama 8)

   d) Taja tamathali za usemi zilizotumiwa katika dondoo hili. (Alama 2)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**
**<u>Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine</u>**
**Ken Walibora na Said A.Mohaned**
**Jibu swali la 5 au na 6**

5). "Kama alivyoshinda nani Yule....nunez?"
   a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake. (Alama 4)
   b) Linganua sifa nne za msemaji na msemewa katika dondoo hili. (Alama 8)
   c) Kwa kurejelea hadithi nzima eleza hisia za utamaduni ulipitwa na wakati. (Alama 6)
   d) Ni mbinu zipi za lugha zilizotumika katika dondoo hili? (Alama 2)

6). Mwanamke katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine amepewa nafasi finyu. Fafanua kwa kuzingatia hadithi zozote nne. (Alama 20)

**SEHEMU YA E. FASIHI SIMULIZI (Alama 20)**

7. a) Eleza maana ya maghani (alama 2)

   b) Fafanua sifa nne za maghani (alama 4)

   c) Taja njia zozote nne za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika jamii. (alama 4)

   d) Fafanua hatua za ukusanyaji wa data katika fasihi simulizi (alama 5)

   e) Eleza matatizo yanaokabili fasihi simulizi katika jamii ya sasa (alama 5)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

# Set8

**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

---

**<u>SWALI LA LAZIMA</u>**

1. Kumetokea shambulizi la kigaidi katika nchi jirani. Wewe kama balozi mwandikie raisi na

watu wa nchi hiyo risala ya rambirambi.

2. Dhuluma dhidi ya wanawake imekita mizizi ndini. Jadili.

3. Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi.

...Na huo ndio ukawa mwanzo mpya.

# Set8

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

---

**UFAHAMU (ALAMA 15)**
**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.**

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na uathihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu msingi mkuu wa uainishaji wa mahusiano hayo ni kukichunguza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache, na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitikadi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hivyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi, na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekena baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya koindi cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mwahali mwa kazi, washirika kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfano wa jamii. Kwa mfano, kwa majirani wanaoishi kwenye janibu, fulani mahususi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri. Uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilkikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi uweza kuumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mapito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi untambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na "uhusiano wa chembe chembe". Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachomshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, kiatu anachokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia n.k. Mahusiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa na kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwezake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiliwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza nji: Je, tunahusiana vipi na jamaa zetu, taasisi zetu, marafiki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni w aaina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

(a) Taja kigezo muhimu cha kuzungumzia mahusiano. (al 1)
(b) Eleza imani ya watu kuhusu uhusiano baina ya jamaa. (al 1)
(c) Fafanua athari ya technolojia kwenye mahusiano ya watu. (al 2)
(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. (al 4)
(e) Taja sifa kuu ya mahusiano ya muda mfupi. (al 2)
(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (al 2)
(g) Eleza maana ya maneno yafutayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (al 3)
   (i) inasigana
   (ii) yameghoshi
   (iii) vighairi

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**UFUPISHO (ALAMA 15)**

Ujambazi wa kimataifa ni tatizo lililowasumbua walimwengu kwa muda mrefu sana. Serikali nyingi zimetumia mapesa mengi kwa miaka mingi sana zikijitahidi kupambana na janga hili. Hata hivyo, fanaka haijapatikana, wala haielekei kamwe kuwa itapatikana leo au karne nyingi baadaye.

Yumkini tatizo kubwa lililopo ni kuhusu jelezi la dhanaya "ujambazi" tena "wa kimataifa". Hili ni tatizo mojawapo na yapo mengi sana. Tatizo la pili ni kiburi. Kuna wale watu binafsi na hasa viongozi w anchi kubwakubwa na serikali zao zilizojiaminisha kuwa ujambaz ni balaa kweli, tena belua, lakini huo ni wa huko, wala hauwezi kuwagusa licha ya kuwashtua wao.

Kulingana na maoni watakaburi hao, ujambazi ni wa watu 'washenzi' wasiostaarabika, wapatikanao katika nchi zisizoendelea bado. Ujambazi peke wanaouona unafaa kukabiliwa ni dhidi ya mbubujiko wa madawa ya kulevya uliosababishwa na vinyagarika kutoka nchi hizo maaluni za "ulimwengu wa tatu". Kulingana na wastaarabu wa nchi zilizoendelea, vinyangarika hivi ndivyo hasa adui mkubwa wa ustaarabu ulimwenguni na ni sharti vifagiliwe mbali bila huruma. Baada ya kusawasagwa, ulimwengu mstaarabu utazidi kutononoka na ahadi ya mbingu hapa ardhini itakamilika.

Imani ya watu hawa ya kuwa ujambazi wa kimataifa, hata iwapo upo, hauwezi kuwashtua wala kuwatingisha wao ilikuwa kamili na timamu. Ilikuwa kamili na timamu hadi hapo mwezi Septemba tarehe 11 mwaka wa 2001, ndege tatu za abiria zilipoelekezwa katika majumba mawili ya fahari, yenye urefu wa zaidi ya ghorofa mia moja na kuyatwangilia mbali. Mshtuko na kimako! Kimako kwa kuwa, kabla ya siku hiyo, Wamarekani hawangeweza kudhani kwamba ingewezekana taifa lolote au mtu yeyote kuthubutu kushambulia nchi yao, taifa wasifa lililojihami barabara dhidi ya aina yoyote ile ya uchokozi kutoka pembe lo lote la dunia.

Hakuna ulimwenguni mzima, aliyeamini kuwa Marekani ingeweza kushambuliwa. Kwa ajili hiyo, mshtuko uliitingisha ardhi yote na huzuni ilitanda kote, kama kwamba sayari nzima imeshambuliwa, wala sio Marekani pekee.

Mintarafu hiyo, Marekani ilipolipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuwemo na wasiokuwemo kwa mabomu hatari huko Afghanistan, idadi kubwa ya watu duniani ilishangilia na kusherehekea. Kwa bahati mbaya, tafsiri ya shambulizi la minara-pacha na Newyork na lile la Pentagon, uti wa uwezo wa kivita wa Marekani, ulizorota. Kuna wengi waliodhani huo ni mwanzo wa vita vya Waislamu dhidi ya Wakristo na kwa muda, Waislamu wote wakashukiwa kimakosa kuwa ni majambazi wa kimataifa.

(a) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za kwanza. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)
Matayarisho
Nakala safi

(b) Ukizingatia aya tatu za mwisho, fafanua fikira za watu na mambo yote yaliyotokea baada ya Septemba tarehe 11, 2001. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)
Matayarisho
Nakala safi

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Silabi ni nini? (al 2)
(b) Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)
(c) (i) igwa
(ii) Oa
(d) Dhihirisha panapotiwa shadda katika maneno yafuatayo. (al 2)
(i) Galagala
(ii) Teketeza

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

(e) Bainisha nomino katika sentensi zifuatazo kisha utaje aina zake. (al 2)
(i) Uhubiri wa mama huyu una mvuto mkubwa
(ii) Kabati hili limevamiwa na wadudu wengi waharibifu.

(f) Eleza matumizi ya kihusishi kwa katika sentensi ifuatayo. (al 2)
Tahadhari huandikwa kwa hati nzito.

(g) Tenga viambishi na mzizi katika neno lifuatalo. (al 2)
Siji.

(h) Unda nomino kutokana na kivumishi kifatacho. (al 1)
Tepetevu

(i) Pigia mstari na kuainisha kirai katika sentensi ifuatayo. (al 2)
Haifai kujenga karubu na nyaya za umeme

(j) Bainisha shamirisho kitondo katika sentensi ifuatayo. (al 2)
Mzalendo amemwandikia mhariri barua.

(k) Eleza kama sentensi ifuatayo ni sahili, ambatano ama changamano. (al 2)
Tulipewa ratiba ya shughuli hiyo lakini hatukuitia maanani

(l) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (al 2)
Simu tamba ambayo ameninunulia imenirahisishia mawasiliano

(m) Kanusha sentensi ifuatayo. (al 2)
Ninamtarajia mpwa wangu awasili leo

(n) Andika katika wingi. (al 2)
Huzuni aliyokuwa nayo yatima huyu ilinitia kite na imani.

(o) Andika kinyume cha neno lililopigwa mstari. (al 1)
Mhalifu huyu alitunga mimba

(p) Bainisha matumizi ya **KI** katika sentensi ifautayo. (al 1)
Jua limekuwa likiwaka tangu Januari

(q) Bainisha matumizi ya **ka** katika sentensi ifuatayo: (al 1)
Sungura alifika nyumbani akamsalimu mkewe, akafululiza msalani akaoga

(r) Akifisha sentensi hii: (al 2)
Mmea wa pareto ni muhimu mno nchini akasema afisa wa kilimo

(s) Badilisha katika usemi wa taarifa: (al 2)
"Tutakusaidia ikiwa utashirikiana nasi," afisa wa usalama akasem.

(t) Andika katika ukubwa ukizingatia neno lililopigwa mstari. (al 1)
Aliyerembesha uso kwa poda.

(u) Bainisha maana mbalimbali za sentensi ifuatayo: (al 3)
Mwalimu amempigia wanafunzi simu

(v) Silabi mwambatano ni nini? (al 1)

(w) Tunga sentensi moja udhihirishe maana mbili za neno hili: Rudi (al 1)

(x) Pigia mstari vivumishi katika sentensi ifuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)
Bibi huyu ni mpole uso wake wenye haya huuinamisha kila mara.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

**Set8**
**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

**SEHEMU YA A**
**LAZIMA**
**FASIHI SIMULIZI (ALAMA 20)**

(a) Toa sifa mbili za fasihi simulizi. (al 2)
(b) Taja na ufafanue aina mbili za hadhira wa fasihi simulizi. (al 2)

(c) Hadithi za kisalua ni nini? (al 1)
(d) Fomyula ya kuhitimsha ina umuhimu gani? Toa hoja mbili. (al 1)
(e) Eleza sifa mbili za hadithi za mazimwi. (al 2)
(f) Ni nini dhima ya misimu katika jamii? (al 2)
(g) Ushairi simulizi ni nini? (al 1)
(h) Taja sifa mbili za hodiya. (al 2)
(i) Eleza sifa tatu za mwigizaji bora. (al 3)
(j) Eleza sifa mbili za ngoma. (al 2)
(k) Tofautisha kati ya malumbano ya utani na maapizo. (al 2)

**SEHEMU YA B: RIWAYA**
**KIDAGAA KIMEMWOZEA: KEN WALIBORA**

1. "We bwana unafikiri natumia petroli nini?"
   (a) Uweke usemi huu katika muktadha wake. (al 4)
   (b) Huku ukitoa mifano, eleza mbinu mbili za lugha zilizotumiwa na mwandishi katika dondoo hili. (al 4)
   (c) Eleza migogoro yoyote sita inayojitokeza katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (al 12)
2. Udhalimu ni maudhui makuu katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. Thibitisha. (al 20)

**SEHEMU C: HADITHI FUPI**
**DAMU NYEUSI: KEN WALIBORA & S. A. MOHAMMED**

1. "Wenzangu wote, mwafahamu hadithi ya kobe?"
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)
   (b) Fafanua sifa 4 za msemaji. (al 4)
   (c) Kwa kiurejelea dondoo taja mbinu inayojitokeza katika hadithi inayorejelewa na msemaji. Kisha ufafanue kwa mifano mwafaka. (al 12)
2. Kwa kurejelea hadithi zifuatazo jadili maudhui ya:
   (i) Tamaa na ubinafsi katika Samaki wa Inchi za Joto.
   (ii) Ushirikina katika Gilasi ya Mwisho Makaburini.

**SEHEMU D: TAMTHILIA**
**MSTAHIKI MEYA: TIMOTHY AREGE**

(i) "Si vyombo vya habari, si wanasiasa. Si wasomi."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)
   (b) Taja na ufafanue mbinu ya lugha katika dondoo hili. (al 2)
   (c) Fafanua sifa zozote nne za msemaji. (al 4)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

(d) Umaskini ni tatizo kuu katika cheneo. Tetea kauli hii huku ukitoa mifano mahususi. (al 10)

(ii) Mwandishi wa Mstahiki Meya ametumia mbinu ya majazi kufanikisha ujumbe wake. Jadili. (al 20)

**SEHEMU E: MASHAIRI**

**Shairi**

Mapenzi kitu ajabu, yakutia bumbuwazi
Yakufanya uwe bubu, kujibu huwa huwezi
Shubiri kwako zabibu, na vitamu huviwezi.

Wamkuta kaemewa, asemayo hayajuwi
Aumba akiumbuwa, aona maruwiruwi
Vigumu kumuopowa, na kwa ngisi kumvuwi.

Hukumbuka ya zamani, yote walofanyiana
Nyumbani barabarani, ayaona kama jana
Akili yake na nyani, aruka ingagongana.

Wangoja nyota ya jaha, kutwa wewe unahaha
Mawazo yako silaha, akukwaaye usaha
Usifanyiwe msaha, waugeuza karaha.

Kalelewa kaleleka, utani kwake ni mwiko
Njiani yeye na kaka, hapokei mauliko
Ghadhabu zake zap aka, hapendi maziko.

*Na Hashil S. Hashil*

1. Andika kichwa mwafaka cha shairi hili. (al 1)
2. Eleza umbo la shairi hili. (al 4)
3. Tambua tamathali za usemi alizozitumia msanii. (al 4)
4. Taja na ufafanue uhuru wa mshairi. (al 2)
5. Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (al 4)
6. Fafanua mambo matatu yanayohusishwa na mapenzi. (al 3)
7. Taja nafsi katika shairi hili. (al 1)
8. Taja toni ya mshairi huyu. (al 1)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Chaguo shairi moja kasha ujibu maswali.**

Mtazameni ....nguzo ya Afrika
Mtumwa wa watumwa waliridhiya
Amekita jembe lake akilisujudia
Kwa tambo lililoumbuka na kusekehea
Uso ukifuka ukata ulojifanya tabia
Na machungu ya maonevu alovumilia.

Moyo wake mzito ulokokomaa kama kuni
Haujui tena kutarajia wala kutamani
Umekufa ganzi, kutohisi raha huzuni
Basi iteni fikira mambo ukiyafikiri
Siku hamaki yake itakapochafuka kama bahari
Siku ukweli wa hali yake utapodhihiri

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Umejiandalia vipi...
Huo mkono ulomuumbua na kumkausha
Kizo pumzi zilomzima taa ya maisha
Kumfunga kizuizi , gizani kumtowesha
Ni jawabu gani alowekewa na wakati
Kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti
Kuikiwaza hamaki ya njaa hii ya dhati
Jnjaa ya maisha itakayo kushibishwa.

1. Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (al 2)
2. Taja nafsi neni katika shairi hili. (al 2)
3. Andika mifano ya uhuru wa mshairi katika shairi hili. (al 4)
4. Eleza mbinu za lugha zilizotumiwa. (al 4)
5. Eleza sifa zilizomkabili mzungumzaji. (al 4)
6. Tambua mishororo miwili mishata. (al 2)
7. Fafanua umuhimu wa mistari mishata. (al 2)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

# Set9

**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

---

**INSHA YA LAZIMA**

1. Kumekuwa na visa vya upiganaji wa kabila zinazozozania mifugo katika Kaunti yako. Wewe kama gavana wa kaunti hiyo watumie waathiriwa risala ukiwaeleza hatua zinazoweza kuchukuliwa kupunguza vita hivyo.

2. Hatua ya serikali kuu kumpa kila mwanafunzi wa darasa la kwanza tarakilishi ni ya manufaa sana. Jadili.

3. Andika insha inayodhihirisha methali
Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani

4. Anza kwa
Walipofungua mlango huo, wengi hawakuweza kuzuia hisia zao. Walitoa kwi! kwi! kwa maafa walioshuhudia...

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

**Set9**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

**SEHEMU YA A : UFAHAMU (AL. 15)**

**1. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Kabla ya kuzungumzia umataifa, tuanze udadisi wetu kuhusu neno 'upeo wa Kiswahili". Neno upeo linaashiria mchakato au tendo linalokwenda mbele hatua kwa hatua.

Ndani ya fikra hii ya upeo tunahitaji kujiiliza kwa nini lugha fulani imekwenda harakaharaka au inasotasota katika hali fulani. Nadhani jibu la swali hili haliwezi kukwepa historia ya Kiswahili na Jamii mbalimbali za Afrika Mashariki.

Kulingana na Prof. S.A Mohammed historia au asili ya Kiswahili haijatafitiwa vyema wala kuainishwa vya kutosha kuhusu mchipuko wa asili yake. Hii ni kwa sababu utafiti na uchambuzi wa asili ya lugha ya Kiswahili mpaka sasa hauna umakinifu tokea hapo kale. Mtazamo uliotumiwa kwa wakati wote wa historia ya Kiswahili ni mtazamo wa upekee wa kuegemea taaluma moja wa 'Atomistic Approach' unaotumiwa katika somo la isimu miundo na isimu historia linganishi.

Hata hivyo, lugha si vipashio tu vya ndani ya muundo wa lugha; lugha si mfumo ndani ya mifumo ya lugha. Kwa namna hii ukosefu wa mtazamo wa pekee unabainika wazi. Kwa hivyo, somo la ziada la Isimu Jamii lazima linahitajika katika kufanya utafiti na kugundua asili ya Kiswahili na hata katika kupanua lugha kwa mtazamo na mahitaji ya lugha yenyewe katika mapana ya Jamii husika za Kiswahili zenyewe.

Hata hivyo, katika kutafuta asili ya lugha ya Kiswahili upana wa mtazamo wa pamoja si mshikamano wa Isimu Jamii tu bali mtazamo mpana zaidi unaotarajiwa kuweka pamoja taaluma kadha wa kadha. Kwa mfano inakuwaje kuitafiti asili ya lugha ya Kiswahili bila ya kuitafiti Jiografia pana na ndefu ya lugha ya Kiswahili na ulingano na mpishano wa tamaduni na maumbile ya mwingiliano baina ya mtu na mtu, watu na watu katika jumuiya mbalimbali za Kiswahili.

Au inakuwaje kutotazama uhusiano wa karibu wa kuishi pamoja katika eneo ya mwambao ya Afrika Mashariki na majirani wao wa Afrika Mashariki? Prof. Mohammed hapa anaelekea kutuambia ni vigumu kutafiti asili ya lugha ya Kiswahili. Na hata tukifanya hivyo, inakuwaje wataalamu wanakimbia u-nje wa lugha ulioko ndani ya historia ya lugha ya Kiswahili katika asili au chipukizi zake? Inakuwaje wataalamu hao kutoangalia mfumo wa maisha ya wazawa wa lugha na wale wasiokuwa wazawa wa lugha hii, ambao lugha na tamaduni zao kwa kiasi zinafanana kwa juu juu au undani zaidi?

Je, kwa nini asili ya Kiswahili haitazamwi na kulinganishwa na kutofautishwa katika Nyanja mbalimbali za taaluma kama vile Fasihi simulizi, Ufinyazi, sosholojia, Antropolojia, Historia Simuliza, Taaluma za Tamaduni za kale zinazohusiana na Mazimu, Matambiko, Harusi, Mazishi, Vitiba, Sadaka n.k.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Maswali**

a. Yape makala haya anwani mwafaka (alama 2)

b. Kwa nini historia au asili ya Kiswahili haijatafitiwa vyema kulingana na S.A Mohammed (alama 2)

c. Je, S.A Mohammed anapendekeza mambo yapi yazingatiwe katika utafiti wa asili ya lugha ya Kiswahili (alama 5)

d. Ni nini umuhimu wa Isimu Jamii katika utafiti wa asili ya Kiswahili (alama 2)

e. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu (alama 4)
   - i) Inasotasota
   - ii) Umakinifu
   - iii) Isimujamii
   - iv) U-nje

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Dhana ya kupatalizwa tuliyo nayo haitokani na hofu ya vita na sababu za vita hazikuzushwa na Sayansi. Utaalamu huu haukuunda vita, umeukuza ujuzi wa vita na kuupotoa.

Kwanza, pasi na shaka, Sayansi imeziongeza nguvu za wachochezi wa vita. Zana za kisasa zinaweza kufisha watu wengi zaidi wasijulikane walivyokufa na kuwaua kwa njia ya manyenzi zaidi kuliko zana za zamani. Kila silaha mpya zinazoundwa ni za maangamizi zaidi, ni za kutisha sana hata kuwapa watu kusema kuwa dola zitalazimika kuacha vita kwa hofu ya uharibifu utakaowapata hata wakiwa washindi. Lakini kweli ilivyo ni kuwa hakuna taifa lililosita kuanza vita kwa kucha ati silaha lililo nazo zitaangamiza waliomo na wasiokuwemo. Kuundwa kwa marisau ya kutikisa miji iliyo mbali, kuundwa kwa makombora ya atomiki, hewa za sumu zinazopaliza na kuzuia pumzi au zinazotawanya vidudu vya maradhi au vya kuua mimea, zana zote hizi hazijazuia wala hazitazuia vita.

Lakini lawama kubwa ni ya wataalamu wa sayansi maana utaalamu wenyewe una kunga kama za wachawi na waganga. Kila mtu azicha wala hajui la kuzifanya na hao wataalamu nao wamejiziba katika kunge la kunga hizi kupagaza waja na kujifanya waungu-wa-nti (miungu wa chini). Kwa sababu ya kujiepusha hivi na watu kile kilicho kimegeuka kuwa hofu na kitisho na kila mtu ataka amwepuke mtaalamu wa Sayansi kama anavyomwepuka mchawi na mganga. Ni juu yao kuyaondosha maoni haya na ni juu yetu sote kutoirika vita Sayansi bali tuifanye chombo cha kudumisha amani.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Maswali**

(a) Kwa kuzingatia mambo muhimu, fupisha aya za kwanza mbili (maneno 50-55) (alama 9, 2 utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala Safi**

(b) Fupisha aya ya mwisho bila kupoteza maana asilia (maneno 40-45) alama 6, 1 utiririko

**Matayarisho**

**Nakala Safi**

**SEHEMU YA C: MATUMIZI YA LUGHA NA SARUFI**

a) (i) Eleza tofauti kati ya Irabu na Konsonati (alama 2)

(ii) Taja sifa za sauti /0/ (alama 2)

b) Ainisha vivumishi katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Ukuta wa nyumba ile umebomoka

c) Tunga sentensi sahihi ukitumia msemo ufuatao (alama 1)
Taka Shujaa

d) Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya "a" (alama 1)
Mwanafunzi hula wali

e) Yakinisha sentensi ifuatayo (alama 2)

Asipofika mapema hatampata

f) (i) Eleza maana ya kihusishi (alama 2)

(ii) Ainisha vihusishi katika sentensi ifuatayo (alama 3)

a. Mama atasafiri kutoka Ujerumani hadi Ufaransa.

g) Tunga sentensi moja kutofautisha vitate vifuatavyo (alama 2)

(i) Mbali (ii) Bali

h) Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali (alama 4)

Nilimuona mamba majini nilipopiga mbizi.

i) Eleza sifa mbili za sauti /ng'/ (alama 2)

j) Tunga sentensi ya rai (alama 1)

k) Andika kwa wingi

Kelele ya amchaye Mungu ni Baraka (alama 2)

l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao (alama 4)

S – S1 + U + S2

S1 (T + E + E) Lakini S2 (N + V) (T + N)

m) Tofautisha kiwakilishi nafsi huru na kiwakilishi nafsi ambata katika sentensi (alama 2)

n) Andika katika usemi halisi (alama 3)

Mwalimu aliomba kitabu cha Kiswahili

o) Tunga sentensi ukitumia mofimu huru (alama 1)

p) Andika katika ukubwa wingi

Nguo iliwekwa kando ya mlango (alama 1)

q) Ni nini maana ya chagizo (alama 1)

r) Tunga sentensi yenye kishazi huru na kishazi tegemezi (alama 2)

s) Tunga sentensi ukitumia tanakali ya sauti ifuatayo 'tifu' (alama 1)

**SEHEMU YA D: ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

1.

(a) Eleza changamoto zinazokumba lugha ya Kiswahili (alama 5)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

(b) Jadili hatua ambazo zimechukuliwa kuimarisha lugha ya Kiswahili (alama 5)

# Set9

**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

**SEHEMU A: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**
**Ken Walibora na Said A. Mohammed**
**Swali la Lazima**

1. ... Hasadiki kama yote yaliyojiri yaliyokuwa mafamba au mazingaombwe au mambo halisi. Mambo mengine yanakuwa kama ndoto au jinamizi...

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
(b) Eleza mambo yote yaliyojiri (alama 10)
(c) Fafanua sifa tatu za anayerejelewa (alama 6)

**SEHEMU B: RIWAYA**

**KEN WALIBORA: KIDAGAA KIMEMWOZEA**
Jibu swali la 2 au la 3

2. ... Huyo mwendawazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi?
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   (b) Jadili uhusiano uliopo baina ya mzungumzaji na maudhui (alama 6)
   (c) Taja mbinu ya lugha zilizotumika katika dondoo (alama 2)

3. (a)Mwandishi wa kidagaa kimemwozea amemulika ukiukaji wa haki za kibinadamu. Jadili. (alama 10)
   (b) Eleza jinsi mbinu rejeshi imetumika katika riwaya ya kidagaa (alama 10)

**SEHEMU C: TAMTHLIA:**
**TIMOTHY AREGE: Mstahiki Meya**
**Jibu swali la 4 au la 5**

4. "...Sisi tunaamini kabisa tunachokitaka ni haki yetu na ya vizazi vingine...
(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
(b) Haki hizi zimekiukwa vipi? (alama 10)
(c) Eleza sifa za anayezungumza (alama 6)

5. (a) Linganua wahusika wafuatao katika Tamthlia ya Mstahiki Meya (alama 12)
   (i) Mstahiki Meya
   (ii) Diwani III
   (b) Methali ni mojawapo wa Tamathali za lugha zilizotumika katika Tamthilia ya Mtahiki Meya. Thibitisha (alama 8)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**
**Jibu swali ya 6 la 7**

6. Angawa mdogo, dagaa, amekomaa
   Kaanga kidogo, dagaa, atakufaa
   Kalia kinaya, dagaa, h'ondoa njaa

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Wa kwako udogo, kijana, sio balaa
Na sio mzigo, kijana, bado wafaa
Toka kwa mtego, kijana, sinyanyapaa

Nasaha kidogo, kijana, ukubwa jaa
Jikaze kimbogo, kijana, acha kukaa
Chimbua mhogo, kijana, usibung'aa

Na wake udogo, dagaa, ndani hukaa,
Kuliko vigogo, dagaa, hajambaa
Hapati kipigo, dagaa, hauna fazaa

Maisha si mwigo, kijana ushike taa
Sihofu magego, kijana, nawe wafaa
Kazana kidogo, kijana, kugaaga

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama 2)
(b) Eleza arudhi zilizofuatwa katika kutunga shairi hili (alama 4)
(c) Onyesha jinsi malenga alivyotumia uhuru wake (alama 3)
(d) Tambua bahari katika shairi hili (alama 3)
(e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (alama 4)
(f) Tambua mbinu za lugha zilizotumika katika shairi (alama 2)
(g) Eleza toni la shairi hili (alama 2)

7.

Eti
Mimi niondoke hapa
Niondoke hapa kwangu
Nimesaki, licha ya risasi
Vitisho na mauaji, siondoki

Mimi
Siondoki
Siondoki siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Kwa mateke hata na mikuki
Marungu na bunduki, siondoki

Hapa
Siondoki
Mimi ni Pahame!
Niondoke hapa kwangu!
Fujo na ghasia zikizuka
Na kani ya waporaji, siondoki

Haki
Siondoki
Kwangu siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Nawaje; waje wanaokuja
Mabepari wadhalimu, siondoki

for free past papers visit www.freekcsepastpapers.com or call:0720502479

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Kamwe
Siondoki
Ng'oo hapa kwangu!
Katizame chini mti ule!
Walizikwa babu zangu, siondoki

Sendi
Nende wapi?
Si hapa kitovu changu
Niondoke hapa kwangu
Wangawa na vijikaratasi
Si kwamba hapa si kwangu, siondoki

Katu
Siondoki
Sihitaji karatasi
Niondoke hapa kwangu
Yangu mimi ni ardhi hii
Wala si makaratasi, siondoki

**Maswali**

a) Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini (alama 2)

b) Taja masaibu anayopitia mzungumzaji (alama 4)

c) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)

d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 3)

e) Tambua matumizi ya mbinu ya usambamba (alama 2)

f) Andika ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)

g) Tambua idhini moja ya mtunzi (alama 1)

h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi (alama 2)
(i) Karatasi
(ii) Nimesaki

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**<u>SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI</u>**

8. (a) Ni nini maana ya ulumbi (alama 2)

(b) Eleza sifa za mtendaji katika ulumbi (alama 8)

(c) Ngomezi zina umuhimu upi katika Jamii (alama 8)

(d) Toa mifano miwili ya ngomezi (alama 2)

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

## Set10

**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

---

1. **Lazima**
   Ukiwa katibu katika wizara ya elimu, uliongozakamatiyakufanyauchunguzikuhusu visa vya udanganyifu katika mitihani ya kitaifa na jinsi ya kukabiliana na changamoto hii. Andika ripoti utakayowasilisha.

2. Wananchi ndio wakulaumiwa kutokana na kuzorota kwa usalama nchini Kenya. Jadili.

3. Andika kisa kitakacho dhihirisha maana ya methali: usipoziba ufa, utajenga ukuta.

4. Andika kisa kinacho mlizikia kwa maneno haya; ……………………………….katu siwezi kuusahau usaliti na aibu aliyoniletea.

## Set10

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

---

Hulka ya binadamu katika maisha yake ni matarajio ya kupata mambo mazuri zaidi kwa kadiri anavyozidi kuishi duniani. Hulka hiyo haiepukiki kwa mtu yeyote ilimradi yungali hai duniani.

Wapo watu wanaofanya kazi kufa na kupona ili kubadili maisha yao au kujiletea hali, watu hawa matumaini yao ni kuona wanaishi vizuri zaidi kesho kuliko walivyoishi jana.

Kadhalika wavivu nao ambao wana tabia ya kutopenda kujishughulisha kutafuta maisha, mawazo yao yanabaki palepale kutarajia maisha bora. Mtazamo huo wa matarajio ya maisha bora uko pia kwa vyombo vyenye dhamana kwa maisha ya watu katika jamii kama vile serikali. Tofauti na mtu binafsi, ambaye huota ndoto hizo peke yake, serikali hushirikisha mipango inayojiwekea ya kuleta hali bora katika jamii, inafanikiwa.

Ndani ya serikali kuna wadau (washika dau) mbalimbali wenye majukumu ya kuhakikisha kuwa mipango inayowekwa inasimamiwa na kutekelezwa katika muda unaotakiwa, ili kukidhi haja ya kuleta maendeleo katika jamii, tofauti na mtu binafsi ambaye wakati mwingine husimama peke yake katika kutekeleza malengo yake hayo.

Serikali ina nafasi nzuri ya kutekeleza malengo kwa kutumia rasilimali zake wakiwemo watu, madini, misitu, ardhi na nyingine nyingi. Matumizi haya ya rasilimali katika kuleta maendeleo, ni

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

jambo muhimu sana katika kutekeleza mipango yake. Kuna sababu kadha zinazotufanya tuishi miaka nenda miaka rudi tukiwa na kiu ya maendeleo na ndoto ambazo zinashindwa kutimia.

Tatizo kubwa lililopo ni kwamba pamoja na kuwa na wataalamu wazuri na sera nzuri, tumeshindwa kuzitekeleza, badala yake tumekuwa mabingwa zaidi wa kuelezea sababu za kushindwa kutekeleza sera hizo kuliko kujikosoa kwa uzembe unaotufanya na kusababisha kushindwa kutekelezwa kwa sera hizo. Jambo hilo limechangia kurudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu kwa miaka mingi. Mipango mingi inayopangwa na serikali, mara nyingi imekwama, matokeo yake badala ya kutafuta udhaifu uliokwamiza kutekelezwa kwa mipango hiyo, nguvu zaidi zinaelekezwa kuhalalisha sababu za kushindwa.

Tunapaswa kujiuliza ni kwa nini tumefikia hapo? Tukipata jibu tukae chini tusioneane aibu, tunyosheane vidole usoni. Tusioneane haya katika kuleta maendeleo.

*(Kutoka gazeti la Majira, Oktoba 31, 2003)*

**Maswali**

a) Upe ufahamu huu anwani mwafaka. (alama 1)
b) Binadamu wote wana hulka moja. Ifafanue. (alama 2)
c) Eleza jinsi serikali ilivyo na uwezo wa kutekeleza ndoto zake (alama 3)
d) Kulingana na taarifa, ni kwa nini serikali hushindwa kuzitekeleza sera zake (alama 2)
e) Mwandishi anatoa wito gani katika aya ya mwisho? (alama 2)
f) Andika methali mbili zinazohusiana na aya mbili za mwisho. (alama 2)
g) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kwa mujibu wa taarifa. (alama 3)
(i) Kukidhi haja
(ii) Kiu ya maendeleo
iii) Tunyosheane vidole usoni

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**SWALI LA PILI: MUHTASARI (Alama 15)**

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

**UFUPISHO**

Katiba mpya imeipa lugha ya Kiswahili hadhi nyingine kuifanya kuwa lugha rasmi kando na kuwa ni lugha ya taifa. Mabadiliko haya muhimu yana changamoto kadhaa.

Kwanza kabisa lugha ya Kiswahili sasa itashindania nafasi sawa na ile ya Kiingereza katika shughuli za kikazi. Swala hapa linahusu majukumu ambayo lugha hizi zitatekeleza. Je, lugha hizi zinatumika mtawalia katika shughuli za kikazi au zitatengewa majukumu maalum?

Lugha ya Kiswahili itachukua nafasi ipi? Kiingereza kitaachiwa nani tukizingatia kuwa kwa muda mrefu lugha ya Kiingereza ndiyo imekuwa lugha tawala katika mazingira haya? Je, wananchi wataweza kufanya maombi kwa lugha ya Kiswahili kando na kuendesha mawasiliano ya kiofisi kwa lugha hii? Kwa kifupi ili kusitokee mgongano wa matumizi ya lugha hizi mbili ni muhimu sana kwa watunga - sera kueleza kinagaubaga mawanda ya matumizi ya lugha hizi mbili katika mazingira ya kikazi.

Changamoto nyingine na muhimu ni kiwango cha maandalizi ya wananchi katika kuyapokea mabadiliko haya. Kwanza, wananchi wanafaa wafahamishwe kuhusu haki yao ya kutumia lugha hii katika mazingira ya kazi. Si ajabu kuwa wao hawana habari kuhusu mabadiliko haya ya kisera. Watumishi wa umma nao wanastahili kupewa mafunzo maalumu kuhusu mbinu za mawasiliano katika Kiswahili ili waendeshe shughuli zao vizuri.

Kwa upande mwingine, vyuo vikuu pamoja na taasisi nyingine za mafunzo zinastahili kutoa kozi ya lazima katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaojiunga nazo ili kuwaandaa kwa mahitaji haya mapya ya kikatiba. Kadhalika, serikali inastahili kuwaandaa wataalamu zaidi wa lugha ya Kiswahili ambao watahusika katika kuwafunza wanaohusika na utekelezaji sera.

Kuna haja pia ya wataalamu wa lugha kuandika vitabu zaidi kwa lugha ya Kiswahili ambavyo vitatoa mafunzo kuhusu mbinu mbalimbali za mawasiliano. Shughuli hii iambatane na ile ya kutafsiri vitabu vilivyoandikwa kwa lugha nyingine kwa ile ya Kiswahili.

Kwa muda mrefu sasa, kumekuwa na tatizo la mitazamo hasi miongoni mwa wananchi kwa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya wananchi wamekuwa na sababu zao za kutoitumia lugha hii wakishikilia kuwa lugha yenyewe ni ngumu.

Aidha, wananchi wengine wamekuwa na uzoefu wa kuzungumza lugha ya kiingereza au lugha nyingine za kigeni huku wakitoa nafasi finyu kwa lugha ya Kiswahili. Serikali Inastahili kutafuta njia ya kuwahimiza wananchi wote kuionea fahari lugha ya Kiswahili, waipende na kuielewa vizuri.

Ni muhimu kufanywe kila juhudi kuhakikisha kuwa wananchi wanatumia Kiswahili sanifu ili wasije wakakivuruga kwa kukiendeleza visivyo au kwa kukiharibu kwa kijilugha cha sheng au kwa lugha za kienyeji.

Vile vile, ni muhimu wananchi watambue kuwa nchi yetu ya Kenya ndiyo kitovu cha lugha hii na hivyo basi wafanye kila juhudi kuitumia ipasavyo ili tusionekane kuwa watumwa katika lugha yetu asili. Tunahitaji viongozi vielelezo nchini ambao wanazungumza Kiswahili sanifu kwa madoido na ufasaha sio tu katika ulingo bali pia katika nyanja nyingine za maisha.

for freepastpapers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Kwa hivyo viongozi wetu wajiepushe na matumizi ya Kiswahili chapwa ili wananchi wahimizike kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha. Ingekuwa hata bora ikiwa wangepewa kipaumbele katika kupokea mafunzo kabambe katika lugha hii. Pengine tungejifunza mengi kutoka nchi jirani ya Tanzania ambayo kwa kiasi kikubwa ilifaulu kurasmisha Kiswahili na kuleta umoja wa kitaifa.

**MASWALI**

a) Fafanua changamoto zinazoikumba lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi. (Maneno 70) (alama 6, 1 mtiririko)

Matayarisho.

Jibu

b) Mwandishi ametoa mapendekezo kuhusu namna ya kuimarisha matumizi ya Kiswahili nchini. Yafafanue. (Maneno 80) (alama 7, 1 mtiririko)

Matayarisho

Jibu

***MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)***

(a) Andika vigezo vitatu vinavyotumiwa katika kuainisha irabu (alama 3)

(b) (i) Eleza maana ya mofimu. (alama 2)

(ii) Toa mfano mmoja mmoja wa mofimu huru na mofimu tegemezi. (alama 2)

(c) Kwa kutoa mifano onyesha majukumu manne ya viambishi awali. (alama 2)

(d) Tunga sentensi ukitumia nomino katika ngeli ya I-ZI kudhihirisha ukubaliano wa kisarufi. (alama 2)

(e) Yakinisha sentensi ifuatayo (alama 2)

Mtu asiyeugua hahitaji daktari.

(f) Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeana (alama 2)

-la

- nywa

(g) Bainisha yambwa tendwa na yambwa tendewa katika sentensi hii. (alama 2)

Ninamtaka mwanafunzi aniandikie barua.

(h) Tambua aina za vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Tulimtembelea alipokuwa mgonjwa.

(i) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale. (alama 4)

Wale wazuri sana watatuzwa zawadi nyingi.

(j) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo (alama 2)

Mtoto anapendezwa na ziwa

(k) Andika sentensi tatu zenye kudhihirisha matumizi mbalimbali ya KI. (alama 3)

(l) Andika kwa usemi wa taarifa. (alama 3)

"Tafadhali, nifungulie mlango sasa. Nitanyeshewa." Mtoto akamwambia.

(m) Andika katika ukubwa. (alama 2)

Mwanamwali huyu alijinunulia viatu vya ngozi.

(n) Andika matumizi mawili ya mshazari. (alama 2)

(o) Eleza matumizi ya neno mzee katika sentensi zifuatazo (alama 2)

(i) Baba mzee amelewa

(ii) Mzee amelewa

(p) Tumia neno 'kuwa' kama kitenzi kishirikishi kikamilifu katika sentensi alama 1)

(q) Tumia amba katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Alaye ndiye aliaye

For free past papers visit www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

***ISIMU JAMII (Alama 10)***

(a) Eleza tofauti kati ya kuchanganya ndimi na kuhamisha ndimi. (alama 2)

(b) Andika sababu nne za kuchanganya na kuhamisha ndimi. (alama 4)

(c) Kiswahili ni lugha ya kibantu kulingana na ushahidi wa ki-isimu. Thibitisha kauli hii. (alama 4)

# ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

**SWALI LA LAZIMA**

1. ***Soma shairinakishauyajibumaswaliyanayofuata.***
***(AbdallaAbdilalif, sautiyadhiki)***

Chema hakidumu, kingapendekeza,
Saaikitimu, **kitakuteleza,**
Ukawanahamu, kukingojeleza,
Huwanivigumu, kamwehutaweza.

Chemasikiimbi, kwambanakitweza,
Japomaratumbi, kinshaniliza,
Na japosiombi, kipaten'ongeza,
Mtuhaniambi, pa kujikimbiza.

Chemamarangapi, kin'niondoka,
Mwananguyuwapi?Hakukaamwaka,
Kwamudamfupi, aliwatilika,
Ningefanyalipi, elakumzika?

Chemawangubabu, kibwanaBashee,
Alojipatabu, kwambaanilee,
Na yakwesababu, ninitengenee,
Ilhaliwahhabu, maraamtwee.

Chemawanguponi, kipenzinyanyangu,
Hadisikuhini, yumoyonimwangu,
Yu moyonindani, hadikufakwangu,
Ningamtamani, hatarudikwangu.

**Maswali**

a) Lipe shairi hili anwan imwafaka (al. 2)
b) Eleza bahari **mbili** zinazojitokeza katika shairi hili (al. 4)
c) Ni nini maudhui ya shairi hili? (al. 2)
d) Onyesha matumizi ya aina **tatu** za uhuru wa ushairi (al. 3)
e) Eleza umbo la betimbilizamwisho. (al. 4)
f) Taja na kuonyesha tamathali **mbili** za Lugha zilizoko kwenye shairi hili. (al. 2)

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

g) Fafanua msamiati huu kwa muktadha wa shairi hili (al. 3)

i) Kitakuteleza
ii) Kinshaniliza
iii) ela.

**SEHEMU B: TAMTHILIA**
***MstahikiMeya* – T. Arege**
***Jibuswali la 2 au 3***

2. "Nanyi vile vile msikate tamaa. Endelee ni kushinikiza kumwona Meya. Mlango hatimaye huenda ukasalimu armi."
a) Weka dondoo hili haya katika muktadha wake. (ala. 4)
b) Taja kwa kutoa mifano; tamathal izozote **mbili** za lugh azilizotumika katika dondoo hili. (ala. 4)
c) Kwa kurejelea hoja **sita**, eleza ni kwanini wanao rejelewa wanakaribia kukata tamaa. (ala.12)
3. Onyesha vile mwandishi ameshughulikia ukosefu wa kuwajibika katika tamthilia ya MstahikiMeya. (ala. 20)

**<u>SEHEMU C: RIWAYA</u>**
**Ken Walibora: KidagaaKimemwozea**
***Jibuswali la 4 au 5***
4. ......wanaume wange wastahiwa na wake kidogo, wawaoneka maabiria wenzao katika mashua, dunia ingekuwa pahali pema zaidi pa kuishi.
a) Tambulisha mbinu **mbili** za kifasihi zilizotumika katik adondoo hili. (alama 4)
b) Thibitisha kwa mifano **mitatu** jinsi msemaji hakustahi wanamume wake. (alama 6)
c) Taja**maudhui**yanayojitokezakatikamanenohayayamsemaji. (alama 2)
d) Fafanua maudhui uliyotaja kwa kuitolea mifano mingine **mine** kutoka kwenye riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 8)
5. "Mwandishi wa Kidagaa kimemwozea amepata ufanisi mkubwa katika matumizi yake ya mbinu ya kweli kinzani." Fafanua kwa kutoa mifano mwafaka (al.20.)

**<u>HADITHI FUPI</u>**
***Damu Nyeusi na Hadhithi Nyinginezo* – S.A Mohamed**
***Jibuswali la 6 au 7***
6. "Mimi nilitaka mke, mwana mke mbichi ni mvumbike mwenyewe mpaka aive."
a) Weka dondoo hili haya katika muktadha wake (ala. 4)
b) Ni kwa nini msemaji alitaka amvumbike mwanamke mwenyewe? (ala. 4)
c) Eleza migogoro iliyochipuka baina ya msemaji na mwanamke huyu. (ala. 12)
7. Fikirini alicheka kila aliposikia redio ya Kenya ikitangaza "...Msifikiri kwamba Mzungu anatupenda sisi watu weusi"Thibitisha ukirejelea hadithi ya Damu Nyeusi.

**<u>SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI</u>**
8. Taja sifa za tanzu zifuatazo za fasihi simulizi
i) Ngomezi (al.5)
ii) miviga (al. 5)
b) Elezahasaratanozinazohusishwanamivigakatikajamiiyasasa. (al. 10)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

**set11**
**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

---

**MASWALI**

1. Jopo linaloshughulikia undanganyifu katika mithani ya Kitaifa (KCSE) limekuchagua wewe kama mwanajopo kati ya wanajopo watano. Mmetakiwa kuchunguza kinachosababisha undanganyifu, madhara ya undanganyifu na jinsi ya kukabiliana na undanganyigu huo. Andika ripoti yenu.

2. Tatizo La kigaidi ni changamoto kubwa sana katika usalama na maendeleo ya kiuchumi hapa nchini. Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu sidhani kapoa.

4. Andika kisa kitakachoishia kwa:
   ........................ niliyakumbuka maneno aliyotwambia mwalimu wetu shuleni siku moja. Nilijilaumu si haba na machozi yakanidondoka pukupuku.

**Set11**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

---

**1. UFAHAMU**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo uliwenguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malighafi inayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji viwanda vinavyoimarika ni vile vidogo. Hivi ni viwanda ambavyo huhusisha amali za mikono. Kuimarika kwa viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu sana kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa na bidhaa za viwanda . Katika msingi huu viwanda vikubwa vitawiwa ugumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vidogo pia vinao uwezo wa kuwaajiri wafanyikazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine. Uajiri huu wa wafanyikazi wengi ni muhimu katika maeneo mengi ambako tatizo la ajira ni mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasmia (yenye viwanda vingi) mataifa mengi yanayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo vidogo hakuhitaji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Sambamba na suala hili ni kuwa ni rahisi kujarisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo. Ikiwa mzalishaji yeyote atazalisha bidhaa mpya kwa mapanu, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana

for free past papers visit www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hiyo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa yenyewe. Majaribio mazuri huwa ni kwa kiwango kidogo.

Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikisha kuwa nafasi za ajira zimezambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huo wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa kiununuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo. Upanuzi na ueneaji wa viwanda vidogo vidogo ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa msingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

**Maswali**

a) Kwa nini viwanda ni muhimu? (alama 2)
b) Ni nini kiini cha matatizo ya uuzaji wa bidhaa katika nchi zinazoendelea? (alama 2)
c) Eleza faida zinazotokana na kuwepo kwa viwanda vidogo vidogo. (alama 4)
d) Usambazaji wa viwanda katika maeneo ya mashambani una faida gani? (alama 4)
e) Fafanua maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu. (alama 3)
   i) Kujasurisha
   ii) Amali
   iii) Utashi
   iv)

**2. MUHTASARI**

**Soma kifungu kifuatacho cha habari kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Watu wengi, wanaamini kwamba kufundisha watoto nyimbo shuleni ni kupoteza wakati unaofaa kwa masomo ya maana. Lakini muziki nyumbani na shuleni una manufaa mengi.

Muziki ni kitulizo kikubwa sana cha moyo wa binadamu. Muziki una njia ya kipekee ya kuwasiliana. Baadhi ya ujumbe hauwezi kupitishwa kwa njia nyingine ila kwa muziki.

Muziki umetajwa kumsaidia mtoto kwa mambo yafuatayo:

Kuendeza hisia nzuri, za kuburudisha na kuzuzua. Muziki humsaidia mtoto kuweza kukabiliana na tajriba mbaya nazo. Unampa fursa ya kutoa moyoni simanzi na dhiki yake na hivyo kumrejeshea raha tena. Liwazo la muziki ni dhahiri wakati mtoto anapolala pindi anapoimbiwa bembelezi.

Inaaminika pia kwamba muziki unakomaza akili ya mtoto na ni nyenzo muhimu sana katika hafla yake ya kujifanya mambo, hasa kwenye miaka yake ya mapema. Muziki huhitaji umakinifu ili kutambua miondoko na maneno halisi ya wimbo huo na mambo haya humfanya mtoto kuhamisha umakini huu kwenye masomo mengine darasani. Inaaminika pia kwamba kupitia kwa muziki mtoto anaweza kujifunza mbinu ya kukumbuka mambo anayofunzwa masomoni.

Watoto ambao hujifunza muziki mara kwa mara hujipatia mbinu za werevu shuleni haswa kwenye somo la hesabu na werevu wa mambo mengine kwa jumla. Utafiti umeonyesha kwamba watu

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

wazima ambao walijifunza muziki kabla wafikishe umri wa miaka 12 huwa na utumizi mzuri wa maneno magumu na msamiati kuliko wale ambao hawakujifunza kuimba.

Muziki pia husaidia watoto walio na kasoro za kuzungumza au walio na ulimi mzito wa kuzungumza.

Watoto au watu wazima walio na shida ya kigugumizi huweza kujieleza kwa ufasaha kwa kupitia muziki na jambo hili huboresha kujiamini kwao kwa kibinafsi. Watoto kama hao huweza kujifunza na kuelewa mila na tamaduni zao.

**MASWALI**

a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi, fupisha aya ya kwanza hadi ya tatu. (maneno 40 – 45) (alama 7)

MATAYARISHO

NAKALA SAFI

b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika aya ya nne na ya tano. (Maneno 45 – 50) (alama 5)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

MATAYARISHO

JIBU

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Andika sifa mbili mbili bainifu za sauti. (alama 2)
   i) /e/
   ii) /n/

b) Eleza tofauti ya kisarufi ya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
   i) Hiki ni kitabu cha mwalimu
   ii) Hiki ni cha mwalimu

c) Ainisha viambishi na mzizi katika kitenzi (alama 3)

d) Hawakunichokoza

e) Bainisha aina za vishazi katika sentensi hii (alama 2)
   Watoto walioachwa mayatima wamesaidiwa

f) Andika kwa ukubwa na udogo (alama 4)
   Sahani zote zimepelekwa nyumbani
   i) Ukubwa
   ii) Udogo.

g) Andika sentensi yakinishi kutokana na sentensi ifuatayo. (alama 2)
   Utawala mkubwa wa meya haukuzuilika.

h) Andika katika usemi wa taarifa
   "Nitawatuza watahiniwa wote watakaopita mtihani mwaka huu". Mwalimu aliwaahidi wazazi. (alama 3)

i) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo (alama 3)
   Juma alimchinjia mamake mbuzi mzuri kwa kisu.

j) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. (alama 2)
   Wanafunzi waliandikiana barua.

k) Ainisha vielezi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
   (i) Jaribu kujitahidi kisabuni usianguke mtihani.
   (ii) Wachezaji wote wameingia uwanjani..

k) Eleza matumizi mawili ya kistari kifupi. (alama 2)

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. (alama 4)

Ouma alianguka mtihani ila Kamau alifuzu vizuri.

m) Eleza matumizi ya "na" katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Wageni na wenyeji walikimbiliana.

n) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Walimu hao walifanya kazi yao kwa bidii.

o) Unda nomino mbili mbili kutokana na vitenzi vifuatavyo. (alama 2)
i) Jaribu
ii) Chuma

p) Kamilisha jedwali (alama 2)

| Kufanya | Kufanyiwa | Kufanyisha |
|---|---|---|
| La | | |
| Fa | | |

p) Fafanua aina ya hali iliyotumika katika sentensi hii. (alama 1
Wanasiasa wengi hulalamika kila mara.

4. **ISIMU JAMII**

a) Taja mambo manne yanayopelekea kufifia/kufa kwa lugha, (alama 4)

b) Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo

................napinga hoja iliyotolewa na waziri wa Finance ya kupiga marufuku matumizi ya plastic bags. Baada ya kumsikiza kwa makini, napenda kumkosoa kwa kudhihirisha kuwa.................. kulingana na kifungu nambari ..................

i) Bainisha sajili ya mazungumzo hayo. (alama 2)

ii) Huku ukitoa mifano mwafaka, eleza sifa nne za sajili hii kwa mujibu wa kifungu hiki.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

# Set11

**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

**Tamthilia; Mstahiki Meya**
**Timothy M. Arege**
**Swali La Lazima**

1. Au unafikiri pakawa na fursa nyingine hii leo ya kuchagua viongozi matokeo yatakuwa tofauti sana?..................Ukipanda huwezi kuvuna kunazi.

a) Eleza muktadha wa maneno haya? (alama 4)
b) Mzungumzaji na mzungumziwa wanafanana. Thibitisha. (alama 8)
c) Taja mbinu za kifasihi zinazojitokeza katika muktadha huu. (alama 4)
d) Eleza maovu yoyote manne yanayokumba wanacheneo. (alama 4)

**SEHEMU B: RIWAYA**
**Kidagaa kimemwozea**
**Ken Walibora**

Jibu swali la 2 au 3

2. Angewezaje kumwambia kwamba mifugo wake walikuwa katika ukalifu tangu Amani kutiwa mbaroni?"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili? (alama 4)

b) Mzungumziwa hakuwa na utu. Fafanua. (alama 8)

c) Toa mifano ya maudhui ya ukatili katika Riwaya ya kidagaa kimemwezea inayofaa. (alama 8)

3. Riwaya ya kidagaa kimemwozea inaonyesha jitihada za vijana kujenga jamii mpya. Thibitisha kwa kutoa mifano. (alama 20)

3. **SEHEMU C: USHAIRI**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:***

Hakika siku ya leo, ni siku ya majivuno
Basi pasiwe na choyo, na **usonono**
Tulekezane yaliyo, unawiri Muungano.

Tuzisafisheni nyoyo, pasiwe na miguguno
Yaongoke tutakayo, kusiwe na mabishano
Mbegu hii tupandayo, ilete mema mavuno.

Tufungulie upeo, Mola usiye mfano
Pa kitasa na komeo, tupite bila kinzano
Tupitishe njia hiyo, pasina masongamano
Twakuomba uumbao, mkono **vyanda** vitano
Tushikane hii leo, tuwe moja tangamano
Tupendane kwa pumbao, hali na maridhiano

Aliye ana machukiyo, adui wa Muungano
Naazibe masikiyo, asisikie maneno
Kisha awe kibogoyo, asiwe na moja jino.

Ya Ilahi ujalie, juu wetu Muungano
Nuru yake izagae, na nguvu za mapigano
Hasidi mpe hakie, mateso yaso mfano

Watamati komeleo, kuimba kwangu hukuno
Nataka maendeleo, yasiyo na malumbano
Daima tuwe ni ngao, palipo **msagurano**

4. (i) Lipe shairi hili anwani yake. (alama 2)
(ii) Liweke shairi hili katika bahari mbili ukitumia: (alama 2)
Idadi ya
(i) Mishororo
(ii) Vina
(iii) Onyesha muundo wa shairi hili. (alama 5)
(iv) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 3)
(v) Toa mifano ya idhini ya kishairi iliyotumika katika shairi hili. (alama 6)
(vi) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 2)
(i) Usonono –
(ii) Msagurano –

**SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI Jibu swali la 5 au 6**

for freepast papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

5. Eleza maana ya: (alama 4)

i)ulumbi

ii)soga

b) Eleza umuhimu wa soga katika jamii yetu. (alama 8)

c) Fafanua sifa bainifu za mlumbi (alama 8)

i)

a) Maghani ni nini? (alama 2)

b) Eleza aina zifuatazo za maghani? (alama 8)

i) Tondozi

ii) Sifa

iii) Tendi

iv) Rara

c) Fafanua sifa za maghani. (alama 6)

d) Eleza majukumu ya maghani. (alama 4)

6. **<u>SEHEMU E: HADITHI FUPI</u>**

**<u>DAMU NYEUSI NA HADITHI ZINGINEZO</u>**

**<u>KEN WALIBORA NA SAID A. MOHAMED)</u>**

(i) Mwana wa Darubini (Kristina Mwende Mbai)

"Ulijuaje alikuwa anaangalia kwetu?

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b. Hadithi hii inaonyesha matatizo ya kijamii. Fafanua. (alama 8)

c. Eleza yaliyotokea baada ya mazungumzo haya. (alama 8)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

## Set12

**102/1**

**KISWAHILI**

**Karatasi ya 1**

**INSHA**

---

1. Umeteuliwa kama katibu wa kamati iliyochunguza kuzorota kwa elimu katika wilaya yako. Andika ripoti kuhusu matokeo ya uchunguzi huo.

2. Uvumbuzi wa tarakilishi una athari kubwa katika maisha ya binadamu. Jadili.

3. Fahali wawili wapiganapo nyasi ndizo ziumiazo.

4. Andika kisa kitakachoanza kwa;

    Nilikaa pale kwa mseto wa hisia, nisijue kama nilifurahishwa ama nilihuzunishwa na kisa hicho......

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

**Set12**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

---

**UFAHAMU** (alama 15)

1. **Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Nimekaa kutafakari kwa kipindi kirefu, juu ya mabilioni ya pesa ambayo yametengwa na serikali ili kudhamini miradi ya maendeleo ya wanawake. Kina mama au wanawake wengi wanakiri na kusema kwamba fedha hizo zimewezesha kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji kutoka kwa waume zao. Kwani kila mmoja anamheshimu mwenzake kwa sababu ya kipato alicho nacho. Wengi wameweza kuanza biashara ndogondogo ambazo huwaletea angaa kipato kidogo.

Ukweli ni kwamba fedha hizi zimesaidia kuwatoa wanawake wengi katika unyanyasaji, kwani wengi wanaweza kuanzisha kazi za ujasiriamali na hata kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kutokana na mafanikio haya, wabunge waliopitisha hoja bungeni za kuanzisha mpango huu wa kuwakwamua wanawake kimaendeleo wanafaa kupongezwa. Mafanikio haya yamewafanya akina mama kujikimu kimaisha na hivyo kutowatengemea wanaume katika kila jambo.

Ukitaka kujua ukweli kuhusu hili, nenda kwenye masoko utaona akina mama jinsi wanavyyohangaika na biashara zao. Kwa hivyo, ujasiriamali huendelezwa na akina mama zaidi na hivyo wanapaswa kuwezeshwa kwa hali na mali.

Akina mama pia wanafaa kupongezwa kwani wameamua kujitosa kukopa fedha kutoka kwenye taasisi mbalimbali na fedha. Fedha hizo kwa kiwango kikubwa zimewainua kutoka katika ufukara uliokithiri hadi katika maisha ya heshima. Wale ambao hawajaribu kuchukua mkopo ni muhimu wafanye hivyo ili wajikimu kimaisha.

Maisha ya sasa ni magumu, hivyo yanahitaji kusaidiana kwa kila hali na mali. Wanaume kwa wanawake ni vyema wachange bia ili wazumbue riziki. Ushirikiano utarahisisha maisha yao. hata hivyo, sio tu akina mama hao wameondokewa na unyanyasaji waliokuwa wakiupata ndani ya nyumba zao, toka kwa akina baba, bali hata masualama ya mrundikano wa kesi za kugombea ardhi kwa akina mama, zimepungua. Sababu ni kwamba akina mama wengi wameweza kujitafutia ardhi wenyewe kwa fedha walizonazo.

Ukweli ni kwamba hali imebadilika kinyume na hapo awali, ambapo majumba ya kifahari na mashangingi yalikuwa hifadhi ya wanaume, siku hizi wanawake wanamiliki hayo yote.

**Maswali.**

1. Taja dhamira **mbili** za makala haya. (alama 2)
2. Eleza ni kwa nini msimulizi anawapongeza wabunge. (alama 2)
3. Wanaume walikuwa wakirudisha nyuma maendeleo nchini kivipi? (alama 2)
4. Sera za serikali zimesaidia wanawake kivipi? (alama 3)

For free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

5. Eleza kwa nini baadhi ya wanawake wanaishi katika lindi la umaskini kulingana na makala haya. (alama 3)
6. Eleza maana ya msamiati na mafungu yafuatayo kama yalivyotumika katika makala haya(alama 3)
   i) kutafakari.

   ii) kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji.

   iii) Riziki.

**UFUPISHO** (alama 10)

2. **Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kulingana na maagizo**.

Imesemwa na kurudiwa tena kwamba, iwapo tuna maono ya kujiondoa katika umaskini wa kupindukia, ni lazima tukipe kilimo umuhimu. Zaidi ya wakenya milioni kumi wamo katika hatari ya kufa njaa katika maeneo mbali mbali kwa sasa kufuaia uhaba wa chakula nchini.

Kiini kikubwa cha njaa hiyo ni mapuuza ya muda mrefu katika sekta ya kilimo. Imesahaulika kuwa karibu asilimia sabini na tano ya wakenya wanategemea kilimo kwa chakula na mapato ya kifedha kila siku. Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa mwananchi na pia kuletea serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mauzo ya mazao katika mataifa ya nje.

Wataalamu wa maswala ya zaraa wanaeleza kuwa pato la nchi linalotokana na kilimo huangamiza njaa mara nne zaidi ya mapato yanayotokana na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Hiyo ni kwa sababu shughuli za kilimo hulenga kuzalisha vyakula moja kwa moja.

Imebainika kuwa, katika mataifa mengi yanayostawi, asilimia sabini na tano ya wananchi huishi katika maeneo ya mashambani na idai hii hutegemea kilimo kujimudu kimaisha ilhali hapa Kenya ni asilimia nne pekee ya bajeti inayowekezwa katika kilimo. Kwa wakati huo, ushuru unaotozwa bidhaa za kilimo katika maeneo haya umebainika kuwa mkubwa. Hii imepelekea uwekezaji katika kilimo kupungua na hivyo kuchangia kukithiri kwa baa la njaa.

Wakati umewadia kwa serikali za Afrika na wapangaji wa masuala ya uchumi kuweka juhudi maradufu katika kushabikia kilimo ili kumaliza njaa na umaskini. Kuna haja ya kuwajulisha, kuwahimiza na kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo kuhusu mihimili ya zaraa kama vile uzalishaji wa matunda na mboga ufugaji wa ndege, samaki na ng'ombe mbali na kuweka mikakati ya kuanzisha nafasi za kazi katika sekta ya kilimo.

Serikali itafikia lengo hili iwapo itaanza kufadhili kilimo, kupunguza gharama za pembejeo za kilimo, kuweka sera zinazodhibiti uuzaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa na kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo. Bila hilo hatutakuwa na lingine bali kukimbilia mataifa yaliyostawi kuomba misaada ili kuwanusuru raia wetu kutokana na ghadhabu ya njaa.

**Maswali.**

a) Fupisha aya mbili za mwanzo kwa maneno 50-55. (alama 8)
   Matayarisho.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Jibu

b) Bila kubadili maana, fupisha aya mbili za mwisho. (maneno 55 - 60.) (alama 6)

Matayarisho.

Jibu

3. **Matumizi ya lugha.** (alama 40)

a) Toa sifa bainifu za sauti /h/ (alama 3)

b) Andika sentensi ifuatayo ilete dhana tatu tofauti. (alama 3)
Mwaura amekuja.

c) Nyambua kitenzi Lewa katika kauli ya kutenduka kisha utungie sentensi. (alama 2)

d) Yakinisha sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (alama 2)
Sitakununulia nguo wala kukutembeza mjini usipomaliza mkate huo.

e) Andika katika umoja. (alama 2)
Nyaraka zetu ziliwasilishwa rasmi kwenu na madiwani wa vyama tawala.

f) Andika sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo. (alama 2)
Nimewaleta askari kituoni ili wawalinde wananchi wote wanaosumbuliwa na majambazi.
(Anza: Wananchi ...)

g) Iandike sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 3)
"Leo nitachimba mtaro uelekeze maji shambani mwangu." mkulima alisema.

h) Tumia neno 'hadi' kama kihusishi cha; (alama 2)
i) Wakati
ii) Mahali.

g) Bainisha matumizi ya viambishi vilivyopigiwa mstari. (alama 2)
Mwalimu ana<u>ku</u>ita ofisi<u>ni</u> <u>u</u>mweleze uli<u>ko</u>weka <u>ki</u>jitabu chake.

i) Bainisha kiima, shamirisho na chagizo katika sentensi hii. (alama 3)
Mwanafunzi aliandika insha vizuri.

j) Kanusha bila kutumia 'amba' (alama 2)

Nitavaa viatu ambavyo ni safi.

k) Kwa kutolea mifano mitatu, eleza miundo mitatu ya nomino katika ngeli ya A-WA. (alama 3)

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale. (alama 4)
Watoto wanacheza vizuri ilhali wazazi wakorofi wanawabeza vikali sana.

m) Ainisha mofimu katika sentensi hii. (alama 3)
Aliyemletea.

n) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. (alama 2)

o) Wapatie nafasi wabunge wale.
Unda kivumishi kutokana na kitenzi <u>dhulumu</u> na utungie sentensi. (alama 2)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

4. **ISIMU JAMII.** (alama 10)

a) Lugha ya Kiswahili inakabiliwa na matatizo mengi sana. Taja matano na kuyaeleza. (alama 5)

b) Fafanua mikakati mitano inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya. (alama 5)

## set12

**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

**SEHEMU A: USHAIRI.**

1. **Swali la lazima.**

**GANGA SHINA.**

1. Maradhi na taathira ya tego na ulemavu
Zimeshajiri ishara za mti kuwa mbovu
Vitawi kuporapora mti wazidi ukavu
Ganga shina la uhai tanzuze hazigangiki

2. Karibu si masihara kwataka kutuma nguvu
Na magambo kuyapara hata viache koru
Haiji thama nusura ukichelea mabivu
Ganga shina la uhai tanzuze hazigangiki

3. Makongwe yanayokera yakate kwa maumivu
Na mizizi ya safura iliyo mikandamivu
Usiwe nayo subira katika utimilivu
Ganga shina la uhai tanzuze hazigangiki

4. Rasharasha sio bora dawa iwe rovurovu
Imwailie imara hadi isombe kitovu
Uchome moto sangara mti uwe muangaru
Ganga shina la uhai tanzuze hazigangiki

5. Fyekafyeka miparura mimea mitatagivu
Inayonyonya ujira wa miti mishughulivu
Nasaha zangu dharura kesho utakula mbivu
Ganga shina la uhai tanzuze hazigangiki

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Maswali.**

a) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)

b) Mwandishi ametumia jazanda katika kueleza jambo fulani. Taja jazanda hiyo na ueleze maana yake. (alama 4)

c) Mwandishi anamaanisha nini anaposema "Kutibu si masihara kwataka kutuma nguvu? (alama 2)

d) Mwandishi ametumia inkisari. Taja mifano miwili na uandike inavyotakikana. (alama 2)
e) Eleza maana ya kibwagizo cha shairi hili. (alama 2)
f) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumiwa katika shairi hii; (alama 5)
   i) Kupora pora
   ii) Isombe
   iii) Sangara
   iv) Miparura
   v) mishughulivu.

**SEHEMU B: RIWAYA**
**K. Walibora: Kidagaa Kimemwozea.**
**Jibu swali la 2 au la 3.**

2. Dhuluma ni jambo la kawaida katika jumuiya ya Kidagaa Kimemwozea. Jadili. (alama 20)

3. "Huyu mwendawazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi? Anafikiri sherehe hizi ni za watu wenye kichaa kama yeye?"

   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

   (b) Eleza tamathali mbili zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)

   (c) Thititisha kuwa anayerejelewa ni mwendawazimu na vile vile si mwendawazimu. (alama 12)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**SEHEMU C: TAMTHILIA**
**Jibu swali la 4 au la 5.**

4. "Tuendelee kusonga mbele hatua kwa hatua. Bwana fedha na kazi ...."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

   (b) Taja sifa nne za anayesemezwa. (alama 4)

   (c) Baraza la Cheneo limeendelea kuwepo mamlakani kwa mbinu kadha . Jadili. (alama 12)

5. Hatua tuchukuazo maishani mwetu zaweza kutuathiri na kuathiri nchi pakubwa. Thibitisha kauli hii ukirejelea mhusika Meya Sosi. (alama 20)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**
**K. Walibora na S. A Mohamed: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.**
**Jibu swali la 6 au la 7.**

6. "Shangazi wakumbuke watoto. Waonee huruma!"
   (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
   (b) Fafanua mbinu ya kisanaa inayojitokeza katika kauli hii. (alama 2)
   (c) Jadili jinsi maudhui ya ukatili yameendelezwa na wahusika wengine katika hadithi (alama 6)
   (d) Eleza sifa nne za anayerejelewa katika dondoo. (alama 8)
7. Mwimba wa kujichoma hauambiwi pole.
   Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi zozote kumi. (alama 20)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI.**

8. (a) Maghani ni nini? (alama 2)

   (b) Eleza fani zifuatazo za maghani. (alama 4)

   i) Vivugo.

   ii) Tondozi

   iii) Pembezi

   iv) Rara

   (c) Eleza maana ya neno ULUMBI. (alama 1)

   (d) Bainisha sifa za mlumbi. (alama 6)

   (e) Eleza umuhimu wa ulumbi. (alama 3)

# Set13

**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

---

1. **Insha ya lazima**
   Andika dayolojia kati ya katibu wa usalama wa ndani na waandishi wa habari kuhusu jinsi ya kuzuia uhalifu nchini

2. Sheria zinazombagua mwanaume na kumpendelea mwanamke zinafaa kutupiliwa mbali. Fafanua

3. Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe.

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno haya

5. Lo, yaliyotendeka katika makazi ya jirani yetu usiku huo yalikuwa ya kutisha sana. Kumbe watu wamegeuka hayawani! Hayawani ........................................

For free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Set13**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

---

1. **UFAHAMU**

**Shule yangu ya upili**

Majio yangu katika shule hii ya upili hayakutokea kwa bahati nasibu bali kwa mipango kabambe niliyoianza tangu nikiwa shule ya vichekechea. Nikiwa sitetereki hata kwa wazazi wangu waliponisihi nijiunge na shule nyingine za karibu nikawa sisikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Nikawa na ragba ya mkanja nikingoja siku ya kujiunga na shule yenyewe. Kweli majuto ni mjukuu na huja kinyume.

Nilizaliwa katika aila yenye nafasi iliyotopea na kubobea katika ukwasi uliodhihirika kutokana na mitaa tulikoselelea kwa muda kabla ya baba kuamua kununua nyumba yake mwenyewe huko upande wa Karen hivyo tukagura kutoka Runda. Wakati wa likizo tukawa tunaruka hadi pwani ambako mama yangu alikuwa amemiliki jumba lililokuwa katika ufuo wa bahari lililojengwa katika kipande kisichopungua ekari tatu alilotunukiwa wakati wa nikahi yao na wakwe wa baba yangu.

Wavyele wangu wakawa wanaendesha magari meusi ya kifahari ingawa sikuwahi kumwona mama akichangamka kuendesha magari yake ya maana, kila macheo ya siku za kazi gari lililoendeshwa na dereva ambaye alimstahi mama hadi akawa anamfungulia mlango wa gari na kuufunga baada ya mama kujitoma katika tumbo la gari lilimjia na kumrejesha kwa wakati. Nikajiunga na shule ya msingi ya kibinafsi ambako nilishughulikiwa kama kikembe. Wengi wa wale tuliosoma nao walikuwa wa tabaka langu na walikuwa wametoka katika kila sehemu nchini Kenya.

Hayawi hayawi huwa na siku ya kuripoti ikafika. Alfajiri, dereva mmoja akatumwa kwenda hadi Kisumu ili atulaki na kutusafirisha kutoka uwanja wa ndege hadi shule ya upili ambayo ilikuwa yangu ya rohoni. Nasi tukaelekea hadi uwanja wa ndege ili turuke hadi Kisumu. Safari yetu kutoka kitongoji cha kifahari hadi Airport ilikuwa njema, safari yetu tulipoabiri ndege ilikuwa bila bughudha, safari yetu kutoka Kisumu mjini haikuwa na kasoro na tulienda kulingana na mpango. Safari yetu ilikuwa mufti hadi tulipofika katika lango la shule ya kitaifa!

Tulipotia ozi tu!!....jamani......jamani nikafa moyo. Labda mama aliweza kubaini mabadiliko ya hisia zangu, nilitamauka, nikawa mchege na kusema kweli niliyoyaona sikuamini. Mvua iliyokuwa imepasua hapo awali ilikuwa imeacha vitua vya maji kwenye vijia vya kutembea vilivyochakaa na kubomoka bila yeyote kujali kuvikarabati. Majengo yalikuwa makongwe yaliyojengwa miaka mia moja iliyopita na yalistahili kuitwa makafadhi badala ya pahali pa kumkaribishia mwanafunzi aliyepita kwa alama mia nne na thelathini na tano. Asiye na wake ana Mungu, nikapiga moyo konde lazima nisajiliwe katika shule ya ndoto langu. Ningewezaje kughairi wazo langu baada ya siku hizo zote za maandalizi tena mbele ya wanuna walionіona kama kielelezo chao tangu walipozaliwa. Nikasajiliwa!

Sikujua, hakika sikujua, sikujua shule ya upili ya kitaifa yaweza kuwa hivi. Kweli mwanafunzi aweza kukosa viatu na hata kushindwa kununua rangi ya kupaka viatu hivyo iwapo amenunuliwa na wahisani? Nilimlaumu nina maana hakunieleza kuwa mtu anaweza kula chakula ambacho mbwa wetu hawezi hata kukiangalia. Nilipoingia katika ukumbi wa chakula nilihisi kitefutefu nusura

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

nichafukwe na moyo, makapi ya mboga na uchafu usioelezeka ulinikumba, kisha nikapewa kisahani cha plastiki na kupakuliwa kipande cha ugali ambacho bado kilikuwa na unga na kuachiwa hiari ya kukila au kukitupa. Wenzangu wakawa wanakirambatia chakula kwa kasi huku mmoja wao alipoona jinsi nilivyokiangalia changu akanihisi nimpe chote na kukimaliza fyu. Wote walikuwa na furaha kemkem na kuajabia utukufu wa shule iliyotukuka ya kitaifa ila mimi.

Baada ya mlo 'rojo rojo', tukaelekea darasani nilikopigwa na mghuma mkubwa. Tulikuwa wanafunzi hamsini na watano katika darasa moja tu! Mwalimu mmoja akaja na kutukaribisha shuleni kisha akatuarifu kuwa atakuwa mwalimu wa darasa letu. Nilipomsikia akinena nusura niishiwe na stahamala, kimombo chake kilinishangaza, hasa matamshi yake yalipungukiwa na kudhirisha athari za lugha ya asili. Nilihisi kana kwamba ningemrekebisha lakini sikudhubutu.

Tukafululiza hadi bweni na nikajilaza kitandani chembamba huku mwingine nisiyemjua lakini asiyejua kuwa kuna nguo maalum za kulala akalala uchi katika ghorofa ya juu ya kitanda chetu. Mgeni njoo mwenyeji apone maana baada ya muda wadudu ambao sikuwahi kuwaona aushini mwangu wakanza kunishambulia. Nikaamka baada ya kumnasa mmoja wa wadudu hawa na kuuliza mmoja wa wenzangu ni wepi wadudu hawa na kwa kutojali hata kidogo, akanieleza kuwa hawana neno bali ni kunguni tu, sikujua na kwa kweli mama hakuniambia kuwa kuna wadudu wanaotafuna mtu na hunuka fye! Sikulala kwa hofu huku wenzangu wakiforota kwa njia ya kunighasi. Sikuwahi kudhani kuwa watu wengi wanaweza kulala chumba kimoja huku changu kikiwa na hamamu na vifaa vyote muhimu kikibaki bila mtu!

Tulisomeshwa na walimu wasiojali kana kwamba tunaelewa au la. Hawakushughulika iwapo tulifanya kazi za ziada au la, ndio, hakujali chochote. Kilichonishangaza ni kuwa wanafunzi waliojiunga nasi kutoka shule za umma wenye alama duni waliwapenda na kuelewa haraka walichosomeshwa na hawakujali matamshi yao, labda hawakuyatambua.

Hatimaye tukafanya mtihani wa mwisho wa muhula wa kwanza. Nilishangaa ghaya iliponibainikia kuwa aliyetuongoza alikuwa ghulamu mmoja mshamba niliyempuuza tu mvulana kutoka kijijini ambacho singetambua katika ramani ya nchi ambaye hata vitu vya kimsingi vilimpiga chenga. Nikafanya uchunguzi nikatambua mwenzangu alikuwa na alama mia mbili hamsini na tatu akitoka katika darasa la nane, nilifanikiwa kuwa nambari mia mbili hamsini na tatu kwa jumla ya wanafunzi mia tatu!

for free pastpapers visit www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Tulipofunga kwa likizo ya Pasaka nikaamua kuchukua hatua nyingine sitawahi kuhama kutoka shule hii ya upili wala kuwa zaidi ya nambari kumi!

**<u>Maswali</u>**

a) Thibitisha kauli kuwa msimulizi ana msimamo dhabiti (alama 2)

b) Tofautisha jinsi mwandishi alivyofunzwa katika shule ya kibinafsi na shule ya upili (alama 3)

c) Taja mambo matatu yanayotuonyesha kuwa msimulizi alilelewa katika aila ya kikabaila kulingana na aya ya pili. (alama 3)

d) Andika masuala matatu yaliyomshangaza katika shule ya upili (alama 3)

e) Andika tamathali mbili zilizotumika katika kifungu. (alama 2)

f) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu. (alama 3)

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

i) alimstahi
ii) kughairi
iii) kunighasi

**MUHTASARI**

Tulipigwa na butwaa kwa kupokea habari kuhusu mauaji ya wasafiri 28 waliouwawa kikatili huko Mandera na kabla kuwasidikiza makaburini wengine waliokuwa 40 wakijitafutia riziki katika chimbo la mawe kuko huko, wakaangamizwa. Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelezwa kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa. Inakera mno kwa vitendo vya kigaidi. Inagadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba magaidi hawa wamelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani, damu ya mwananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini. Vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauaji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Iwapo mbunge anayelindwa na askari wawili atawauwa, je wananchi wa kawaida watakosa kumuua? Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao imedumishwa. Polisi nao wanashambuliwa huko Kapendo na kumiminiwa marisasi wasiweze kujikinga tukabaki kuwazika licha ya umri wao mdogo ili kukabiliana na tatizo hili, polisi wakaamua kusaka wahalifu. Lakini cha kusikitisha kuwa mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa hii ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kinachoendelea, inawaongezea Wakenya mateso. Hali hii inawaacha Wakenya kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hii ya misako imeishia kunasa raia wengi wasio na makosa. Wanaponaswa, hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, mbinu hii yaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majajusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia. Ni ajabu kuwa sisi tunaelekeza kidole cha lawama kwa serikali ilhali wahalifu hawa tunaishi nao katika mitaa tunakoishi, viongozi wapinzani wasipinge mikakati yoyote ya serikali kama vile mpango wa nyumba kumi kisa na maana si wazo lao. Iwapo hawapendezwi na mpango kama huo waibuke na mbinu badala tuzijaribu. Suala la 'serikali ingilie kati' hata bwana mlevi anapochapwa na mkewe lisukumwe katika kaburi la sahau.

**Maswali**

a) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi?
Tumia maneno 80 (alama 7, 1 utiririko)
Matayarisho

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call:0720502479

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Nakala safi

b) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50, fupisha aya mbili za mwisho (alama 6, 1 utiririko)

Matayarisho

nakala safi

3. Matumizi ya lugha

a) Badilisha vitenzi hivi viwe katika hali ya kuamuru (alama 2)
   1) kuleta
   2) kuja

b) Tumia kiungo 'na' katika sentensi kuonyesha: (alama 2)
   1) Ufupisho wa nafsi ya kwanza umoja fulani
   2) kihusishi kuonyesha aliyetenda jambo fulani

c) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (alama 2)
   1) Mwalimu amesema ya kwamba watoto wengi wamekuwa wahuni.
   2) Ikiwa nitamwona mama sokoni, nitamweleza kila kitu

d) Ainisha viungo vya kisarufi katika sentensi hii (alama 3)
   Alani

e) Tumia kitenzi **'cha'** katika kauli ya kutendesha katika sentensi (alama 2)

f) Tumia kiambishi ngali katika sentesi kuonyesha hali ya kuendelea (alama 2)

g) Tofautisha kwa kueleza maana ya istilahi hizi: (alama 2)
   ghuna
   si ghuna

h) Changanua sentensi kwa njia ya matawi (alama 4)
   Yeye na mama yule si watu wazuri sana

i) Eleza sifa bainifu za sauti zifuatazo (alama 4)
   i) /l/
   ii) /ch/

j) Tumia kielezi cha namna kiigizi katika sentensi (alama 2)

k) Andika sentensi hii upya katika **usemi halisi** (alama 2)
   Mwanafunzi alimsihi mwalimu asimwadhibu wakati huo

l) Onyesha chagizo katika sentensi hii (alama 2)
   Mtoto alikula kwa utaratibu jana jioni

m) Tambua na uainishe shamirisho katika sentensi hii
   (alama 3) Hamu amemwandikia mwalimu riwaya kwa kalamu

n) Unda vitenzi kutoka kwa maneno haya kisha uyatumie katika sentensi yakiwa katika hali hiyo ya kitenzi (alama 2)
   i) Marashi
   ii) bora

o) Tofautisha kati ya vivumishi hivi kwa kueleza maana ya kila kimojawapo(alama 2)
   i) -ingine
   ii) -ingineo

p) Sahihisha makosa katika sentensi hii (alama 2)
   Mtoto mgani mwenye kupiga kelele darasani

q) Tumia maneno haya katika sentensi ili kuyatofautisha (alama 2)

shoka
choka
shoga

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Isimu jamii**

Nani kuku.....? Sosi poa leo ...... Mate ndo! ndo! ndo!. Ukimanga hii hutaona daktari kwa miaka kumi...... Ng'ombe je? nani? ......nani!... Ni wewe....... poa basi naja............

a) Ni sajili gani inayorejelewa hapo juu? (alama 2)

b) Andika sifa za sajili hii ukitoa mifano ndani na nje ya muktadha huu (alama 8)

## set13

**102/3**

**FASIHI**

**KARATASI YA TATU**

---

**SEHEMU A**

1. **Swali la lazima**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo**

1. Ningali kinda nishike, viungo vi teketeke,
Sinipe simi nizuke, na vichaka nivifyeke,
Dhibiti nivuvumke, usidiriki makekeke,
Pulika usikiuke, mpe mtoto hakiye,

2. Mungavunja haki yake, madhara milele kwake,
Wa kiume na wa kike, mpeni yaliyo yake,
Kwa makini mumshike, kadiri makamo yake,
Pulika msikiuke mpe watoto haki yake.

3. Kwanza ni watani wake, Uandae aridhike,
Atuze mtima wake, maudhi yasimshike,
Kuta nne zizunguke, na hofu imbanduke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake.

4. Pili ni chakula chake, 'jengeke siha yake,
Mpe titi alishike, anyonye asihinike,
Kuta nne zizunguke, na hofu imbanduke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake.

5. Mpe tiba 'sidhurike, ndwele asiathirike,
Fikira zimpanuke, atambue rika lake,
Penye daraja avuke, mvushe asighurike,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake.

6. Angakuwa chekecheke, apande shule avuke,
Mpe taaluma yake, adhibiti apanuke,
Ufundi na dhima zake, ayashike ajivike,

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

**7.** Jifanye kipenzi chake, mpende asihinike,
Amani ijae kwake, daima asikereke,
Vizito usimtwike, visivyo vipimo vyake,
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

**8.** Elimu chuo ashike, apanuke bongo lake,
Atende jukumu lake, ahudumie wenzake,
Ajue wajibu wake, atende asitepweke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

**9.** Hima kwa Muumba wake, muhimidi aongoke,
Roho yake isafike, ahera asisumbuke,
Neema imzunguke, maovu yamuepuke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

**Maswali**

a) Nafsi neni ametaja haki zinazomstahiki mtoto. Zitaje na uzifafanue (alama 4)
b) Eleza kwa kutoa mifano mbinu mbili zinazotumiwa na mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi
c) Bainisha umuhimu wa tamathali zozote mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili (alama 4)
d) Eleza ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)
e) Taja na ufafanue toni ya mshairi (alama 2)
f) Eleza maana ya misamiati ifuatayo (alama 2)
   i) Mtima
   ii) Asihinike
   iii) mbi
   iv) asighurike

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**SEHEMU B**
**TAMTHILIA**: ***Timothy Arege: Mstahiki Meya***
**Jibu swali la 2 au 3**

2. "Mtu huvuna alichopanda. Ukipanda pojo huweza kuvuna kunaziu"
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Thibitisha kuwa warejelewa walikuwa wamepanda pojo (alama 10)
   c) Eleza sifa za mnenewa (alama 6)
3. Tamthilia ya Mstahiki Meya inamulika na kupiga vita utawala dhalimu katika mataifa ya kiafrika. Jadili (alama 20)

**SEHEMU C**
**RIWAYA**: **Ken Walibora:** ***Kidagaa Kimemwozea***
**Jibu swali 4 au 5**

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

4. "Aliwaonea gere wanawake wengine katika eneo la Sokomoko waliovaa rinda moja..........."

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)

b) Eleza sifa na umuhimu wa anayemfanya mrejelewa kuwaonea wanawake wengine gere (alama 10)

c) Jadili maudhui matatu yanayodokezwa katika dondoo hili (alama 6)

5. "Mla naye huliwa zamu yake ifikapo."
Thibitisha kauli hii kwa kuirejelea riwaya ya kidagaa kimemwozea. (alama 20)

**SEHEMU D:**
**HADITHI FUPI: Ken Walibora : *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine***
***Jibu swali la 6 au 7***

6. Onyesha jinsi swala la ubaguzi linavyodhihirika katika hadithi zozote nne(alama 20)

7. "Hawakurudhisha macho tu, bali pia walicheza michezo ya ujana ama wakijua au kutojua kuwa ujana una tegemeo."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Dhihirisha namna 'Michezo ya ujana' ya wanaorejelewa ilivyosambaratisha tegemeo la ujana wao. (alama 8)

c) Jadili ukweli wa kauli kwamba, "Tamaa mbele mauti nyuma" ukirejelea hadithi ya "Tazamana na mauti" (alama 8)

**SEHEMU E**
**FASIHI SIMULIZI**

8. a) Eleza sifa nne za ushairi simulizi (alama 8)

b) Taja na uelezee aina tatu za magizo (alama 6)

c) Jadili mbinu nne za kimtindo za methali huku ukitoa mifano mwafaka (alama 4)

d) Eleza umuhimu wa hekaya katika jamii (alama 4)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Set14**
**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

---

**MASWALI**

1. **INSHA YA LAZIMA**
Wewe ni katibu wa kamati iliyoteuliwa na mkuu wa wilaya kujadili kuhusu madhara ya pombe haramu na mbinu za kuangamiza pombe hiyo wilayani. Andika ripoti ya kamati hiyo.

2. Unyanyasaji wa kijinsia umekithiri katika jamii yetu ya leo. Thibitisha.

3. Sikio la kufa halisikii dawa.

4. Andika insha itakayomalizikia na:
.................. Wazima moto waliwasili saa tatu baadaye. Uharibifu wa mali na maisha ulikuwa umeshatokea. Maajabu yaliyoje!

# MARANDA SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

---

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**
***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia.***

Nchi yetu imeraukia mawio ya machafuzi ya kisiasa baada ya shughuli za uchaguzi zilizogonga mwamba mkuu. Hili lilijiri baada ya Tume ya uchaguzi kukoka kuendeleza uchaguzi kwa njia inayostahili. Jambo hili lilizaa msukosuko wa kisiasa usiomithilishwa katika historia ya taifa letu.
Hivi sasa wakenya wanaishi kwenye kambi za watu wasio na makazi. Hiki ni kinaya kikuu kwani matukio haya yamezuka baada ya miongo minne ya uhuru. Vilio vya wakenya vimeshamiri na kupaaza sauti vikilalamikia kukosa makazi, lishe na ndoa kusambaratika. Ndoa zimevunjika baada ya 'wenyeji' kuwatimua 'wageni' na damu kumwagika.

Kenya imekuwa miongoni mwa mataifa yanayowapa faraja wakimbizi kutoka nchi jirani zinazokubwa na vita vya wenyewe. Vita katika Somalia vimesababishwa na koo mbali mbali zinazopigania uongozi hali ambayo imekwamisha shughuli zote za kiuchumi.

Hali ya sasa ya Kenya imechochewa na msururu wa sababu; ukabila na tamaa ya uongozi zilionekana wazi katika miundo ya vyama vikuu vya kisiasa na katika kampeni zao. Wakenya walipiga kura kwa misingi ya kikabila kila upande ukitazamia mtu wao kushinda uchaguzi huo.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Kwa upande mwingine, viongozi hao kutokana na tamaa ya uongozi walikuwa wameamua kushinda uchaguzi huo kwa vyovyote vile. Leo tunavuna matunda ya siasa za ukabila na tamaa ya mamlaka.

Maelfu ya Wakenya ni wakimbizi nchini na katika nchi jirani ya Uganda. Wakenya hao wanahitaji msaada wa chakula na mahitaji mengine ya kimsingi. Serikali na shirika la msalaba mwekundu zimefanya juhudi kuwasaidia wahasiriwa lakini kuna tetezi kwamba ubaguzi umejipenyeza katika ugawaji wa msaada huo.

Waliopewa jukumu la kugawa msaada huo ni sharti waelewe kuwa waathiriwa ni wakenya wenzao na hawafai kubaguliwa kwa misingi ya makabila yao.

Matukio kama haya hayastahili kutukia asilani katika taifa hili.

Twahitaji zao **aali** la viongozi wasiojitwika ubabe bali wawe watumishi wa wananchi wanastahili kutupilia mbali tamaa za kujilimbikizia mali na kung'ang'ania uongozi. Pia katiba inafaa irekebishwe. Wakenya wanastahili kuelimishwa kuhusu undugu na utaifa. Fauka ya haya masuala yanayohusiana na hatimiliki za ardhi yanafaa **kutadarukiwa kwa dhati.**

**Maswali**

a) Toa anwani mwafaka kwa makala haya. (alama 1)
b) Taja madhara **manne** ya ukabila. (alama 2)
c) Shughuli za ugawaji wa misaada zimekubwa na changamoto gani? (alama 2)
d) Eleza tofauti ya chanzo cha vita nchini Somalia na Kenya. (alama 2)
e) Mwandishi anatoa mapendekezo gani ya kutatua tatizo hili la ukabila. (alama 4)
f) Eleza kinaya cha maisha ya wakenya kwa sasa. (alama 2)
g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu cha ufahamu. (alama 2)
i) Mawio -
ii) Tandarakiwa kwa dhati

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

Ajira ya watoto ni tatizo sugu linalokumba ulimwengu wa sasa, hasa katika nchi zinazoendelea. Jambo la kusikitisha ni kwamba hivi ndivyo ilivyo katika nchi nyingi za ulimwengu huu. Kuna idadi kubwa ya watoto wanaoajiriwa katika nyanja mbalimbali za jamii. Zipo sababu nyingi zinazowasukuma watoto kutafuta ajira barani Africa kwa mfano, familia nyingi huishi maisha ya ufukara hivi kwamba hushindwa mahitaji muhimu hususan kwa watoto. Kupanda kwa gharama ya maisha kunazidisha viwango vya umaskini. Ukosefu wa lishe pia huwafanya waoto kutoroka nyumbani kutafuta ajira. Janga la ukimwi limesababisha kuwepo kwa idadi kubwa ya mayatima wanaoishi kutafuta ajira ili kuyakimu maisha. Ukimwi umezifanya familia nyingi pia kuwaondoa watoto shuleni ili waweze kuajiriwa kwa lengo la kusalisha pato la familia hizo. Watoto wengine hutoroka makwao kwa sababu ya maonevu. Maonevu haya ni kama vile kupigwa, kutukanwa kila wakati, kunyanyaswa kijinsia na kadhalika. Huko nje hutaabishwa kimwili na kiakili. Hufanyishwa kazi za sulubu zenye malipo duni au wasilipwe kabisa. Hili huwasononesha na kuathiri afya yao.

Wengine hujiingiza katika vitendo vya jinai pale wanapokosa ajira huchukua sheria mikononi mwao, wakaendeleza vitendo vya ukatili kama vile kuwahangaisha watu na kupora mali yao au hata kuwakaba roho. Aidha wengine hujikuta kwenye madanguro ambako huendesha biashara haramu.

Uundaji wa umoja wa Africa hivi majuzi ni hatua muhimu ya kushughulikia matatizo ya Afrika kama vile ajira ya watoto, kuzorota kwa miundo msingi, magonjwa, njaa, umaskini, ufisadi na ukabila. Katika kushughulikia haki za watoto nchi za Africa hazina budi kuzingatia masharti yaliyowekwa na umoja wa mataifa kuhusu haki za watoto. Nchi nyingi za Afrika ziliidhinisha mkataba wa masharti hayo, ikiwemo nchi ya Kenya. Nchi hizi basi lazima zishughulikie haki za watoto kupitia sheria za nchi. Watoto ni rasilmali muhimu na ndio tumaini la kuwepo kwa kizazi cha binadamu.

**Maswali**

a) Eleza mambo yote muhimu anayozungumzia mwandishi katika aya ya kwanza.
(maneno 45 - 50)
(al 6, 1 ya mtiririko

b) Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi, fupisha aya mbili za mwisho
(maneno 50 - 55)
(Alama 7, 1 ya mtiririko)

3. **MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Taja vikwamizo **viwili** ambavyo ni kosonanti hafifu (alama 2)

b) Sentensi hizi ni za aina gani? (alama 2)
i) Uvutaji wa sigara ni hatari kwa afya
ii) Naomba uwaite wanafunzi wale

c) Onyesha silabi inayowekewa shadda kwenye nomino zifuatazo (alama 2)
i) meza
ii) Maneno

d) Nomino 'Risasi' iko katika ngeli gani? (alama 1)

e) Andika sentensi ifuaayo katika hali yakinishi (alama 2)
Askari wasipopiga doria wala kushirikiana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama.

f) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya alama za mtajo.(alama 2)

g) Andika katika wakati ujao hali timilifu (alama 2)
Wanafunzi walifanya mtihani wa mwigo

h) Tunga sentensi mwafaka ukitumia kielezi cha:- (alama 2)
i) Namna kiigizi
ii) Cha mahali

i) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. (alama 4)
Mwanasiasa mwingine amepoteza kiti chake cha ubunge.

j) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya kiambishi ndi-(alama 2)

k) Onyesha kishazi huru na tegemezi katika sentensi hii. (alama 2)
Kuimba ambako kutavutia kutashinda tuzo

l) Tunga sentensi yenye fungu tenzi lenye muundo ufuatao (alama 2)
tS + T + N

m) Andika kwa usemi wa taarifa (alama 2)
Mama watoto aliuliza, "mbona mnajikunyata kama mayatima".

n) Badilisha vitenzi vifuatavyo viwe katika hali ya kutendeka. (alama 2)
i) kwea
ii) dhuru

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

o) Tunga sentensi sahihi ukitumia kihisishi cha kukataa. (alama 2)

p) Bainisha aina za nomino zilizotumika katika sentensi ifuatayo (alama 3)
Kikosi cha askari kiliabiri ndege hadi ujerumani

q) Kanusha kwa umoja (alama 2)
Mkilia mtapewa maziwa

r) Andika kwa udogo hali ya wingi (alama 2)
Ngoma imepigwa na msichana yule mpaka imepasuka.

s) Unda kitenzi kutokana na nomino ifuatayo. (alama 1)
Taifa

4. **ISIMU JAMII (AL 10)**
Eleza makosa matano yanayoweza kutokea wakati wa mazungumzo. (alama 10)

## Set14``

**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

**SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI**

1. "Mjukuu wangu, masomo ni jambo muhimu sana. Ufikapo shuleni na kuanza maisha ya shule ya upili, usijingize katika mambo ya dunia anasa na raha nyingi. Vifanye vitabu rafiki wa karibu. Wasikize waalimu na uzingatie wanayoyasema, saidiana na wenzako na utie bidii za mchwa katika masomo. Kumbuka kuwa elimu ndio ufunguo wa maisha mema hapo usoni."

**Maswali**

a) Tambua kipera cha fasihi simulizi kinachohusishwa na kifungu hiki. (alama 2)

b) Taja sifa za kipera hiki. (alama 8)

c) Taja umuhimu wa kipera hiki katika jamii. (alama 8)

d) Matumizi ya kipera hiki huwa na lengo gani katika maisha ya kila siku katika jamii? (alama 2)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**SEHEMU YA B: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

2. "Nashangaa vile kwetu tunavyoabudu watu hao wasiojali

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Fafanua hulka za msemewa. (alama 6)

c) Jadili ukweli wa kauli hii. (alama 10)

3. Ndoa ni asasi inayokumbwa na changamoto kadhaa katika jamii ya leo. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi zifuatazo. (alama 20)

a) Mke wangu

b) Maeko

c) Mwana wa Darubini

d) Maskini Babu yangu

**SEHEMU YA C: RIWAYA - KIDAGAA KIMEMWOZEA**

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

4. "Tunaposherehekea uhuru wetu tunayo furaha tele maana idili na juhudi za watangulizi wetu hazikuwa za bure"
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   b) Kwa kurejelea riwaya nzima onyesha kinyume cha kauli hii. (alama 10)
   c) Onyesha sifa za mzungumzaji katika riwaya (alama 6)
5. Jadili mchango wa wahusika Imani na Amani katika ujenzi wa jamii mpya(alama 20)

**SEHEMU YA D: MSTAHIKI MEYA**

6. Jina si kitu. Tumbo ndilo muhimu. Tumbo lako na jamaa zako. Watoto wako.
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
   b) Taja mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
   c) Eleza sifa zozote nne za mzungumzaji. (alama 8)
   d) Dondoo hili linadokeza maudhui fulani katika tamthilia. Yataje na utoe mifano mingine miwili inayothibitisha maudhui hayo. (alama 6)
7. Jadili mbinu na mikakati wanayotumia wanacheneo kupambana na uongozi dhalimu wa Baraza la jiji la cheneo. (alama 20)

**SEHEMU YA E: USHAIRI (AL 20)**

8. **Siafu wamekazana**

Nyoka amegutuka, ndani ya shimo kutuna,
Tena amekasirika, hasira zenye kununa,
Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Shimoni ataondoka, hilo nataja kwa jina,
Nyoka anajuwa fika, siafu wakiungana,
Nguvu zao zaongezeka, shimoni watagomana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Siafu wakijishika, mshiko kushikamana,
Kwamba wanampeleka, sultani wao bwana,
Shimoni wanapofika, nyoka la kufanya hana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika

Siafu wanapofika, na nyoka wakikutana,
Nyoka hawezi kufoka, huwa ametulizana,
Ndipo nyoka huondoka, na wana wakilizana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika

Kupo na kukanganyika, hilo na natujue sana,
Nyoka anapoondoka, siafu hulaliana,
Huuma hupumzika, hapo hakutafanana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Nyoka akishaondoka, na siafu hujazana,
Shimoni wakipeleka, vyakula kutiliana,
Ndilo walilotaka, wale kwa kutulizana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.
(S. Abdu Kandoro)

for freepast papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Maswali**

a) Shairi hili linazungumzia nini? (alama 2)

b) Ukitumia vigezo vifuatavyo, eleza aina za shairi hili. (alama 2)
   i) Vipande
   ii) Vina

c) Bainisha matumizi manne ya Jazanda katika utungo huu. (alama 4)

d) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. (alama 4)

e) Onyesha mtunzi alivyotumia kibali chake cha utunzi katika ubeti wa pili. (alama 4)

f) Fafanua umuhimu wa mkarara wa shairi hili. (alama 4)

## set15

**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

---

1. Lazima
   Siku za hivi karibuni imekuwa kawaida kwa wanafunzi wa shule ya upili ya Matumaini kusokotwa na tumbo baada ya kila mlo. Ukiwa katibu wa Baraza la Wanafunzi matokeo ya uchunguzi wenu.

2. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali:
   Atanguliaye kisimani hunywa maji maenge

3. Matokeo mema ya mtihani wa katika shule yoyote ya humu nchini hutegemea juhudi za mwalimu mkuu pekee Jadili.

4. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo:
   ...mwishowe nilikuja kungamua kwamba jitihada za wenzangu ndizo zilizonisaidia kuvuka daraja hiyo.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**Set15**

**102/2**

**KISWAHILI**

**Karatasi ya 2**

**(LUGHA)**

---

Tunapoakisi hatua ambayo mfumo wa kiteknohama umepiga misamba, kizazi cha vichakazi (facebook) kimetoweka na kupisha kile cha kututumiwa (GMO). Sidhalilishi hivi vikembe na vijikembe vya kututumuliwa japo kunao wenye falfasa hasi kuhusu vikembe hivi. Vijetegemeo mji wao ja waso haya.Hivi vya kutitimuliwa vina mitindo anuai ya kujinakia.Kama wewe si kufu au lahiki yao basi wewe jua bayana kuwa umepitwa na wakati. Utembeapo katika vitongoji vya janibu hizi si Gitau hadi Kaanwa, si Thuchi hadi Mutuati...sisemi Mukothima, utapatana na vikembe HIVI VYA KUTUTUMULIWA. Barobaro hujivika magwanda yanayoonekana kama yatabambuka wakati wowote na kuacha wazi sehemu tunazotegemea.

Vijembe navyo huwa vimejisetiri nusu kwa vijigwanda ambavyo vimeundwa kutoka kwenye shashi. Wafahamu shashi?Kile kitambaa kidogo cha kupangusia pua. Japo mimi vizazi hivi huviona maridadi na anisi, ni yakini kwamba maadili yamewapaa kabisa. Maghulamu wa kukutumuliwa hutembea kwa miondoko au kwa kudakia ukipenda. Zamani nikiwa mdogo tulivaa kaptura na shati za kawaida.Tulijinakia kuchezea matope huku tukivaa nguo safi siku ya Dominika pekee.

Vikembe vya kututumuliwa daima vina vidubwasha maskioni vikiburudika kwa mahadhi ya miziki kutoka kwenye simu zao za ruhunu. Hata kikutane na nani au nani sharti ampishe njia.Enzi zetu mwalimu hakuwa akifanya mambo mengine kama vile kula aina fulani ya chakula sisemi hata kwenda haja. Ukipatana naye njiani wee! Sharti utafute mahali ujifiche mpaka mwalimu apite.Vikembe vya kututumuliwa huwa tunaviheshimu sana. Mara nyingi vitakuona vipi na huku vikembe na vijikembe hutembea huku vimepatikana kama mwanakima na mamake. Waso haya wana mji wao.

Ukikutana nvyo njiani utatamani kurudisha saa yako ya maisha nyuma kidogo. Lakini ndugu, ujajani moshi, ukienda .. Hubagui baina ya vikembe na vijikembe kwani wote vipuli vimebanwa katika sikio moja na kama si moja kijikembe cha kututumuliwa huwa na kipuli kirefu kifikiapo hadi begani.Kijikembe hutembea huku kimesetiri miguu yake kwa jumu yake kwa jumu ambazo zimefika hadi kwenye goti. Na visigino je? Yuatembeahuku akihofu ardhi isibonyee au kuseteka./

Enzi zetu kila baada ya shughuli za shule jioni tulikuta faradhi za kila nui zatusubiri. Mojawapoilikuwa kuwapeleka mifugo malishoni. Kizungumkuti kilikuwa pale ambapo katika michezo yetu ya vijana, ng'ombe wataishia katika shamba la jirani. Jioni hiyo sharti uyatayarishe sisemi makalio kwa utovu wa tafsida Lakini mijeledi itazuru hapo si katiyi.

Vile vikembe vyetu vya kututumuliwa vitakuwa pengine kwenye runinga au kwenye simu zao za rununu na wakati mwingine vimepakata vipakatalishi huku vikibovya vidude hapa na pale. Kila shughuli yao huwa ya mwendo wa pole pole havina mchapuo. Vinyonge hivi si kama vya enzi ya mababu zetu ambao walikuwa wakichapa mpira juu na kuketi kunusa ugoro huku wakisubiri mpira

for freepast papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

urudi ndiposa waendelee na mchezo wao. Vikembe vya kutumuliwa huupisha tu na kikiteleza na kuanguka kidogo basi, mchezo umekoma hadi kipelekwe si zahanatini Lakini katika hospitali kuu ya daraja latano.

Kila jumapili jirani yangu alikuwa na zamu ya kushughulikia kichwa change kwa wembe wake. Hakuwa na shufaka au huruma ukipenda. Kichwa kilibaki kama kupe. Usishtuke kuviona vikembe vya kututumuliwa vichwa vyao vina ukwasi wa nywele si kipilipili bali kama za Bob Marley. Naona kana kwamba siku hizi kunz uhaba wa vinyoleo

Sisemi kizazi kimetukinai, hata chembe. Ni kwa kiteule kwa hivyo tusikipurukushe au kukinyanyapaa. Kila uchao lawana zaradidiwa kuhusu kizazi hiki. Haya ni mambo mazito ja jabali na hivyo basi kinachobaki ni kukihusisha katika ushaui na nasaha. La sivyo sisi wenyewe ndio tutakuja kulio kilio cha mbwa mdomo juu.

**Maswali**

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 2)

b) 'Kizazi chetu kimekosa maadili.' (alama 3)
Thibitisha kwa mujibu wa taarifa hii.

c) Eleza tofauti nne ambazo mwandishi ameangazia kati ya kizazi cha zamani na kile cha kisasa. (alama 4)

d) Mwandishi anamaanisha nini kwa : (alama 3)
   i. ...umepitwa na wakati
   ii. ...vimeundwa kutoka kwenye shashi
   iii. mijiledi itazuru hapo si katiti

e) Eleza maana za maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 3)
   i. kujinaki
   ii. faradhi
   iii. tusikipurukushe

for freecsepast papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

**2. SEHEMU B:UFUPISHO(ALAMA 15)**

Inaridhisha kuyasikia mengi kuhusu mikakati ambayo serikali imeanzisha kuimarisha maendeleo ya nchi.Ni kweli kuwa maendeleo huhitajika kuonyesha mafanikio ya nchi ili kumaliza umaskini nchini.Ni juzi tu serikali imeanzisha ujenzi wa reli ambao umeibua malumbano mengi pamoja na upanuzi wa uwanja wa ndege wa Jomo Kenyatta ukiwa miongoni mwa miradi mengine mingi.

Kuna mipango kabambe ya kuwezesha usafiri wa maji uimarike zaidi katika mto Nile ili manufaa yake pia yaonekane katika eneo la Afrika mashariki sio tu Misri.

Ustawi wa taifa pia umelengwa kwa kupigia debe swala la pesa mashinani ili serikali za gatuzi ziweze kufadhili miradi moja kwa moja bila kutegemea serikali kuu.Na Ikiwa ugatuzi huu utafaulu basi vijana na wanawake washugulikiwe kwa kuwapa mikopo ya kuanzisha biashara ndogo ndogo.

Maendeleo hayawezi kuimarika bila ujenzi na upanuzi a barabara ili kukuza teknolojia ya mawasiliano.Jambo hili litarahisisha usafirishaji wa bidhaa kutoka sehemu moja hadi nyingine.

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

Elimu pia ni kigezo muhimu na msingi thabiti wa kuega uchumi kwa kila nchi.Katika mabara yalioendelea asilimia kubwa ya wnanchi huwa na kiwango cha juu cha elimu.Kwa hivyo ni jambo muhimu kwa serikali kutoa elimu ya bure katika shule za msingi hadi shule za upili.Pia kilimo kipanuliwe kwa kutumia mbinu za kisasa na teknolojia mpya iwezeshe kwa hali na mali mashambani ili kuwaajiri watu wengi katika sekta hiyo.

Azma na matumaini ya kila nchi kuendelea hukabwq na matatizo kwa kuwa Fedha zinazohitajika zinashinda hata bajeti y mwaka mzima ya nchi hizo.Kuna uhaba mkubwa wa wataalamu mbalimbali wenye ujuzi wa kufaa katika sekta nyingi hapa nchini.

Pamoja na kuweko kwa viongozi wenye matumbo makubwa ambao humimina Fedha zenye manufaa kwa wananchi,kuna ukosefu wa vifaa vya kisasa vinavyorahisisha utenda kazi.Vikiwepo huwa duni kulingana na viwango vya maendeleo.

Kuna pengo kubwa sana kati ya matajiri na maskini hivi kwamba itachukua muda kuyashawishi matabaka haya mawili.Takwimu sahihi ya mahitaji ya watu katika maeneo fulani yahitajika ili serikali iweze kusambaza miradi kulingana na jinsi eneo lilivyo.Wamiliki ardhi kubwa wamekuwa na mzizi iliyokita kwenye ulingo wakisiasa hivi kwamba ni vugumu na hatari kugusia suala la umiliki wa ardhi.

a) Ni juhudi zipi zilitiliwa maanani kuimarisha uchumi? (maneno 55) (alama 6,1 ya utiririko)
   Matayarisho
   jibu
b) Kwa maneno yasiyozidi 55 fupisha aya tatu za mwisho. (alama 7, 1 ya utiririko)
   Matayarisho
   Jibu

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

## 3. SEHEMU YA C : MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Andika mifano minne ya vitenzi vya silabi moja katika ya kutendesha. (alama 2)
b) Unda sentesi yenye muundo ufuatao : (alama 2)
   KN(N+V),KT(t+ V+E)
c) Taja sifa inayotofautisha sauti / ny/na/ng/ (alama 2)
d) Ainisha vihusishi katika sentensihii :
   Tulichakura tarakilishi ya mwalimu iliyokuwa kando ya dawati baada ya mtihani kukamilika.

   (alama 3)
e) Tumia kiunganishi seuze / sembuse katika sentensi. (alama 2)
f) Eleza maana tatu za sentensi hii.
   Chakula kingine kimeliwa na wageni. (alama 3)
g) Ainisha vitenzi katika sentensi hii.
   Hawa ndio wageni tuliokuwa tukingojea kwa hamu. (alama 2)
h) Hizi ni mofimu za aina gani? (alama 3)
   Kiwavi
   Miwani
   Karatasi
i) Akifisha

   Toka nje au niku nyanya akaamuru murithi (alama 3)
j) Changanua kwa kutumia vishale.

Swali hilo lilikuwa rahisi sana. (alama 4)

k) Yakinisha
Chakula hakiko tayari hivyo wageni wasinawe mikono. (alama 2)

l) Ainisha vishazi katika sentensi hii.
Kama nitamkuta nyumbani nitamshauri asome kwa bidii. (alama 3)

m) Tunga sentensi ya neno moja yenye sehemu zifuatazo : (alama 3)
Kikanushi
Hali timilifu
Mtendewa
Kitenzi cha silabi moja
Kauli ya kutendesha
Kiishio

n) Andika katika usemi wa taarifa :
"Mkishinda timu hii leo nitamtuza."Mkufunzi akatwambia. (alama 3)

o) Tambua yambwa na ueleze ni za aina gani.
Wazazi waliwanunulia wanafunzi bora zawadi nyingi kwa hundi. (alama 2)

p) Nyambua neno hili katika kauli ya kutendesha. (alama 1)
Jua

4. **SEHEMU D : ISIMU JAMII (ALAMA 10 )**

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali
Anachukua ile ngoma kijana Rooney,
Kwake chicharito...anachenga moja , mbili
Hatari! Hatari! Hatari kwenye lango..

a) Hii ni sajili gani? (alama 2)
b) Eleza sifa nane za sajilli hii. (alama 8)

**Set15**
**102/3**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**

---

Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine : Ken Walibora , S.A Mohammed, Kanda la Usufi : Rhoda Nyaga

1. "Tutaondoka ndio, Lakini elewa uchungu wa mwana ajuaye ni mzazi."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Taja na utolee mfano tamathali ya useme iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
   c) Eleza sifa nne za msemewa. (alama 4)
   d) Eleza madhara ya mapenzi miongoni mwa wanafunzi. (alama 10)

**RIWAYA , Kidagaa kimemwozea : Ken Walibora**

2. Eleza namna mbinu zifuatazo zilivyotumiwa na mwandishi wa Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea
   a) Sadfa
   b) Kinaya (alama 20)
3. "..unautukanisha ukoo wetu mtukufu. Naona aibu kukuita ndugu yangu."
   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Ni tamathali gani imejitokeza katika usemi huu? (alama 2)
   c) Bainisha na ueleze migogoro kati ya ndugu hawa. (alama 6)
   d) Fafanua umuhimu wa msemewa katika dondoo hili. (alama 8)

For free pastpapers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**TAMTHILIA.Mstahiki Meya : Timothy Arege**

4. "Haitokani na maji Sir. Ni harufu ya taka barabarani sir."
   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Eleza yaliyopelekea kuwepo kwa harufu hii. (alama 4)
   c) Msemaji ana umuhimu gani? (alama 4)
   d) Harufu hii ni ishara ya uozo uliotawala jamii nzi,a ya Cheneo. Fafanua aina zingine za uozo zinazopatikana katika tamthilia hii. (alama 8)
5. Jadili jinsi maudhui yafuatayo yamejitokeza katika tamthilia ya Mstahiki Meya.
   a. Ukoloni mamboleo (alama 10)
   b. Unafiki (alama 10)

**FASIHI SIMULIZI**

6. a) Nini maana ya maigizo katika Fasihi Simulizi. (alama 2)
   b) Taja vipera vyovyote vine vya maigizo. (alama 4)
   c) Fafanua sifa za mwigizaji bora. (alama 8)
   d) Taja vikwazo vinavyoweza kukumbuka utanzu wa maigizo. (alama 6)

7. **USHAIRI**

Jicho , tavumiliaje , kwa hayo uyaonayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo?
Kwacho, litajalo nalije, nimechoka vumiliyo
Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhui tusikiayo
Nayo , visa na mauko, wanyonge yawakutayo
Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo
Naandika!

Hawa, wanatulimiya, dhiki wavumiliayo
Hawa, mamiya, na mali wazalishayo
Hawa, ndo wanaoumiya, na mafia wakutayo
Naandika!

Hawa, sioni wengine , kwao liko angamiyo
Hawa, huwapa unene,watukufu wenye nayo
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waitikayo
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo
Bado, tofauti sana, kwa pato na mengineyo
Bado, tuling'owe shina, ulaji pia na choyo
Naandika!

a) Ni nini shabaha ya mwandishi aliyetunga shairi hili? (alama 2)
b) Eleza kwa kutoa sababu bahari zinazopatikana katika shairi hili. (alama 4)
c) Je, mwandishi ametumia mbinu zipi ili kutimiza mahitaji ya kiarudhi? (alama 4)

d) Mtunzi wa shairi hili anawasilisha ujumbe gani katika ubeti wa kwanza? (alama 2)
e) Eleza sura ya shairi hili. (alama 4)

for free past paper visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

f) Taja mambo yanayomkera mshairi huyu? (alama 2)

g) Eleza maana za maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 2)

i. zuiliko

ii. mauko

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

For More Papers and Marking Scheme at a Small Fee: Website: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479